# JINSIA INAVYOWAKILISHWA KATIKA NYIMBO ZA KAMPENI ZA KISIASA KATIKA KAUNTI YA BOMET NCHINI KENYA

**NANCY CHEPKEMOI KONES**

**Tasnifu hii Imewasilishwa Katika Shule ya Mafuzu Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Egerton.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**JULAI, 2021**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halijatolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote kile.

**Sahihi**.................................................... **Tarehe**...28/5/21...................

**Nancy Chepkemoi Kones**

**AM 12/3529/13**

**IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

**Sahihi**.......................................... **Tarehe**...31/5/2021...................

**Dkt. Abdulrahim Hussein Taib Ali**

**Chuo Kikuu cha Egerton**

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu**

**Sahihi**.......................................... **Tarehe**...28/05/2021...................

**Dkt. Mayaka Gwachi**

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu**

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

**HAKILINZI**

**© 2021, Nancy Chepkemoi Kones**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri au kuitoa tasnifu hii kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mume wangu mpendwa Bwana Mhandisi Joseph Kones pamoja na watoto wetu Joan, Duncan, Brian, Diana, Marion na Collins.

## SHUKRANI

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo na rehema zake nyingi alizonitunukia nilipokuwa nikiishughulikia shahada ya uzamili. Yeye alinipatia nguvu za kipekee na kuniwezesha kufika tamati katika kazi hii.

Nawashukuru sana wasimamizi wangu Dkt. James Mayaka Gwachi na Dkt. Abdulrahim Hussein Taib Ali kwa kukubali kunielekeza na kunivumilia katika kazi hii hadi nikaikamilisha. Bila nyinyi nisingekuwa na uwezo wa kuitamatisha kazi hii. Kazi hii haingeendelea na kufikia mwisho bila mafunzo na uongozi wenu. Mwenyezi Mungu awateremshie baraka zake za kipekee.

Shukrani zangu za dhati zimwendee Profesa James Onyango Ogola kwa kunitia moyo, kunipa mawaidha na kunisaidia katika masomo haya. Vilevile, ningependa kumshukuru Dkt. Dishon Kweya kwa usaidizi wake. Ulinikwamuana kunipa mwelekeo mwema ulionisaidia katika kazi hii. Nawashukuru pia Dkt. Bartoo na Dkt. Ayodi kwa kunihimiza kuendelea nilipokuwa nikielekea kutamauka.

Nawashukuru marafiki zangu na wanafunzi wenzangu Wanyeki Mwai, Naomi Kimotho, Susan Wairimu, Patrick Wanyama na Pamela Otieno kwa kushirikiana pamoja na kutiana moyo katika masomo yetu. Ningependa pia kuwashukuru marafiki zangu Janice Mutua na Melvin Ouma kwa namna ambavyo mlinisaidia na kunipa moyo katika kazi yangu.

Heko za dhati zimwendee mume wangu mpendwa Bwana Mhandisi Joseph Kones kwa kunikubalia kusoma , kunivumililia nilipokuwa masomoni, kunipa moyo kupambana na kazi hii na mchango wako mwingi katika kazi hii iliyokuwa kubwa. Siwezi kuwasahau watoto wangu kwa kunivumililia na kunitia nguvu katika masomo haya.

Ningependa pia kumshukuru baba yangu marehemu Bwana Samwel Talam na mama yangu Bi. Nelly Talam kwa kunilea kwa njia ya kipekee, kunisomesha na kunipa motisha katika masomo yangu. Shukrani chungu nzima ziwaendee ndugu zangu wote akina Esther Mburu, Elzabeth

Chemiron, Emily Lang'at, Mwalimu Nelson Mutai, Mhandisi Jasper Mutai, Philemon Mutai, Dkt. Mhandisi Wesley Mutai, Dkt. Norah Lang'at , Lilian Rotich, Leonard Mutai na Julius Mutai kwa kunipa nguvu ya kipekee iliyoniwezesha kuhitimu masomo haya. Nawashukuru wale wote waliochangia katika mwendo huu wote hadi nikafanikiwa kupata shahada ya uzamili. Mungu awabariki.

## IKISIRI

Nyimbo ni njia bora ya mawasiliano katika jamii. Nchini Kenya, nyimbo za kisiasa hutumika wakati wa kampeni za uchaguzi wa rais, magavana, maseneta, wabunge, wawakilishi wa wanawake na wajumbe wa wadi. Matokeo ya uchaguzi wa kitaifa yameonyesha kuwa wanaume wengi huchaguliwa kuliko wanawake. Utafiti ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Ulichunguza iwapo nyimbo zilisababisha kuchaguliwa kwa wanaume wengi kuliko wanawake. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchanganua na kufasili namna nyimbo za kampeni za kisiasa zinawakilisha jinsia. Malengo mahususi yalikuwa: Kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha jinsia, kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia na kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu jinsia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubabedume. Mihimili yake ni: Mgawanyo wa mamlaka, uwezo kijinsia na mielekeo kuhusu kila mwanajamii. Huu ni utafiti wa kithamano mkabala wa kifasili. Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ya Bomet iliyoko katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya. Mtafiti alizikusanya nyimbo hamsini na mbili za kisiasa zilizorekodiwa. Alitumia sampuli ya kimakusudi kuteua nyimbo ishirini na mbili za kampeni za kisiasa zilizohusika na jinsia. Wasanii kumi na sita waliimba nyimbo hizo ambazo zikawa deta za kuchanganuliwa. Deta zilikusanywa kwa usikilizaji wa kanda za nyimbo pamoja na mwongozo wa maswali ya mahojiano. Mbinu ya ufasili wa deta ilitumiwa katika utafiti huu. Matokeo yalithibitisha kwamba nyimbo nyingi za kampeni za kisiasa ziliteteа wagombezi wa jinsia ya kiume. Kulikuwa na wimbo mmoja uliodhalilisha jinsia ya kike. Nyimbo nyingi ziliipa hadhi ya juu jinsia ya kiume kuliko ya kike. Wasanii wengine walieleza kwamba kumekucha na tunataka mabadiliko siasani. Utafiti utawanufaisha walimu na wanafunzi wa somo la Fasihi Simulizi. Wanajamii watafahamu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Wasanii wa nyimbo za kampeni za kisiasa wataelekezwa katika ubunifu wao. Wagombezi, wawe wanaume au wanawake, watawaelekeza wasanii kwa namna ambavyo wangetaka kuzibuni aina fulani za nyimbo zitakazotumika katika kampeni zao za kisiasa matokeo yapate kuwa mema.

# ABSTRACT

Songs are an effective means of communication in society. Political songs are used in Kenya during campaigns for elections of president, governors, senators, members of parliament, women representatives and members of county assemblies. General elections' results have shown that more men than women are elected. The study analyzed how gender is represented in political campaign songs in Bomet County. The research examined if the songs contributed to the election of more men than women. The broad objective of the study was to analyze and interpret how gender is represented in political campaign songs. The specific objectives were: To interpret how the content of political campaign songs represents gender, to explain how political campaign songs present gender power relationship and to interpret how political campaign songs presents what ideology explains about gender. This research was guided by Hegemonic Masculinities theory. Its tenets are: Division of power, gender strength and societal attitudes concerning each of its members. It is a qualitative study interpretive perspective. It was carried out in Bomet County in the Rift Valley region of Kenya. The researcher collected fifty two recorded political songs. Purposive sampling was used to identify twenty two political campaign songs based on gender. Sixteen artistes sang those songs that were analyzed. Listening to recorded songs along with an interview guide were used to collect data. Intrepretive data analysis was used in this study. The results indicated that majority of the political campaign songs supported male politicians. One of the songs downgraded the female gender. Many songs bestowed higher position on men than women. Some artistes explained that this is the time to bring change in politics. The study will benefit teachers and students of Oral Literature. The society will understand how gender is represented in political campaign songs. It will be a guide to the artistes of political campaign songs as they compose their songs. Political campaigners either men or women, will guide the artistes on how to compose certain songs to be used in their political campaigns for good results.

## YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** ........ **i**

**HAKILINZI** ........ **ii**

**TABARUKU** ........ **iii**

**SHUKRANI** ........ **iv**

**IKISIRI** ........ **vi**

**ABSTRACT** ........ **vii**

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ **xi**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Usuli wa Mada ........ 1

1.1.1 Matokeo ya Uchaguzi Mkuu Nchini Kenya ........ 2

1.2 Suala la Utafiti ........ 3

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 4

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 5

1.7 Maelezo ya Istilahi ........ 5

**SURA YA PILI** ........ **6**

**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** ........ **6**

2.1 Utangulizi ........ 6

2.2 Mapitio ya Maandishi ........ 6

2.2.1 Maandishi Kuhusu Mada ya Utafiti ........ 6

2.2.2 Dhima za Nyimbo za Kisiasa ........ 14

2.3 Misingi ya Nadharia ........ 20

**SURA YA TATU** ........ **21**

**MBINU YA UTAFITI** ........ **21**

3.1 Utangulizi ..... 21
3.2 Muundo wa Utafiti ..... 21
3.3 Eneo la Utafiti ..... 21
3.4 Ukusanyaji wa Deta na Uteuzi wa Sampuli ..... 21
3.5 Vifaa vya Ukusanyaji wa Deta ..... 23
3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Deta ..... 23
3.6.1 Mfumo Maalum wa Uchanganuzi wa Deta ..... 24

**SURA YA NNE ..... 26**
**UCHANGANUZI NA UFASILI WA DETA ..... 26**
4.1 Utangulizi ..... 26
4.2 Mpangilio wa Deta ..... 26
4.2.1 Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Jinsia. ..... 26
4.2.1.1 Mgawanyo wa Mamlaka ..... 27
4.2.1.2 Hitimisho ..... 41
4.2.2 Mahusiano ya Uwezo Kijinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa ..... 41
4.2.2.1 Siasa ya Kijinsia ..... 42
4.2.2.2 Kinyang’anyiro cha Kiti cha Urais ..... 42
4.2.2.3 Sifo ya Muungano wa NASA ..... 47
4.2.2.4 Kampeni ya Kiti cha Ugavana ..... 48
4.2.2.5 Kampeni ya Kiti cha Useneta ..... 51
4.2.2.6 Kampeni ya Kiti cha Ubunge ..... 53
4.2.2.7 Kampeni ya Kiti cha Ujumbe wa Wadi (MCA) ..... 56
4.2.2.8 Hitimisho ..... 58
4.2.3 Itikadi Kuhusu Jinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa ..... 58
4.2.3.1 Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kiume ..... 58
4.2.3.2 Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kike ..... 72
4.2.3.3 Hitimisho ..... 73

**SURA YA TANO** ........................................................................ **75**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........................................................................ **75**
5.1 Utangulizi ........................................................................ 75
5.2 Muhtasari ........................................................................ 75
5.3 Matokeo ya Utafiti ........................................................................ 76
5.4 Mafanikio ya Utafiti ........................................................................ 78
5.5 Matatizo ya Utafiti ........................................................................ 78
5.6 Hitimisho ........................................................................ 79
5.7 Mapendekezo ........................................................................ 80

**MAREJELEO** ........................................................................ **82**
**Kiambatisho A: Ramani ya Kaunti ya Bomet** ........................................................................ **87**
**Kiambatisho B: Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Jinsia** ........................................................................ **88**
**Kiambatisho C: Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Wagombezi** ........................................................................ **96**
**Kiambatisho D: Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kulingana na Itikadi Kuhusu Jinsia** ..... **107**
**Kiambatisho E: Mwongozo wa Maswali ya Mahojiano** ........................................................................ **115**
**Kiambatisho F: Kibali Kutoka NACOSTI** ........................................................................ **116**
**Kiambatisho G: Makala Yaliyochapishwa** ........................................................................ **117**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **CORD** | Coalition of Reforms and Democracy |
| **CCM** | Chama cha Mapinduzi |
| **DDDG** | Digital Device Development Group |
| **IJ** | Itikadi kuhusu Jinsia |
| **FM** | Frequency Modulation |
| **FORD** | Forum for Restoration of Democracy |
| **GIS** | Geographic Information Services |
| **IEBC** | Independent Electoral and Boundaries Commission |
| **KANU** | Kenya African National Union |
| **KNC** | Kenya National Congress |
| **MCA** | Member of County Assembly |
| **MM** | Mgawanyo wa Mamlaka |
| **MUK** | Mahusiano ya Uwezo Kijinsia |
| **NARC** | National Rainbow Coalition |
| **NASA** | National Super Alliance |
| **NHIF** | National Hospital Insurance Fund |
| **NWHM** | National Women's History Museum |
| **ODM** | Orange Democratic Movement |
| **POA** | Party Of Action |
| **PNU** | Party of National Unity |
| **SD** | Social Democratic |
| **UDF** | United Democratic Front |
| **URP** | United Republican Party |
| **WCP** | Workers Congress Party |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Nyimbo ni njia bora ya mawasiliano katika jamii. Nchini Kenya, nyimbo za kampeni za kisiasa hutumika wakati wa uchaguzi wa rais, magavana, maseneta, wabunge, wawakilishi wa wanawake na wajumbe wa wadi. Wasanii hubuni nyimbo za kuvisifu vyama na wagombezi wenyewe. Utafiti ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo hizo katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Riordan (2007) aeleza kwamba kuna hisi zenye nguvu zinazoambatana na nyimbo za kisiasa. Nyimbo hizo zina uwezo wa kuwasilisha ujumbe wa siasa. Utafiti ulichunguza iwapo viashiria vya jinsia katika nyimbo zilisababisha kuchaguliwa kwa wanaume wengi kuliko wanawake. Vilevile, utafiti ulimakinikia kuchunguza jinsi gani jinsia iliwakilishwa katika nyimbo hizo na namna zilichangia wanaume ama wanawake kuchaguliwa.

Kabila la Kalenjin hujumlisha wanawake na watoto kuwa sawa. Hivyo basi, wanaume huona wanawake kama hawawezi kuwa viongozi.Wanawake wameshawishiwa na wanaume kuwa wanawake wenyewe hawana uwezo wa kuongoza. Kwa hivyo, wanawake wagombezi hudharauliwa na wanawake wenzao. Kuna madai kwamba wanawake wanaweza kuchaguliwa iwapo wanagombea kiti katika chama maarufu kinachoongozwa na mwanaume aliye na ushawishi mkubwa. Marehemu Kipchamba alieleza katika wimbo wake kwamba gari linapokimbia, hakuna wakati magurudumu ya nyuma yanaweza kufikia ya mbele daima. Mtafiti alizichanganua nyimbo za kampeni za kisiasa zilizo na misimamo na mielekeo kama hii.

Kalenjin ni jamii moja ya kikundi cha Nailotiki na ina makabila yafuatayo: Kipsigis, Nandi, Tugen, Marakwet, Keiyo, Pokot, Sabaot na Terik. Wenyeji wa Kaunti ya Bomet ni kabila la Kipsigis. Toru (1984) anaeleza kuwa Kipsigis ni kabila linalotambulika zaidi kuliko makabila mengine ya jamii ya Kalenjin nchini Kenya. Hii ni kwa sababu Wakipsigis walipatana mapema na wakoloni na hata wakati huu wengi wao ni wasomi.

Simatei (2010) aeleza kwamba mipango ya kijamii na kisiasa, baada ya siasa ya vyama vingi nchini Kenya mwaka wa 1992, ilileta ubunifu mwingi katika uwanja wa usanii hasa katika utanzu wa nyimbo. Mwaka wa uchaguzi wa 2002, ulioumaliza utawala wa Hayati Daniel Arap Moi wa miaka ishirini na minne uongozini, kulizuka aina nyingi za muziki wa kisiasa kutoka makabila mbalimbali. Nchini Kenya, nyimbo za kisiasa zimetumika kuelimisha watu kabla na baada ya uhuru. Siasa ni dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa uendeshaji wa masuala ya kijamii katika taifa.Siasa inaweza kutumika kuelezea mahusiano kati ya makundi mbalimbali kama vile siasa ya kijinsia.

### *1.1.1 Matokeo ya Uchaguzi Mkuu Nchini Kenya*

Uchaguzi wa kitaifa wa 1992, Hayati Daniel Arap Moi aliyekuwa rais wakati huo, alishinda katika chama cha KANU. Marehemu Kenneth Matiba wa chama cha FORD-ASILI alichukua nafasi ya pili. Hakukuwa na mwanamke mgombezi aliyewania kiti hicho mwaka huo. Katika uchaguzi wa bunge, wanaume walipata viti mia moja tisini na sita na wanawake walipata sita.

Uchaguzi wa kitaifa nchini Kenya mwaka wa 1997, Hayati Daniel Arap Moi wa chama cha KANU aliongoza na Mwai Kibaki alikuwa wa pili. Charity Ngilu kama mwanamke wa kwanza nchini Kenya na katika Afrika Mashariki, alikuwa wa tano. Alikuwa katika chama cha Social Democratic (DDDG, 1998). Marehemu Waangari Maathai katika chama cha Labour alikuwa namba kumi na tatu.

Mnamo 2002, shughuli za kisiasa zilitajwa kuwa za haki na huru na Jamii ya Kimataifa. Kukazuka makundi mengi maarufu ya wanawake. Malengo yao mahususi yalikuwa kuelimisha jamii kuhusu uwezo wa wanawake siasani, uimarishaji wa wanawake wagombezi na wapigaji kura, na elimu kuhusu usawa wa jinsia. Wanawake washindi katika uchaguzi huo walikuwa pamoja na Charity Ngilu, Beth Mugo na Martha Karua. Serikali mpya ilipoundwa mwezi Machi 2003, uwakilishi wa wanawake katika idara ya serikali ilikuwa hivi: Baraza la Mawaziri: wanawake watatu kwa wanaume ishirini na watatu, Manaibu wa Mawaziri: wanawake wanne kwa wanaume ishirini na wanne, Makatibu wa kudumu: wanawake tisa kwa wanaume ishirini na wanne na Wakurugenzi wa idara: wanawake watatu kwa wanaume ishirini na saba.

Uchaguzi wa 2007, mshindi alikuwa Mwai Kibaki wa chama cha PNU na wa pili alikuwa Raila Odinga wa chama cha ODM. Nazlin Umar katika chama cha WCP of Kenya alikuwa wa sita (IEBC, 2007). Wanawake wabunge waliongezeka hadi ishirini na mmoja kati yao kumi na watano waliochaguliwa na sita walioteuliwa.

Uchaguzi wa kitaifa wa 2013 ulifanywa chini ya katiba mpya iliyopitishwa 2010. Huu ni uchaguzi ulioshughulikiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Kulingana na IEBC, Uhuru Kenyatta wa Muungano wa Jubilee aliongoza na Raila Odinga wa CORD alikuwa wa pili. Martha Karua wa NARC-Kenya, kwa wagombea wanane, alikuwa namba sita (Commonwealth Observer Group, 2013). Katika bunge, wanaume mia mbili na tisini na wanawake kumi na sita walichaguliwa.

Uchaguzi wa kitaifa wa 2017, Uhuru Kenyatta wa Muungano wa Jubilee alikuwa wa kwanza na Raila Odinga wa Muungano wa NASA, alichukua nafasi ya pili. Hakukuwa na mwanamke aliyegombea kiti cha urais. Magavana wa kike watatu walichaguliwa kwa mara ya kwanza nchini kama ifuatavyo: Charity Ngilu kutoka Kaunti ya Kitui, Ann Waiguru kutoka Kaunti ya Kirinyaga na marehemu Dkt. Joyce Laboso kutoka Kaunti ya Bomet. Vilevile, maseneta wa kike watatu walichaguliwa kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo: Margaret Kamar wa Kaunti ya Uasin Gishu, Susan Kihika wa Kaunti ya Nakuru na Fatuma Dullo wa Kaunti ya Isiolo. Katika bunge la kitaifa, wanawake walikuwa arubaini na saba kwa mia mbili themanini na tisa. Baada ya kila uchaguzi, wabunge kumi na wawili huteuliwa kutoka makundi matatu maalumu, yaani, kundi la vijana, la walemavu na la wanawake. Wao huchukuliwa kama watu wasioweza kushindana kwa usawa na wagombezi wengine.

### 1.2 Suala la Utafiti

Matokeo ya uchaguzi wa kitaifa nchini Kenya, yameonyesha kuwa wanaume wengi huchaguliwa kuliko wanawake. Utafiti ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Ulichunguza iwapo nyimbo zilisababisha kuchaguliwa kwa wanaume wengi kuliko wanawake.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua na kufasili namna nyimbo za kampeni za kisiasa zinawakilisha jinsia katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Malengo mahususi ni pamoja na:

(i) Kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la jinsia katika Kaunti ya Bomet.

(ii) Kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia katika Kaunti ya Bomet.

(iii) Kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu jinsia katika Kaunti ya Bomet.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

(i) Maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilishaje suala la jinsia katika Kaunti ya Bomet?

(ii) Nyimbo za kampeni za kisiasa husawirije mahusiano ya uwezo kijinsia katika Kaunti ya Bomet?

(iii) Nyimbo za kampeni za kisiasa huelezaje suala la itikadi kuhusu jinsia katika Kaunti ya Bomet?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Nyimbo huelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo, utafiti huu utawanufaisha walimu na wanafunzi wa somo la Fasihi Simulizi. Utachangia katika kupanua tasnia ya nyimbo kwani nyimbo za kampeni za kisiasa zina nafasi katika jamii. Utatoa mchango kwa wasanii wakati wanapotunga nyimbo hasa wakati wa kampeni za kisiasa huku wakizingatia suala la jinsia. Wanajamii watafahamu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Kwa mfano, wasanii wa nyimbo za kampeni za kisiasa wataelekezwa katika ubunifu wao. Wanasiasa watakaowania viti mbalimbali watafaidika. Kwa mfano, wagombezi wawe wanaume au wanawake wanaweza kuwataka wasanii kuzibuni aina fulani za nyimbo. Nyimbo hizo zitatumika katika kampeni zao za kisiasa ili matokeo yawe mema.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulishughulikia nyimbo za kampeni za kisiasa kama deta ya kimsingi. Ulijikita zaidi kuchunguza namna jinsia inavyowakilishwa katika nyimbo hizo. Viashiria vya jinsia vilitumika kama kurunzi. Mtafiti alishughulikia maana na fasili ya maana fiche vya viashiria hivyo. Nyimbo za kampeni za kisiasa ziliimbwa katika Kaunti ya Bomet katika ngazi ya urais, ugavana, useneta, ubunge na ujumbe wa wadi kuanzia 1992 hadi 2017. Kuanzia 1992 hadi 2007, hakukuwa na viti vya ugavana, useneta na uwakilishi wa wanawake. Kulikuwa na uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani (wajumbe wa wadi). Utafiti ulishughulikiwa kuanzia 1992 ili kuchunguza iwapo maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa ni sawa hadi 2017 au yamebadilika.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

**Itikadi**: Ni mfumo wa mawazo yanayochukuliwa na jamii husika kuhusu tajriba ya maisha.

**Jinsia**: Ni hali ya kuwa mume au mke kulingana na jamii inayohusika.

**Mfumodume**: Hii ni namna ambavyo jamii imempa mwanaume hadhi na uwezo wa kumtawala mwanamke.

**Nyimbo za kisiasa**: Nyimbo ambazo hulenga kuwahamasisha na kuwaleta watu pamoja kisiasa.

**Nyimbo za kampeni za kisiasa**: Nyimbo ambazo hulenga kuwashawishi watu wampigie mgombezi au chama kura.

**Ubabejike**: Dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa kijamii ambapo itikadi inayotawala inawakuza wanawake.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alieleza kuhusu mambo yafuatayo: Nyimbo kwa jumla katika jamii, nyimbo za kisiasa katika harakati za uchaguzi, maandishi kuhusu mada ya utafiti, madhumuni ya kampeni, dhima za nyimbo za kisiasa na nadharia ya Ubabedume ambayo ilitumika katika utafiti huu.

## 2.2 Mapitio ya Maandishi

Mtafiti aliyamulika maandishi ya awali yanayohusiana na utafiti huu. Kupitia maandishi haya, mtafiti alipata habari aliyohitaji inayohusiana na mada yake ya utafiti. Maandishi haya hujuza mambo yaliyofanywa kuhusu mada husika na yale ambayo hayajafanywa.

### *2.2.1 Maandishi Kuhusu Mada ya Utafiti*

Mulokozi (1989) aliainisha ushairi kama mojawapo ya tanzu sita za fasihi simulizi. Amegawa ushairi katika mafungu mawili ambayo ni nyimbo na uwasilishaji. Anaeleza kwamba kutokana na hali mbalimbali za kijamii, inawezekana kuainisha aina mbalimbali za nyimbo kama vile: Nyimbo za kusifu na kupongeza kama za kisiasa, za kukashifu na za kutumika kwa minajili ya kuburudisha kama za sherehe. Kuna nyimbo za arusi na taarabu za kushauri au kutoa wosia kama za tohara, za kuomboleza, za kushajiisha kama za vita, za kutiana moyo kama za mavuno, za dini na za watoto. Nyimbo katika fasihi simulizi ni za kuburudisha, kuelimisha, kufunza, kuonya, kuelekeza, kuliwaza, kusifia kitu au mtu katika jamii, kudumisha tamaduni za jamii, kukuza talanta na sanaa katika jamii na kutumika katika mbinu nyingi za kifasihi kama vile hadithi. Utafiti uliofanywa una uhusiano na wa Mulokozi kwa vile ulihusika na nyimbo. Tofauti ni kwamba Mulokozi alitafiti juu ya ushairi kwa jumla. Mtafiti alisaidika alipopanua ushairi kwa kuchunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Mazigwa (1991) aeleza kwamba nyimbo ni kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi, hazina ambayo huhifadhi na kusambaza mawazo juu ya maisha ya binadamu na maendeleo yake. Kwa kufanya hivyo, nyimbo huweza kutoa mafunzo mbalimbali kama vile kuonya, kukosoa na

kuadilisha jamii. Kazi iliyofanywa na Mazigwa inaambatana na utafiti huu kwani alishughulikia dhima za nyimbo. Tofauti ni kwamba mtafiti alitafiti kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Alifaidika kwa kutafiti zaidi kuhusu aina moja ya nyimbo, yaani, nyimbo za kampeni za kisiasa.

Mazrui (1992) aeleza kwamba mahusiano ya kijamii hujengwa kutokana na historia, mazingira na shughuli za watu za kila siku na imani yao. Watu wa jamii moja aghalabu husikilizana kwa lugha, mila na desturi. Misingi hiyo ya utamaduni na utamaduni wenyewe huwa ni vigezo maalum vya kumfanya mtu aitambue nafasi yake katika jamii na vilevile kutambua wajibu wake na majukumu yake. Sifa moja ambayo hubainisha nyimbo ni matumizi yake ya lugha hasa zile tamathali za usemi kama vile tashbihi, methali, semi, jazanda, taashira na majina ya majazi. Hii inafanya utanzu uweze kuchunguzwa kwa makini kiusomi kwa kuchanganua ufani wake kupitia lugha iliyotumika. Huu ni utafiti unaohusiana na uliofanywa kwa vile imeshughulikia nyimbo. Tofauti yao ni kwamba namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa ilifanywa katika utafiti huu. Mtafiti alipiga hatua zaidi kwa kuchunguza namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la jinsia.

Katika fasihi, maneno hutumiwa kiufundi au kisanii ili kuwasilisha ujumbe na maudhui mbalimbali kuhusu maisha ya wanadamu. Fasihi ya Afrika ni utanzu uliokomaa sasa na kujipambanua miongoni mwa fasihi za ulimwengu. Kitabu cha Okpewho (1992) kinahusu fasihi katika Afrika na fasihi ya Kiafrika. Fasihi ya Kiafrika bado inaendelea kupata mengi kutoka katika masimulizi, na utafiti mwingi hauna budi kufanyika kuhusu yale ambayo hayajaandikwa na wala hayafahamiki miongoni mwa wale ambao hasa hupata maarifa hususan katika maandishi. Fasihi simulizi ni kioo cha jamii kwa sababu maudhui na hali halisi za utamaduni huhusishwa. Kupitia kwa nyimbo, jamii inajifunza, inacheka, inaomboleza, inafarijiana, inapeana moyo na kupitisha taarifa za siri. Tafiti hizi zinahusiana kwa maana zote huhusika na fasihi ya Kiafrika lakini tofauti yao ni kwamba namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya ilitafitiwa. Okpewho alichunguza nyimbo kwa jumla na mtafiti alifaidika kwa kuchungua hasa nyimbo za kampeni za kisiasa.

Miruka (1999) *Studying Oral Literature*, amefanya uchunguzi juu ya masuala mbalimbali ya nyimbo kama kipengele kimoja cha ushairi. Amegusia mgawo wa nyimbo, utendaji na uwasilishaji wa nyimbo, muundo wa mbinu za kisanaa, maudhui na dhima inayotekelezwa na nyimbo katika jamii. Kazi ya Miruka inahusiana na uchunguzi huu kwa kuchunguza nyimbo kwa jumla. Tofauti ni kwamba namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya ilitafitiwa  na mtafiti. Mtafiti alifaidika kwa kazi iliyofanywa na Miruka alipopiga hatua kushughulikia namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Wamitila (2002) aeleza kwamba fasihi simulizi ni fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya mdomo kwa kusimuliwa, kuimbwa, kutongolewa au kughaniwa. Kwa jumla, fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa fikrani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na vitendo bila maandalizi. Wanasosholojia waliamini kuwa uamilifu wa fasihi simulizi uko hai na haufi na kwamba unabadilika kulingana na maendeleo ya jamii husika. Tafiti hizi mbili zinalingana kwani nyimbo za kisiasa ni kipengele kimoja cha fasihi simulizi. Tofauti ni kwamba mtafiti alifanya utafiti juu ya namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Mtafiti alisaidika na utafiti uliofanywa na Wamitila alipopanua zaidi kuhusu mfano mmoja wa fasihi simulizi ambao ni nyimbo za kampeni za kisiasa.

Deane (2005) afahamisha kuwa Mwanahistoria Whitmer aliandika akiunga mkono umuhimu wa muziki kwa kufundisha na kusoma historia. Anaeleza kuwa nyimbo zinaweza kuangaza jinsi ya kufahamu historia ya watu wa Marekani kuliko njia yoyote nyingine kwa sababu zina nia kadha wa kadha zinazoweza kufafanuliwa kwa njia nyingi. Anafahamisha kwamba baadhi ya walimu wamegundua njia zao za kutumia muziki katika kozi zao kwani wanatambua kuwa muziki ni kioo cha matukio na desturi ya itikadi katika jamii. Aliamini kwamba njia hizi zote zinaunda mazingira yaliyo bora kwa masomo ya wanafunzi. Utafiti wa Deane unalingana na huu kwa sababu alifanya juu ya muziki kwa kufundishia. Tofauti ni kwamba alichunguza umuhimu wa muziki kwa kufundisha ilhali namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa ilitafitiwa. Mtafiti alipiga hatua kwa kuelezea mielekeo na mitazamo ya kijamii kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Wamitila (2008) anayo maelezo yafuatayo kuhusu wajibu wa nyimbo katika jamii: Nyimbo hutumiwa kuwasilisha thamani, itikadi, historia na imani za jamii inayohusika. Hii ni njia ya kuuendeleza uthabiti na muungano wa jamii hiyo. Zinatumiwa kupitisha thamani za kitamaduni katika jamii mbalimbali. Nyimbo ni njia kuu ya kutumbuiza na kumpa msikilizaji na mwimbaji burudani nzuri. Vilevile, nyimbo hutumiwa kuwahamasisha watu kutenda jambo fulani au kushirikiana katika matendo fulani. Wamitila anafahamisha kwamba nyimbo za kisiasa ni nyimbo zinazoimbwa kwenye shughuli za kisiasa kwa azma ya kuwahamasisha na kuwaleta watu pamoja kisiasa. Nyimbo hizo hulenga kuwashawishi watu kisiasa na pia kuwakosoa na kuwanyumbua wanasiasa kwa matendo fulani. Nyimbo zenyewe huwasilisha ujumbe kwa upesi mno hususan kupitia redio, runinga au hata jukwaani. Watu wengi hupenda kusikia muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji pamoja na ala za muziki kwa sababu huzivuta na kuzinasa hisia zao. Nyimbo hutumika sana wakati wa kampeni za kisiasa kwani hisia zinazowasilishwa kwa njia ya kuimbwa huwa na athari kubwa. Utafiti wa Wamitila unahusiana na utafiti huu kwa sababu umelenga wajibu wa nyimbo. Kuna tofauti kati yao kwani utafiti huu ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Mtafiti alifaidika na utafiti wa Wamitila kwa kuelezea zaidi kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo hizo za kampeni za kisiasa.

Dinkin (1989) atufafanulia kuwa kampeni nyingi hupenda kuweka ujumbe kuwa wazi ili kuvutia wapigaji kura wengi. Kwa mfano, katika uchaguzi wa urais kule Marekani, mwaka wa 2008, Barack Obama, aliyekuwa rais, alitumia ujumbe mwepesi mfululizo uitwao “Mabadiliko” katika kampeni yake. Ujumbe ukiundwa kimakini, itamhakikishia mgombezi ushindi wa kura. Katika historia ya demokrasia, uchaguzi huleta mifano ya jumla ya maamuzi ya raia. Kila mtu ambaye anapiga kura hushawishiwa na mambo mbalimbali kama vile upokezi wa kuwa mshiriki wa chama fulani, utathmini wa cheo, tabia, thamani na mashauri ya mgombezi. Maono ya wanaopiga kura juu ya wagombezi wa viti mbalimbali, yanaweza kuumbwa na vitendo na maneno ya mgombezi, mijadala yake na hoja zake kwa familia na marafiki. Vilevile, jitihada za vyama vya kisiasa, mgombezi na maombi ya kuyashawishi maono ya wanaopiga kura huchangia. Uchunguzi uliofanywa unalingana na wa Dinkin kwa sababu alichunguza namna ujumbe katika mazungumzo wakati wa kampeni za uchaguzi huathiri upigaji wa kura. Tofauti ni kwamba mtafiti alitafiti namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika

Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Mtafiti alifaidika kwa kazi ya Dinkin ilivyofafanua namna mazungumzo huathiri upigaji wa kura kwa kuchunguza namna nyimbo za kampeni za kisiasa huathiri upigaji huo wa kura.

Wamitila (2003) atufahamisha kwamba maudhui yapatikanayo katika nyimbo teule za kampeni za kisiasa ndiyo yale yanayopatikana katika jamii nyingi za Kiafrika hasa zile ambazo zina kiwango kikubwa cha mfumodume. Kutokana na mfumodume, wanawake wengi wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza na kujikomboa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kutokana na hadhi ya mwanamke kuwa chini ikilinganishwa na mwanaume, taswira ya mwanamke inayopatikana katika misemo, nyimbo na kazi nyingi za kifasihi zimedhihirisha udogo wa mwanamke. Tendo la mwanaume linakuwa na mwelekeo chanya na la mwanamke linaleta sifa hasi.

Wamitila afafanua kuwa nyimbo za kisiasa hutumiwa kueleza aina za nyimbo ambazo dhamira zao kuu ni siasa. Nyimbo za kampeni kihistoria, zimekuwa mojawapo ya ufundi wa kuwahamasisha, kuwashawishi na kuwaleta watu pamoja ili waweze kuuchukua mtazamo fulani wa kisiasa. Vilevile, wanasiasa hurekebishwa kama wamekosea kupitia nyimbo hizi. Tangu mwanzo wa siasa, yaonekana kama nia za nyimbo zilikuwa njia muhimu ya kuwasilisha ujumbe kuhusu mgombezi au jambo lililoko. Uchunguzi wa Wamitila unahusiana na utafiti huu kwani alidadisi kuhusu maudhui ya nyimbo za kisiasa. Utafiti wake ulikuwa dira katika utafiti huu uliofanywa. Tofauti iliyoko ni kwamba mtafiti alipiga hatua kuchunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

William (2012) aeleza kwamba ujumbe wa kampeni unao mawazo ambayo mgombezi angependa yawafikie wapigaji kura. Yeye angependa kuwaleta pamoja wale ambao watakubaliana na mawazo yake ili wapate kumwunga mkono katika kampeni za kisiasa. Kwa kawaida, ujumbe huwa ni masuala na sera za kisiasa. Mambo haya hujumlisha mawazo mahususi ya kampeni na hurudiwarudiwa mara nyingi ili kuleta ushawishi kwa wapigaji kura. Kwa vile utafiti wa William umeshughulikia ujumbe upatikanao katika kampeni za kisiasa, umeambatana na utafiti huu. Tofauti zao ni kwamba namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa ilitafitiwa. Mtafiti alinufaika kutoka utafiti wa William kwa kuelezea zaidi kuhusu ujumbe upatikanao kuambatana na jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Boller (1984) alifanya utafiti kuhusu nyimbo za kampeni za kisiasa Marekani. Anaeleza kwamba nyimbo za kampeni za uchaguzi huu zinaweza kusaidia wanahistoria. Wanahistoria hao wanaweza kudadisi kuhusu siasa na utamaduni wa Marekani. Nyimbo hizi zinabuniwa ili kumfanya mgombezi apendezeke kwa wapigaji kura wengi. Ikichunguzwa kisemwacho na nyimbo hizi kuhusu wagombezi, tunaweza kupata kidokezo kilichoshughulikiwa na Wamarekani na kilichothaminiwa wakati uchaguzi ulipokuwa ukifanywa. Utafiti uliofanywa na Boller unahusiana na huu kwa sababu zote mbili zinashughulikia nyimbo za kampeni za kisiasa. Tofauti yao ni kwamba utafiti huu ulishughulikia namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo hizo. Utafiti wa Boller ulielekeza mtafiti kuchunguza zaidi kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Boller aeleza kwamba madhumuni ya kampeni ni kuhakikisha habari inafikia watu ili wafanye uchaguzi wa ujuzi, kuongeza ufahamu wa upikaji kura na haki za mpiga kura. Madhumuni zaidi ni kusaidia kuhakikisha kuwa hoja ya raia ni mojawapo ya orodha ya mambo ya kampeni, kuongeza heshima kwa wagombezi, kuleta usaidizi kuinua kushiriki kwa wanawake na vikundi vilivyomo pambizoni na kuboresha mazingira yanayofaa kupiga kura iliyo huru. Haya maelezo ni kama mlinzi katika kazi ya uchaguzi na kuhakikisha kuwa hakuna ufisadi wala vurugu.

Kulingana na nakala ya Mchanganuo wa Hoja za Kihistoria na Uundaji wa Maamuzi (Historical Issues Analysis and Decision Making), nyimbo za kampeni zafaa kuwa na masuala maalum yaliyo msingi katika utafiti huu. Masuala haya ni kama vile wito wa kutiana shime katika sisa na maana ya wito wenyewe. Katika utungaji wa nyimbo, mambo ya msingi ni ufundi ambao waimbaji wanatumia kusihi wapigaji kura, nguvu na udhaifu wa ufundi wenyewe,namna mwimbaji hupinga mpinzani wa mgombezi ambaye anamwunga mkono katika kampeni.

Kampeni kama hii ilitangulizwa kule India mwaka wa 2006 na Chama cha Ushirika wa Utafiti kule Asia (The society for Participatory Research in Asia). Ilipongezwa kama mafanikio kulingana na ripoti ya kuongezeka kwa ushirika wa wapigaji kura. Tafiti hizi zinalingana kwa kuhusika na nyimbo za kisiasa isipokuwa utafiti uliofanywa ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Utafiti huu ulimwelekeza mtafiti alipokuwa akizichanganua nyimbo za kampeni za kisiasa zilizotumika wakati wa uchaguzi.

Nyimbo za kampeni zinaweza kufanikisha kampeni za uchaguzi iwapo kampeni zenyewe zina utaratibu ufaao. Kampeni ya Ufahamu kwa Mpigaji Kura kabla ya Uchaguzi (Pre-election Voter Awareness Campaign) inaeleza kwamba ni vyema kutumia ufundi wa kusikia na kuona katika eneo ambalo wengi hawana elimu ili kupitisha ujumbe wa uchaguzi. Nyimbo za kampeni za kisiasa zinafaa zikiandamana na picha. Boller alichunguza ujumbe upatikanao katika nyimbo za kampeni za uchaguzi. Uchunguzi wake unahusiana na utafiti huu isipokuwa mtafiti alipiga hatua kutafiti kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Maelezo ya Boller yalimwelekeza mtafiti alipokuwa akichanganua nyimbo za kampeni za kisiasa.

Miles (1990) ambaye alikiandika 'The Song, Odes, Glees and Ballads' alieleza kwamba madhumuni ya kitabu hiki yalikuwa jaribio la kiasili la kuleta uzuaji wa elimu ya habari za vitabu. Huu ulikuwa utanzu mmoja wa nyimbo za kampeni za ugombeaji wa kiti cha urais wa Marekani. Miles aliamini kwamba nyimbo za kampeni zilianza kustawi kuanzia mwaka wa 1840. Miles alithibitisha kuwa nyimbo hizo za kampeni za mwaka wa 1840 zilichapishwa hususan ili kuleta umoja katika chama na katika pahali pengi pa ushiriki wa umma. Uchunguzi wake una uhusiano na utafiti huu kwa sababu alifatiisha juu ya nyimbo za kampeni za kisiasa kwa jumla. Mtafiti alishughulikia namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Kazi ya Miles ilimnufaisha mtafiti katika utafiti wake kuhusu jinsia inavyowakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Newman (1997) aligundua kwamba nyimbo za kisiasa zingeweza kuimbwa na kufunzwa na takriban Wamarekani wote. Wamarekani wangeweza kushiriki katika uenezaji wa habari na kupata ufahamu kuhusu masuala ya itikadi. Newman alitumia maneno kadha wa kadha ya mashairi ya kinubi kuimarisha maneno yake lakini angechunguza mifano ya nyimbo zote ili atoe maelezo kamili ya habari ambayo nyimbo hizi ziliwasilisha. Utafiti wa Newman ni muhimu katika utafiti huu hasa pale alipoelezea masuala ya itikadi. Tofauti kati ya utafiti uliofanywa na

Newman na utafiti huu ni kwamba huu ulidhamiria kushughulikia namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Cohen (2005) alichunguza kupendwa kwa waimbaji katika karne ya kumi na tisa. Katika ustadi wa kazi yake, Cohen alieleza kuwa uimbaji ulikuwa jambo la kawaida la kusukuma wakati kwa Wamarekani wengi. Cohen anaunga mkono hoja za Miles ambaye anaamini kuwa wimbo wa kampeni ulijitokeza ili kufanyia kazi muhimu kampeni ya urais na uenezi wa demokrasia. Utafiti uliofanywa na Cohen unahusika na utafiti huu kwa maana yeye alichunguza nyimbo za kampeni za uchaguzi. Mtafiti alitafiti namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.
Utafiti ambao ulifanywa na Minal (2009) kuhusu wanawake siasani katika uchaguzi wa kitaifa kule Maharashtra, ulionyesha kwamba wanawake wagombezi huongezeka kutoka uchaguzi mmoja hadi mwingine lakini asilimia ya wanaochaguliwa inaendelea kupungua. Kwa mfano, mwaka wa 1952, ilithibitishwa kwamba kati ya wanawake wagombezi kumi na sita, watano walifanikiwa. Mwaka wa 2004, kati ya wanawake wagombezi mia moja na hamsini na saba, kumi na wawili walichaguliwa. Mwaka wa 1980, wanawake kumi na tisa walichaguliwa kati ya wanawake arubaini na saba. Mwaka wa 1995 kati ya wanawake mia mbili arubaini na saba, kumi na mmoja tu walifanikiwa. Utafiti wa Minal unahusiana na utafiti huu kwa sababu alishughulikia jinsia ya kike siasani. Tofauti ni kuwa mtafiti alichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Smith (2012) aeleza kwamba lugha ni chombo chenye nguvu ambacho wanasiasa wanaoutafuta uwezo wa mamlaka hutumia kuwasilisha sera na nafasi zao za kiitikadi. Vilevile, wao hutumia lugha hii kuiunda mitazamo fulani ili kuwashawishi na kuwaongoa wapiga kura kwa lengo la kuwashinda wapinzani wao. Kabla ya kuwahutubia watu katika mikutano ya kisiasa, wanasiasa huwachangamsha watu kwa nyimbo na ngoma za kuvutia kwa minajili ya kuuwasilisha ujumbe wa kisiasa. Matangazo ya kisiasa yaliyo na miziki bora ya kizalendo, huleta hisia za furaha. Muziki una uwezo wa kuboresha hisia, kuimarisha ushiriki wa kisiasa na kuleta ushindi katika uchaguzi wa kisiasa.

Vilevile, anaeleza kuwa hali ya jinsia ni kikwazo kikuu katika nyanja zote za maisha ya Marekani. Jambo hili liligundulika katika uchaguzi wa urais mwaka wa 2008. Utafiti wa

‘National Women’s History Museum’ kule Marekani, unaonyesha kwamba wanawake thelathini na watano wamewahi kuwania kiti cha urais lakini hakuna aliyechaguliwa. Utafiti wa Smith unahusiana na utafiti huu kwa sababu alichunguza namna wanasiasa wanaitumia lugha katika siasa zao. Tofauti ni kwamba mtafiti alichunguza namna nyimbo za kampeni za kisiasa zinawakilisha jinsia. Utafiti huo ulimsaidia mtafiti kudadisi zaidi namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha jinsia.

Mungai (2015) afafanua kwamba katika bara la Afrika si habari kubwa ngeni wakati mwanamke anawania kiti cha urais. Ni nadra sana Waafrika kuwapatia kura zao lakini ni vigumu wanawake wagombezi kupata zaidi ya asilimia moja ya kura zote. Utafiti wa Mungai unaambatana na utafiti huu kwa vile alitafiti kuhusu jinsia ya kike katika uwaniaji wa kiti cha urais. Tofauti ni kwamba mtafiti alitafiti namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Mtafiti alinufaika kwa kazi ya Mungai kwa kupiga hatua kuchunguza kwa nini wanaume wengi wanachaguliwa kuliko wanawake katika uchaguzi.

### *2.2.2 Dhima za Nyimbo za Kisiasa*

Chiuri (1984) alifanya uchunguzi kuhusu nyimbo za kisiasa, kimapenzi na za kijamii za msanii Joseph Kamaru. Utafiti wa Chiuri unahusiana na utafiti huu kwa sababu alishughulikia lugha iliyotumika na Kamaru katika muziki wake. Mtafiti alipiga hatua kutafiti namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Collier (1991) aeleza kwamba nchini Tanzania nyimbo nyingi za dini na za ulimwengu ni ufunuo wa maendeleo ya kijamii na kisiasa. Aina nyingi za nyimbo za dini huonya dhidi ya ufisadi na uasherati zinazoweza kuleta ugonjwa wa Ukimwi na madhara mengine katika jamii. Vilevile, nyimbo za ulimwengu hueneza mambo yayo hayo lakini kwa njia iliyo tofauti. Wimbo mmoja uitwao ‘Mr. Politician’ ulioimbwa na msanii aitwaye Nakaya, ni mfano mmoja unaoonyesha jinsi mambo ya kisiasa yanadhihirika katika nyimbo. Katika wimbo huo, kati ya mambo mengi yaliyomo, msanii anauliza kwa nini wanasiasa wanaonekana tu nyakati za uchaguzi? Nyimbo mbili, ‘Lekaputigute’ na ‘Nyumbani’ zilizoimbwa na wasanii waitwao Kigoma All Stars, ni maelezo ya uzalendo, ambao ni ufunguo wa maendeleo ya kijamii na kisiasa katika kila nchi. Nyimbo hizi mbili zilikuwa ufunguo wa ujenzi wa azimio wa kitaifa nchini Tanzania

ulioanzishwa na Azimio la Arusha mwaka wa 1967. Mawazo ya mtaalamu huyu ni muhimu katika utafiti huu kwa vile amegusia nyimbo. Tofauti iliyoko ni kwamba alishughulikia nyimbo za kisiasa na za dini ilhali mtafiti alitafiti kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

King'ei (1992) alifahamisha kuhusu nyimbo za taarab kutoka mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki kati ya miaka ya 1963-1990. Alifanya utafiti kuhusu muundo na kazi za nyimbo za taarab ambapo ni njia moja ya kuangaza hisia za jamii na utamaduni. Vilevile, alichunguza mtindo na namna lugha ilivyotumika katika nyimbo za taarab. Utafiti wa King'ei unahusiana na utafiti huu kwa sababu alishughulikia muundo na kazi za nyimbo za taarab. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa King'ei na utafiti huu ni kuwa mtafiti alichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Mtafiti alinufaika kwa kazi ya King'ei alipochunguza zaidi namna jamii inawakilisha jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Fadiman (1993) alichanganua matumizi ya lugha katika nyimbo za kampeni ya kabila la Kichuka nchini Kenya. Fadiman alidadisi namna maneno fulani kama vile nomino za kipekee, vitenzi na vivumishi yametumika kimakusudi katika nyimbo za kampeni za jamii ya Kichuka ili kuwavuta wapigaji kura na siasa ipate kufanikiwa. Utumizi wa maneno au vikundi vya maneno ya kiisimu kimakusudi, katika matini fulani ya kisiasa, huwawezesha wanasiasa kunyang'anya kwa kutumia nguvu uwezo wa kisiasa kutoka kwa wapigaji kura kwa ajili ya ubinafsi wao. Uchunguzi huu unaohusu nyimbo za kampeni za kisiasa, ulimfaidi mtafiti kwa kuchunguza zaidi namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa zinawakilisha jinsia. Utafiti huu ni tofauti na wa Fadiman kwa sababu ulihusika na namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Dunaway (1996) aeleza kwamba nyimbo hupendwa katika jamii. Kulingana na yeye, dhima za nyimbo za kisiasa ni kuwashawishi watu, kutia nguvu thamani na mawazo ya wasikilizaji, kuunda mshikamano wa watu katika jamii au kuleta umoja katika chama .

Anafafanua kwamba nyimbo za kampeni ni muhimu katika kila uchaguzi. Kazi za nyimbo zinatofautiana kutoka uchaguzi mmoja hadi mwingine kulingana na ukubwa na nguvu ya mambo

husika ya kila kampeni. Utafiti wa dhima za nyimbo za kisiasa unahusika na huu lakini mtafiti alichunguza zaidi namna jinsia inawakililishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Zukas (1996) katika nakala ya American Historical Association iitwayo “Different Drummers: Using Music to teach history,” aeleza kuwa inambidi mwalimu kuwa na ustadi wa muziki ili autumie ipasavyo katika darasa la historia. Nyimbo zinashtahili kutumika kufafanua mambo kuhusu daraja, jinsia, umuhimu wa utamaduni, siasa na uchumi. Utafiti wa Zukas ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu umechunguza nyimbo. Mtafiti alidadisi zaidi namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa kwani umuhimu wa muziki kwa kufundishia umekwishatafitiwa.

Martin (1998) aeleza kwamba muziki wa “Hip Hop” nchini Tanzania ulipata msukumo kutokana na mawazo na mandhari ya ujamaa. Baada ya Rais Nyerere kuanzisha itikadi mpya ya siasa, ikatekelezwa na wanasiasa wa Tanzania. Aliahidi kwamba ingewakomboa Watanzania kutoka ubeberu wa kimataifa. Kanuni za ujamaa zilifufuliwa tena kupitia njia ambayo haikuwa inatarajiwa. Anafahamisha kwamba dhana za umoja na usawa wa familia zilikuwa ndio ujumbe uliowasilishwa katika muziki. Kushirikiana kwa wananchi wa kawaida ili kujipatia mahitaji muhimu ya maisha, ni maneno yanayoweza kuonekana katika nyimbo nyingi za ‘Hip Hop’ za wasanii wa Tanzania. Nyimbo hizi zinapiga upatu ukuzaji wa biashara na kujitegemea katika jitihada za kuinua mioyo ya vijana na kuhamasisha mabadiliko katika jamii. Tafiti hizi zinaambatana kwa kushughulikia nyimbo. Tofauti ni kwamba Martin alishughulikia nyimbo za “Hip Hop” nchini Tanzania na mtafiti alishughulikia namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Wambua (2001) alichunguza mtindo wa nyimbo za kisiasa za Kakai Kilonzo. Anafafanua kwamba nyimbo za Kakai zinavuma sana hata kama ameaga dunia kwa sababu ya jinsi alizitumia tamathali za usemi katika nyimbo zake. Utafiti wa Wambua ulimsaidia mtafiti kufanya uchunguzi zaidi kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Mutembei (2005) afahamisha kuwa katika siasa, nyimbo za kizazi kipya zinahusika hasa na hali na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania. Nyimbo hizi za kizazi kipya huitwa 'Bongo Flava'. Leo hii vijana wanaimba na kujadili kuhusu maana na kushiriki kwa vyama vingi katika siasa za Tanzania. Wanaimba kuhusu mabadiliko ya katiba na upatikanaji wa Katiba Mpya Tanzania. Huu ni utafiti unaohusiana na huu uliofanywa isipokuwa Mutembei alizichanganua siasa katika nyimbo za 'Bongo Flava' nchini Tanzania. Mtafiti alitafiti namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Njogu na Maupeu (2007) waeleza kuwa nyimbo na siasa katika nchi za Afrika Mashariki huleta pamoja habari muhimu kuhusu nyimbo na siasa za eneo lenyewe na pande nyinginezo. Kupitia uchanganuzi wa sauti kwa kina, waandishi huanza kujadiliana kuhusu utunzi wa mambo ya utamaduni na mabadiliko ya siasa. Wanatufahamisha kuwa maneno yanayotunga nyimbo yalichunguza mambo yapasayo binadamu. Mambo haya ni kama elimu ya sayansi ya ulimwengu pamoja na uasili na maendeleo yake, maono ya walimwengu, daraja, na uhusiano wa jinsia, tafsiri ya thamani ya siasa na mazoezi mengine ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, hata kama yanachangamsha hadhira. Mazuio, masikitiko na uchofu wa hisia kutokana na ufisadi na siasa ya udikteta ambao unazuia uwezo wa raia, ulisukuma na bado unasukuma muziki unaovuma katika nchi za Afrika Mashariki. Ni nyongeza maalumu katika uchunguzi wa utamaduni unaosifika na dhima yake kwa kuumba jamii. Licha ya nyimbo kuwa nzuri, pia ni vyombo muhimu vya kuchunguzia namna matukio ya kisiasa na kijamii huendelezwa na kueleweka na raia. Mambo yanayohusika na miji, uchumi na utandawazi yalichangia umaarufu wa nyimbo zinazopendwa katika nchi za Afrika Mashariki miaka ya 1990. Nyimbo hizo ziliainishwa kwa mchanganyiko mbalimbali, matumizi ya maana mbalimbali ya maneno na ubunifu. Haya yalikuwa matokeo ya maendeleo ya kijamii ambayo hayawezi kutenganishwa na jamii, siasa na mambo mengine mahususi ya wakati huo. Utafii huu ulishughulikia nyimbo na siasa katika nchi za Afrika Mashariki na unahusiana na utafiti uliofanywa. Mtafiti alidadisi zaidi kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Mbogo (2008) atufahamisha kwamba wanasayansi wa kisiasa na wanahistoria wanaweza kupekua kupitia njia nyingi ambazo wanaona Mstaafu Hayati Rais Moi alitumia katika uaminifu wa uraia kwa zaidi ya miaka ishirini na minne katika utawala wake. Kwa kupanga njia hizi

katika uratibishaji wa ushawishi, huenda wasikumbuke nguvu zinazosababishwa na uimbaji. Walakini jinsi uhamasishaji wa sauti zilizopangwa ipasavyo, wakati mwingi husongesha, hulainisha na kuamsha moyo zikituliza akili. Moi akawa baba wa taifa hivi kwamba nyimbo zikichezwa sura ya rais ikaja kwa akili za wasikilizaji kama mtu aliyejali. Mtafiti alifaidika na utafiti wa Mbogo, aliyetafiti nguvu za uimbaji, kwa kuupanua na kupata mwelekeo katika utafiti wake unaohusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Samwel (2010/2011:18) katika jarida, aeleza kwamba mambo kama ubaguzi, matabaka, ukosefu wa ajira, mgawanyo mbaya wa rasilimali, ufisadi na ukosefu wa huduma muhimu katika jamii, ni mambo yanayohusiana na utashi wa kisiasa wa wanasiasa yanayosawiriwa katika nyimbo za mapenzi. Utafiti huu unahusiana na ule uliofanywa kwa vile ulishughulikia siasa katika nyimbo za mapenzi. Tofauti ni kwamba mtafiti alifanya utafiti unaohusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Jarida hili lilimsaidia mtafiti kushughulikia namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la jinsia.

Sakawa (2012) aeleza kwamba mitaani, nyimbo simulizi katika muziki wa kizazi kipya au kama wauitavyo ‘Bongo Flava’, unaendeleza sio uhamasishaji tu, bali elimu na maoni na mjadala kuhusu siasa, kujilinda na magonjwa, kujadili changamoto za kila siku na mambo yanayowagusa hasa vijana. Katika vituo vinavyopendwa sana, mashairi na nyimbo redioni ni tanzu ambazo zimetawanyika katika jamii nyingi za Tanzania kupitia vituo vya FM ambavyo vipo karibu katika kila mkoa. Kupitia televisheni na redio, fasihi simulizi ingawa imebadilika kutoka katika gamba la zamani, bado inabeba dhima ile ile: kuwafanya watu wasikie sauti na kupata ujumbe wa kisanaa na uliojaa ubunifu mkubwa. Kwa mfano, kupitia katika vyombo hivi, Tanzania nzima imeshiriki katika kuelewa mauaji ya Albino yanayotokea hasa katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Nyimbo zimetungwa kupinga ukatili huu, kuhamasisha watu kuelewa kinachoendelea na kupinga imani za kishirikina. Dhima ya muziki katika siasa nchini Tanzania inaendelea. Katika kampeni za kisiasa, wagombezi hutumia muziki kukusanya watu. Wale walio na pesa nyingi za kampeni, kama vile wagombezi katika Chama Cha Mapinduzi, huzungukazunguka wakiandamana na wasanii wanaocheza na kuimba kwenye mikutano. Wakati huu baadhi ya waimbaji hodari ni wabunge. Captain Komba, Joseph Mbiinyi na Vicky Kamata ni mifano ya wabunge hao. Wanasosholojia pamoja na Wanaanthropolojia wanahitajika kufanya

uchunguzi zaidi kuhusu jambo hili nchini Tanzania. Huu ni utafiti ulioshughulikia nyimbo za 'Bongo Flava' nchini Tanzania lakini ule uliofanywa na mtafiti ulihusika na namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Utafiti uliofanywa na Sakawa imemnufaisha mtafiti kupiga hatua zaidi kuchunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

Matu na Wanjiku (2012) walitafiti juu ya "Uwezo wa Muziki katika siasa ya Kenya, 1992 hadi 2008" na mgongano wake kwa uhusiano wa makabila hasa wakati wa kampeni za uchaguzi. Wanatuelezea kwamba historia ya muziki katika siasa za Kenya hutoa jinsi muziki umefanya kazi muhimu na kuleta pigo katika mambo ya siasa nchini Kenya. Uchunguzi uliofanywa kuhusu vurugu za uchaguzi nchini Kenya unaungama dhima ya hotuba ya chuki, vituo vya redio za lugha za wenyeji, historia ya mambo yasiyo ya haki, uchumi usio sawa, umaskini, ukosaji wa kazi, ufisadi na utawala mbaya na mchango wa muziki wa kuongeza vurugu katika siasa nchini Kenya. Uwezo wa muziki kwa kuleta mapatano, uponyaji na uundaji wa amani umethibitishwa. Uchunguzi huu unahusiana na utafiti huu kwa sababu unahusu uwezo wa muziki katika siasa ya Kenya. Tofauti ni kwamba namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya ilitafitiwa. Utafiti wa Matu na Wanjiku ulimwelekeza mtafiti kufanya uchunguzi zaidi kuhusu namna nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha jinsia.

Nkoala (2013) afafanua kwamba nyimbo za mapigano ni sehemu asili ya siasa ya awali, kisasa na wakati ujao nchini Afrika Kusini. Kwa sababu nyimbo ni za thamani katika siasa kule Afrika Kusini, tafiti nyingi zimefanywa za kufuatia historia na maana ya nyimbo za ukombozi. Tafiti za kutosha hazijafanywa kuhusu nyimbo za mapigano kama msingi wa hoja ambao unaweza kuenezwa. Matokeo yake ni kwamba watendaji wa kisiasa wameweza kushirikisha uwezo wa ushawishi ulioko ndani ya nyimbo za mapigano katika madaraka, baada ya wakati ule wa mgawo kisiasa na kijamii kule Afrika Kusini.

Siku hizi ni chama cha African National Congress na miungano mingine inayopatana nacho kama vile Congress of South Africa Trade Unions na chama cha South African Community huonekana kuzitumia peke yao nyimbo za mapigano. Chama cha Democratic Alliance kimejaribu kupinga matumizi ya nyimbo katika kampeni, kwani chama chenyewe hakijaelewa

jinsi nyimbo hizi hutumika kama vyombo vya ushawishi. Mtaalamu huyu ametufafanulia kuhusu nyimbo za mapigano na ukombozi kule Afrika Kusini, jambo ambalo linahusiana na utafiti huu. Nkoala alichunguza nyimbo za mapigano na ukombozi kule Afrika Kusini lakini utafiti huu ulihusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Utafiti uliofanywa na Nkoala ulimwezesha mtafiti kufanya utafiti zaidi kuhusu namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa.

## 2.3 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliegemea nadharia ya Ubabedume. Nadharia hii iliasisiwa mwaka wa 1987 na mwanasosholojia mmoja wa Australia aitwaye Raewyn Connell. Mihimili ya nadharia hii ni: mgawanyo wa mamlaka, uwezo kijinsia, na mielekeo kumhusu kila mwanajamii. Majukumu ya mihimili hii ni kama yafuatayo: Mgawanyo wa mamlaka: Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la mgawanyo wa mamlaka kulingana na jinsia wakati wa uchaguzi. Uwezo kijinsia: Huu ni mhimili uliomwezesha mtafiti kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia wakati wa uchaguzi. Mielekeo kumhusu kila mwanajamii: Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu kila mwanajamii kuambatana na jinsia wakati wa uchaguzi. Nadharia hii hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Connell anaeleza kwamba utamaduni na mazingira huwa vigezo muhimu katika kukuza ubabedume ambao hukolea katika fahamu za wanajamii. Hali hii huathiri mahusiano ya mwanamume na mwanamke katika jamii. Mwanaume huwa na haki zaidi ya mwanamke katika masuala mbalimbali yanayohusu asasi ya jamii za mfumodume.

Nadharia ya Ubabedume ilifaa kufanyia utafiti kwa sababu imelingana na suala na madhumuni ya utafiti huu. Hii ni mihimili ambayo ilimwongoza na kumwelekeza mtafiti kukusanya deta inayohusiana na mada, suala la utafiti, madhumuni na maswali ya msingi ya utafiti. Mtafiti alichanganua na kufasili deta kulingana na kila mmoja wa mihimili yote mitatu mfululizo ili aufikie uamuzi wake.

# SURA YA TATU

# MBINU YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji, uchanganuzi na ufasili wa deta. Deta hizi zilikitwa katika namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano mkabala wa kifasili. Hii ni kwa sababu deta ya utafiti huu si ya kitakwimu. Creswell (2009) aeleza kwamba utafiti wa kithamano huandaliwa kwa njia ya maelezo na wala si takwimu. Schwandt (2000) aeleza kuwa mkabala wa kifasili husaidia kuelewa matendo ya wanajamii.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ya Bomet iliyoko katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya. Mtafiti alitumia sampuli ya kimakusudi kuchagua kaunti hii. Kaunti ya Bomet ina kaunti ndogo tano zifuatazo: Sotik, Bomet Mashariki, Chepalungu, Bomet ya Kati na Konoin. Imepakana na kaunti zifuatazo: Kericho katika upande wa Kaskazini, Nyamira katika upande wa Magharibi, Narok katika upande wa Kusini na Nakuru katika upande wa Kaskazini-Mashariki (County Government of Bomet, 2018). Mtafiti alilichagua eneo hili kuwa mfano wa kufanyia utafiti huu. Katika eneo hili, kuna wasanii wengi ambao wameimba nyimbo kadhaa zilizo maarufu. Miongoni mwa wasanii hawa, wengi ni wanaume na wanawake wachache. Wanawake wachache wako uongozini kisiasa katika kaunti hii. Mtafiti anafahamu lugha ya wenyeji na kwa hivyo ilikuwa rahisi kutafsiri nyimbo kutoka lugha hiyo hadi lugha ya Kiswahili.

## 3.4 Ukusanyaji wa Deta na Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti alinunua kanda ishirini na moja. Kati ya kanda hizo, alinunua kumi na mbili madukani na tisa kwa wafanyizaji wa nyimbo. Baada ya kuzinunua kanda hizo ishirini na moja, mtafiti alizipatia msimbo ambazo ni A, B, C, D, E, F, G, H, I, J, K, L, M, N, O, P, Q, R, S, T na U. Msimbo huwakilisha nyimbo za kisiasa zilizokusanywa. Alizikusanya nyimbo hamsini na mbili

za kisiasa ambazo zilirekodiwa katika kanda hizo. Alitumia sampuli ya kimakusudi kuziteua nyimbo ishirini na mbili za kampeni za kisiasa zilizohusika na jinsia katika nyimbo hizo hamsini na mbili. Nyimbo ishirini na mbili za kampeni za kisiasa zilipatikana katika kanda hizo. Kati ya nyimbo hizo ishirini na mbili, tano zililenga vyama vya kitaifa ambavyo ni Jubilee, NASA, URP na CCM. Nyimbo zote za kampeni za kisiasa zilipewa majina kama zilivyoainishwa katika viambatisho C, D na E. Kulikuwa na wasanii walioimba zaidi ya wimbo mmoja. Wasanii walioimba nyimbo hizi walikuwa kumi na sita, wa kike walikuwa wanne na wa kiume walikuwa kumi na wawili.Wasanii hao kumi na sita ndio wale walioimba nyimbo za kampeni za kisiasa zilizokusanywa. Mtafiti alitumia nyimbo hizo kuchunguza namna wasanii wa kike na wa kiume waliwakilisha jinsia katika kazi zao wakati wa kampeni za kisiasa. Nyimbo hizo ni zile zilizoimbiwa wawania viti vya urais, useneta, ugavana, ubunge na ujumbe wa wadi.

Muhtasari wa nyimbo husika zilizokusanywa kutoka ngazi ya urais hadi wajumbe wa wadi zilipangwa. Idadi ya nyimbo za kisiasa katika kila kanda iliainishwa ifuatavyo: Kanda A ilikuwa na tatu, B mmoja, C mbili, D mmoja, E tatu, F mbili, G tatu, H tatu, I mbili, J tatu, K nne, L mbili, M tatu, N nne, O mbili, P mmoja, Q tatu, R tatu, S mbili, T mbili na U tatu. Nyimbo zote za kisiasa zilikuwa hamsini na mbili kwa jumla.

Idadi ya nyimbo za kampeni za kisiasa zilizoteuliwa kutoka nyimbo hamsini na mbili za kisiasa ni kama ifuatavyo: A mbili, B mmoja, C sufuri, D mmoja, E mbili, F sufuri, G mmoja, H mbili, I sufuri, J mmoja, K mbili, L mmoja, M sufuri, N mbili, O sufuri, P sufuri, Q mmoja, R mbili, S mbili, T mmoja na U mmoja. Nyimbo zote za kampeni za kisiasa zilikuwa ishirini na mbili kwa jumla. Idadi ya nyimbo za kampeni za kisiasa iliyolingana na jinsia ni kama ifuatavyo: tisa zilihusika na wanaume na mbili zilihusika na wanawake. Nyimbo hizo zote zilikuwa kumi na mmoja kwa jumla. Lengo la kwanza linasema: Kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la jinsia.

Idadi ya nyimbo za kampeni za kisiasa kulingana na wagombezi ni kama ifuatavyo: tano zilihusika na Rais na Naibu wa Rais, tatu zilihusika na Magavana, mmoja ulihusika na Seneta, tatu zilihusika na Wabunge na mbili zilihusika na Wajumbe wa Wadi. Nyimbo hizo zote

zilikuwa kumi na nne kwa jumla. Lengo la pili linasema: Kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia.

Idadi ya nyimbo za kampeni za kisiasa kulingana na itikadi kuhusu jinsia ni kama ifuatavyo: kumi na mmoja zilihusika na wanaume na tatu zilihusika na wanawake. Lengo la tatu linasema: Kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu jinsia.

Mtafiti alitumia mwongozo wa maswali ya mahojiano kama mbinu nyingine ya ukusanyaji wa deta. Alitumia mbinu hii ili kupata ufahamu wa ndani zaidi katika utafiti huu na pia kuyapata maoni ya wakaaji wa sehemu iliyofanyiwa utafiti. Aliwahoji wasailiwa kumi na wawili wa jinsia ya kike na kiume kati ya miaka kumi na minane hadi thelathini, thelathini hadi arubaini, arubaini hadi hamsini na zaidi ya hamsini. Kati ya wasailiwa hao kumi na wawili, watunga maoni walikuwa wanne. Majibu ya wahojiwa yaliandikwa katika karatasi za mahojiano.

### 3.5 Vifaa vya Ukusanyaji wa Deta

Mtafiti alitumia kanda zilizorekodiwa nyimbo za kisiasa kama vile diski ndogo na kaseti. Alitumia kicheza diski na kicheza kaseti kusikiliza nyimbo hizo. Alitumia kalamu kuandika nyimbo katika daftari. Alitafsiri nyimbo kutoka lugha ya Kalenjin hadi lugha ya Kiswahili. Alitumia kipakatalishi kupiga chapa nyimbo. Alitumia printa kuzichapisha nyimbo karatasini. Alitumia kipakatalishi kuhifadhi deta. Deta iliyokusanywa ilichanganuliwa na kufasiliwa na mtafiti.

### 3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Deta

Deta ya kimsingi ya utafiti huu ilikuwa nyimbo. Deta hii ilikusanywa kwa usikilizaji wa kanda za nyimbo. Mtafiti alichezesha kanda akisikiliza nyimbo na kuziandika  Deta zaidi ilikusanywa kwa kufasili maana za nyimbo na kutoka majibu ya maswali ya mahojiano. Mbinu ya ufasili wa deta ilitumiwa kuchanganua deta ya utafiti huu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Ubabedume.

### *3.6.1 Mfumo Maalum wa Uchanganuzi wa Deta*

Hatua ambazo zilitumika katika uchanganuzi wa deta ni kama zifuatazo:

**Hatua 1**

Mtafiti aliweka kanda za nyimbo katika kicheza diski. Akasikiliza nyimbo za kisiasa akisaidika na mada za nyimbo hizo ambazo ziliandikwa katika kanda.

**Hatua 2**

Unukuzi wa deta: Mtafiti alizinukuu nyimbo hizo za kisiasa ambazo zilikuwa zimerekodiwa. Aliweka kanda halafu akazisikiliza nyimbo huku akiziandika daftarini. Baada ya kuziandika nyimbo, akazitafsiri kutoka lugha ya Kalenjin hadi lugha ya Kiswahili.

**Hatua 3**

Aliziainisha na kuzitenganisha nyimbo za kampeni za kisiasa na zile ambazo hazihusiani na mada.

**Hatua 4**

Nyimbo za kampeni za kisiasa zilizoainishwa kwa ajili ya uchanganuzi, mtafiti alizidondoa kwa kutumia viashiria vilivyomwongoza ikiwa kama kurunzi yake. Viashiria hivi vilikuwa kama taashira, jazanda na methali. Mtafiti alivibainisha viashiria hivi kwa kukoleza wino.

**Hatua 5**

Viashiria vilivyoainishwa katika wimbo husika vilifasiriwa kwani vilionyesha kubeba maana fiche.

**Hatua 6**

Kila wimbo ulichanganuliwa na kufasiliwa kulingana na mihimili ya nadharia ya Ubabedume pamoja na malengo yote matatu. Mgawanyo wa mamlaka ni mhimili uliotumika kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la mgawanyo wa mamlaka kulingana na jinsia. Uwezo kijinsia ni mhimili ulitumika kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia. Mielekeo kuhusu kila mwanajamii ni mhimili

uliotumika kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu kila mwanajamii kuambatana na jinsia.

**Hatua 7**

Uwasilishaji wa deta: Deta iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo yaliegemea maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa zinavyowakilisha suala la jinsia, namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia na suala la itikadi kuhusu jinsia.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UFASILI WA DETA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii iliangazia uchanganuzi na ufasili wa deta iliyokusanywa kuhusiana na namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Mtafiti alizikusanya nyimbo na kuzinukuu halafu akazitafsiri kutoka lugha ya wenyeji hadi lugha ya Kiswahili. Baada ya utafsiri wa nyimbo hizi, alichanganua na kufasili maudhui yao huku pia akiyatumia majibu ya wasailiwa. Maudhui hujumlisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo. Mbinu na mtindo huwasilisha maudhui kupitia mada, dhamira, tasnifu, wahusika na matumizi ya lugha ya wasanii husika kulingana na hadhira wanayoilenga. Nyimbo ambazo zilitumika zilikuwa za wasanii wafuatao: Kipchamba Tapotuk, Ben Bii, Chama Cha Mashinani Women (CCM), Jeremiah Kosgei, Sogers Mekenyo, Arumutik Kosgei, Marion Chelang'at, Tapnyole Rotich, Shuttle Sisters, Titus Kosgei, Sweetstar, Kipkurui Ng'eny, Ras Wageni, Hotstar Kutundetunde, Cheres Daniel na Kachwes Rotich. Kila msanii alikuwa na kikundi chake cha waimbaji. Mtafiti alitumia nyimbo hizi ili kuchunguza namna wasanii wa kike na wa kiume, wanawakilisha jinsia katika kazi zao wakati wa kampeni za kisiasa. Vilevile, mtafiti aliwahoji wasailiwa ili kupata matokeo kwa undani zaidi.

## 4.2 Mpangilio wa Deta

Mtafiti alichanganua na kufasili deta kulingana na mihimili ya nadharia ya Ubabedume pamoja na malengo yote matatu mfululizo. Deta iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo yaliegemea malengo yote matatu.

### *4.2.1 Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Jinsia.*

Kwa mujibu wa Sengo na Kiango (1973) kazi ya fasihi hutumia lugha kwa njia ya ubunifu. Fasihi ina uhusiano na hali kamili ya jamii. Fasihi simulizi ni sanaa ya lugha inayofungamanishwa na maisha ya binadamu katika jamii. Nyimbo za kisiasa ni aina moja ya tanzu za ushairi simulizi. Nyimbo hizi huimbwa kwenye shughuli  za kisiasa kwa azma ya kuelewesha, kuhamasisha, kubeza na kutumbuiza kwenye sherehe. Demokrasia ya muziki imewawezesha wagombezi wa kisiasa kuleta tofauti kubwa katika matokeo ya uchaguzi. Hali

halisi husawirika katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Jambo hili limedhihirika katika utafiti huu.

#### *4.2.1.1 Mgawanyo wa Mamlaka*

Nadharia ya Ubabedume hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Utafiti huu ulishughulikia namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha suala la jinsia.

Msanii mmoja aitwaye Jeremiah Kosgei aliwapigia debe Uhuru Kenyatta na naibu wake William Ruto wakati wa kampeni za kisiasa za 2017. Mada ya wimbo ulikuwa 'Jubilee'. Chama chao kiliunganisha vyama viwili, United Republican Party na The National Alliance. Rejea sehemu ya wimbo wa kwanza.

***1. <u>JUBILEE</u>***

| | |
|---|---|
| *Kokiyokten Samoei Arap Ruto.* | *Tunakutuma Samoei Arap Ruto.* |
| *Asiimutwech Uhuru konyo Kapkatet.* | *Utuletee Uhuru aje nyumbani Kapkatet.* |
| *Si kikochin **mwaita** nebo Kalenjin.* | *Ili tumpatie **mafuta** ya Kalenjin.* |
| *Kou weritab Jesse nemi Bible.* | *Kama mwana wa Jesse katika Biblia.* |
| *Si koribwech emet.* | *Yeye apate kutulindia nchi.* |

Katika sehemu ya wimbo huu, Ruto alitumwa apeleke Uhuru atakaswe na wazee wa kiume wa Kalenjin apate kulinda nchi ya Kenya. Uhuru alifananishwa na Daudi mwana wa Jesse katika Bibilia ambaye alikuwa mfalme wa maajabu aliyetenda makuu kule Uyaudi. Utawala wa jinsia ya kiume pekee ulisawirika. Connell (1983) :185, 186, 239 anaeleza kwamba, ubabedume sio namna wanaume wenye nguvu hujidhihirisha kwa jamii, bali ni njia ya kuhifadhi nguvu yao, na ndio maana idadi kubwa ya wanaume wanahamasishwa kuunga mkono ubabe-dume huo kwa sababu unawafaidi.

Kuna wasanii waliojiita Shuttle Sisters ambao walimpigia debe Ruto akiwa katika chama cha United Republican. Alikuwa akigombea kiti cha naibu wa rais mwaka wa 2013. Rejea sehemu ya wimbo nambari mbili.

***2. URP***

| | |
|---|---|
| *Nyiganenyon Ruto koriborjige.* | *Shujaa Ruto umejitahidi.* |
| *Kot iboru chamaitab URP.* | *Hadi ukaunda chama cha URP.* |
| *Arap Ruto ko chorwetab chi tugul..* | *Arap Ruto ni rafiki ya kila mtu.* |
| *Mami bororiet Kenya ne moingen kainetab Samoei.* | *Hakuna jamii nchini Kenya isiyotambua jina la Samoei.* |
| *Kisaun kot indochi emenyon Kenya.* | *Sisi tunakuombea hadi uongoze nchi yetu ya Kenya.* |
| *Ibur kou Baba Moi.* | *Ukae kama Baba Moi.* |

Ruto, akiwa mwanaume, alisifika kama shujaa aliyejitahidi kuunda chama cha URP. Vilevile, ilielezwa kwamba yeye ni maarufu kote nchini kwa kuwa rafiki ya kila mtu. Anaombewa Mungu amwezeshe yeye wakati mmoja aongoze nchi ya Kenya akifuata nyayo za Mstaafu Hayati Rais Moi katika uongozi wake. Mstaafu Hayati Rais Moi alitawala nchi ya Kenya miaka ishirini na minne mfululizo hadi 2002 alipostaafu. Sehemu hii ya wimbo imebainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume.

Sehemu ya wimbo inayofuata iliimbwa na msanii mmoja aitwaye Daniel Cheres. Aliwasifu viongozi wote wa kisiasa nchini Kenya wakati wa kampeni za kisiasa mwaka 2017. Rejea sehemu ya wimbo nambari tatu.

***3. JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kitinye kelchin en Kenya, en kandoik che makibestos.* | *Naomba usaidizi kutoka kwako shujaa wa Tunayo bahati nchini Kenya, kuwa na viongozi wasiotenganishwa.* |
| *Oribech asi keribok.* | |
| *Osome toretet koyobun nyiganetab* | *Mtuchunge halafu tuwachunge.* |

*Kalenjin.* *Kalenjin.*

Msanii alimwomba Ruto ambaye ni shujaa wa Kalenjin pamoja na viongozi wengine nchini Kenya kuwalinda wananchi ili wananchi wapate kuwalinda. Waliosifika katika wimbo huo hususan walikuwa wanaume kwa sababu kulikuwa na mmoja ambaye alitajwa kama shujaa. Wanaume wanaheshimika katika jamii na kwamba wanastahili kuwa viongozi. Connell (1990): 83, afahamisha kwamba uinuaji wa uume, huimarisha muundo wa utawala na ukandamizaji katika utaratibu wa kijinsia kwa ujumla.

Kikundi cha kina mama kinachoitwa CCM Women, yaani, Wanawake kutoka Chama cha Mashinani, waliimba wimbo wenye mada 'Chama cha Mashinani'. Waimbaji hao walikisifu chama cha Mashinani kikiwa ndani ya Muungano wa National Super Alliance (NASA). Muungano huu uliongozwa na Raila Odinga na ulikuwa maarufu sana katika ugombezi wa kiti cha urais wakati wa uchaguzi wa kitaifa wa mwaka wa 2017. Chama cha Mashinani kilianzishwa na Isaac Ruto kutoka Kaunti Ndogo ya Chepalungu aliyekuwa akigombea kiti cha ugavana mwaka huo. Wasanii walimshukuru yeye kwa kuanzisha chama hicho na wakaeleza kwamba yeye ni fahali yao na hawakutaka aumizwe na yeyote. Walimwinua yeye wakisema kwamba wanampenda na yeye ni shujaa wao, shujaa mfano wa moto ambaye anatambulika katika nchi nzima ya Kenya. Walieleza kwamba kwa sababu ya maendeleo aliyofanya katika kaunti yao, hawezi kubadilishwa na kwamba angebaki kuwa kiongozi wao tena miaka mingine ijayo. Kupitia wimbo huu, uhodari wa jinsia ya kiume, ambao ni kielelezo chake cha mamlaka, umedhihirika. Rejea sehemu ya wimbo nambari nne.

***4. <u>CHAMA CHA MASHINANI</u>***

| | |
|---|---|
| *Kongoi inye* ***kirginyon*** *Mashinani kityo.* | *Asante* ***fahali*** *yetu Mashinani pekee.* |
| *Mokichomndoi kesilwech.* | *Haturuhusu aumizwe.* |
| *Kichome echek nyiganet.* | *Tunampenda shujaa wetu.* |
| *Kongoi nyiganet neu* ***mat.*** | *Asante shujaa mfano wa* ***moto.*** |
| *Ne kikenai en Kenya.* | *Anayejulikana nchini Kenya.* |
| *Mokiwole kora.* | *Haibadilishwi tena* |

Msanii mmoja aitwaye Ben Bii alifahamisha kwamba kumekucha na watu waamke kwa sababu tunataka  mabadiliko hususan katika siasa. Mada kuu yake ilikuwa ‘Daktari Joyce Laboso’ na mada ndogo ilikuwa ‘Daktari Joyce Laboso Kaunti ya Bomet, mama na kazi.’ Alikuwa akimtetea mgombezi huyu wa kike katika kampeni za kisiasa za 2017. Rejea sehemu ya wimbo nambari tano.

### 5. ***<u>DR. JOYCE LABOSO BOMET KAUNTI MAMA NA KAZI</u>***

| | |
|---|---|
| *Bikab Bomet Kounti ong’et kakoech emet.* | *Watu wa Kaunti ya Bomet mwamke kumekucha.* |
| *Kogeger konyone walet.* | *Tumeona mabadiliko yakija* |
| *Dr. Joyce Laboso ne koketach koik Gavana.* | *Tumepokea Dkt. Joyce Laboso kuwa Gavana.* |
| *Kiwole ra kele kiwole.* | *Tutabadilisha wakati huu, tutabadilisha.* |
| *Kondoikyok ko kokelewen en chamaitab Jubilee.* | *Viongozi wetu wamechaguliwa katika Muungano wa Jubilee.* |
| *Kokomwa kole kiwole.* | *Wamesema tutabadilisha.* |
| *Walaken ana komataikany si kewalin i.* | *Badilika au ungoje ubadilishwe.* |
| *Ni ko tugetab ng’omnotet o papa.* | *Hii ni sauti ya busara papa.* |

Kuna dhihirisho kwamba wimbo wenyewe ulikuwa ukimtetea mgombea huyu wa jinsia ya kike katika mashindano ya kiti cha ugavana katika kaunti hiyo. Msanii huyo alikuwa akizungumzia mabadiliko tofauti tofauti katika jamii hasa kisiasa. Alikuwa akieleza kwamba watu hawakuwa wanamkubalia gavana aliyekuwa akitoka apate tena kiti hicho. Vilevile, hawakuwa wanatakia tena jinsia ya kiume ugavana huo kulingana na namna mwimbaji alisema, ‘Mama na kazi.’ Huenda pia alikuwa akiongea kuhusu kiongozi mwenye elimu ya juu ni yule ahitajikaye siku hizi. Msanii huyo aliwatetea wagombezi wengine wa Mrengo wa Jubilee. Aliwataja wagombezi sita wa jinsia ya kiume na wawili wa kike kuonyesha fika kwamba kulikuwa na mashindano ya wanasiasa wengi wa kiume na wachache wa kike. Alifafanua kwamba viongozi wao wote wakiwa katika mrengo huo, waliungana na kusema wanataka mabadiliko. Aliwataja wawakilishi

wa wanawake waliokuwa katika mrengo huo ingawa hawakuwa wakishindana na wanaume. Carrigan na wengine (1985) wafafanua kwamba taasubi za kiume ni suala la jinsi vikundi fulani vya wanaume vinavyomiliki nafasi za utawala na utajiri, na jinsi wanavyohalalisha na kuunda mahusiano na jamii ambayo yanazalisha utawala wao.

Ben Bii alizidi kueleza kwamba kina mama wote kwa jumla ni mwangaza duniani humu na wale waliojitolea kuingia siasa ni stima. Kusema tena wanawake hawawezi kuongoza, kumepitwa na wakati kulingana na mwimbaji huyu. Msanii huyo alitukuza jinsia ya kike kwa kueleza kwamba wao wanaweza kutawala katika jamii ambapo jinsia ya kiume imehusishwa na madaraka ya juu. Rejea sehemu ya wimbo nambari sita.

### *6. __DR. JOYCE LABOSO BOMET KAUNTI MAMA NA KAZI__*

| | |
|---|---|
| *Kwonyik ko lobkeiyet* | *Kina mama ni mwangaza.* |
| *Chu ko* ***sitimok.*** | *Hawa ni* ***stima.*** |
| *Okweng'ch Bomet, amakichut keringonik.* | *Mtumulikie Bomet, tusipate kuingia mashimoni.* |
| *Kondoikyok asi oyoiywech bandab tai* | *Viongozi wetu mtufanyie maendeleo* |

(Obenga 2004: 595) aeleza kwamba katika enzi za Farao, kisheria, wanawake walikuwa sawa na wanaume. Waliweza kumiliki na kutumia mali na kufanya kazi kama za utawala na kuwa wakaguzi wa hekalu lakini wakilinganishwa na wanaume, hawakuwa wakitambulika katika kazi hizo. Katika kumbukumbu za Misri ya kale, wataalamu wa kiume, waandishi na wanafunzi wa kiume, wote walipata umaarufu lakini haikuwa hivyo kwa wanawake katika nafasi sawa.

Wasanii wengine walichanganya nyimbo za ulimwengu na za dini. Mfano mmoja ni msanii huyo aitwaye Ben Bii aliyemwunga mkono marehemu Dkt. Laboso wakati wa kampeni za kisiasa mwaka 2017. Wakati alikuwa akiomba kuwe na mabadiliko ya uongozi, aliimba akidondoa maneno ya Bibilia. Aliyanukuu maneno hayo akielewa  wazi kwamba neno la Mungu halitaweza kupingika kamwe. Alimwomba Mwenyezi Mungu mwenyewe ayalete mabadiliko hasa katika siasa inayopiganiwa na jinsia zote mbili. Alimwona marehemu Dkt. Laboso akiwa na uwezo wa

kuleta maendeleo kwani mwanamke anaweza kupanda ngazi kiutawala. Rejea sehemu ya wimbo nambari saba.

### *7. DR. JOYCE LABOSO BOMET KAUNTI MAMA NA KAZI*

| | |
|---|---|
| *Kimwa Kiptaiyat,'Osom si kekonok, ocheng si onyoru, okongon si keyotwok.'* | *Yesu alisema, 'Mwombe halafu mpewe, mtafute halafu mpate na mgonge halafu mfunguliwe.'* |
| *Joyce Laboso ko Gavana nebo Bomet Kounti.* | *Joyce Laboso ni gavana wa Kaunti ya Bomet.* |
| ***Chepyoset** o papa.* | *Ni **mwanamke** o papa.* |
| *Ibuch Bomet kwo kotililit.* | *Fagia Bomet hadi ing'are.* |

Marion Chelang'at ni msanii aliyeeleza zaidi juu ya uongozi wa jinsia ya kike. Yeye pia alikuwa akimunga mkono marehemu Dkt. Laboso awe gavana mwaka wa 2017. Alimdhihirishia kwamba alikuwa akipendezeka na kuhitajika sana katika kaunti. Ingawa watu wanataka maziwa, si lazima kuweko na ndume halafu maziwa yapatikane kwani kuna njia nyingine ya kuyapata. Hii ni wazi kwamba si lazima mwanamume aongoze na kwamba watu wanataka mabadiliko. Wanataka mwanamke apewe mamlaka ili aweze kutawala. Rejea sehemu ya wimbo nambari nane.

### *8. JUBILEE OIYE*

| | |
|---|---|
| *Omwochin **Chemaluk** chamat mising.* | *Mmwambie **Chemaluk** anapendezeka sana.* |
| *Ndandan kimoche chego, ko malazima **kirgit.*** | *Ingawa tunataka maziwa, si lazima tuwe na **ndume.*** |
| *Kimoche tuguk che lelach.* | *Tunataka vitu vipya.* |
| *Ongele kiwole en Bomenyon.* | *Tuseme tutageuza katika Bomet yetu.* |
| *Gavana ko Joyce, kamenyon korur bai.* | *Gavana ni Joyce, mama yetu mwenye uwezo wa kulisha jamii.* |
| *Telel en sera che koimwa.* | *Simama imara kwa sera zako ulizo nazo* |

Msanii huyo aliwapinga wagombezi wengine wa kiume akimwambia Laboso kwamba kuna wale ambao wamekaa kwa muda mrefu mamlakani na wamepitwa na wakati. Kwa hivyo, wawachie watu wengine nafasi waweze kuongoza. Rejea sehemu ya wimbo nambari tisa.

### ***9. <u>JUBILEE OIYE</u>***

| | |
|---|---|
| *Mi okot bamong'o chombo saa nane.* | *Kuna wale kina baba wa saa nane.* |
| *Konyor 20% komoche 100%.* | *Waliopata 20% wakitarajia 100%.* |
| *Omwochinewech bamong'o komusta gaa.* | *Mtuambilie baba araukie nyumbani.* |
| *Ak konaisi bomori kakorik yosin.* | *Amwambie babu uzee umekaribia.* |
| *Kakoyam ko ng'alal ng'alek che kong'yotin.* | *Imemtosha anene maneno yaliyokomaa.* |

Kupitia wimbo huu, jamii imekuwa na mwelekeo tofauti kuhusu majukumu ya mwanamke na mwanaume. Jinsia zote mbili zipewe nafasi sawa katika jamii hasa kisiasa bora wanajamii wapate huduma bora.

Kuna mwimbaji aitwaye Arumutik Kosgei ambaye alimtetea William Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi.

### ***1O. <u>PROFESA WILLIAM LESAN</u>***

| | |
|---|---|
| *Kokekonuge vijana kisib ng'alekab boisiek.* | *Sisi vijana tumejitolea kufuata mawaidha ya wazee.* |
| *Kegas ng'alekab bamong'o.* | *Tusikie mawaidha ya baba.* |
| *Si ketech Bomet Kounti ba kolili, komoche chito ne somanat.* | *Tukitaka kujenga Kaunti ya Bomet hadi ing'are, tunahitaji mtaalamu.* |
| *Profesa somananing'ung ko **sobunitab** Bomet Kaunti.* | *Profesa masomo yako ni **sabuni** ya Kaunti ya Bomet.* |
| *Si kotililit bororienyon en ng'omnotet.* | *Ili nchi yetu itakasike kielimu.* |

Katika kabila la Kalenjin wazee wa jinsia ya kiume huheshimika sana. Mwimbaji alieleza kwamba vijana walishauriwa na wazee hao kuchagua mgombezi aliyebobea katika masomo kuwa seneta wao. Hii ni njia moja ya kuukuza ubabedume kwa maana mwanaume amehusishwa na hadhi ya juu. Vilevile, hili ni dhihirisho la kuimarisha ngazi ya mamlaka kwa jinsia ya kiume.

Msanii alieleza kwamba Lesan ni mgombezi aliye shujaa na hawezi kushtuliwa wala kutingishika katika kazi yake. Angeweza kuwa mwangaza wa kaunti na kwa sababu ya ukarimu wake, angeichunga sahani ya wazee ili wanaume wengine wadogo waje wakailia siku za usoni. Msanii huyo alikiona kiti hiki kikiwa cha jinsia ya kiume kulingana na maelezo yake. Alieleza kwamba mgombezi alitarajiwa kukalia kiti cha useneta kwa njia ifaayo na muda wake ukiisha, awawachie wanaume wengine wadogo wa vizazi vingine vijavyo. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na moja.

***11. <u>PROFESA WILLIAM LESAN</u>***

| | |
|---|---|
| *Si koribwech **kisienyon** bo kok.* | *Apate kutuchungia **sahani** yetu ya wazee.* |
| *Sinyon kwomisien murenjun chon mengech.* | *Ili wanaume wale wengine wadogo wapate kuilia.* |
| *Profesa Lesan ko nyiganet.* | *Profesa Lesan ni shujaa.* |
| *Lesan, konyoljin ng'echeret.* | *Lesan, kiti kimekufaa.* |
| *En oyebindo ak nyiganatet ne itinye.* | *Kwa ukarimu na ujasiri ulio nao.* |
| *Ma kitisionin.* | *Huwezi ukatishwa.* |
| *Seneta nenyon ko moitumtumokse.* | *Seneta wetu hawezi kutingishika.* |

Msanii alifafanua kuwa Lesan alikuwa mwanaume aliyekuwa akipenda kuletea watu maendeleo na hakuwa na mapendeleo. Alimshauri yeye kwamba akishinda katika uchaguzi, asimame imara na kuwatatulia watu shida ya njaa jinsi Yusufu katika Bibilia aliwaokoa Wayaudi kule Misri kwa kuwapatia chakula. Lesan alifananishwa na Yusufu, mwanaume aliyetambulika katika kazi aliyowafanyia watu. Alionekana kama mwanaume ambaye angeweza kuwalinda wanyonge kama angechaguliwa. Utetezi kama huu ungewavuta wapiga kura wengi kwa mgombezi kwa maana

watu hupenda mtu ajaliaye masilahi yao. Jinsia ya kiume ilipewa hadhi ya juu ambayo ingeiwezesha kupata nafasi ya kutawala. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na mbili.

**_12. PROFESA WILLIAM LESAN_**

| | |
|---|---|
| *Lesan ko moche bandab tai.* | *Lesan anataka maendeleo.* |
| *Kipkorir ko moilotu chi.* | *Kipkorir hana mapendeleo.* |
| *Si tonon en Bomet en rubet.* | *Usimame hapa Bomet na utusaidie katika shida ya njaa.* |
| *Asi isoru bik en rubet kou Joseph en Misri.* | *Waokoe walio na njaa kama Yusufu kule Misri.* |

Msanii alimshauri mgombezi ajadiliane na wenyeji namna ya kuelekeza vijana katika mambo ya masomo, ukulima, afya na maendeleo kwa jumla. Alielezea umma kwamba Lesan alikuwa mwanaume aliyekuwa bingwa katika masomo na matibabu kwani shahada yake ya uzamifu ilikuwa kama fimbo iliyotumiwa na Musa katika Biblia. Musa aliyagonga maji ya Bahari Nyekundu na yakatawanyika halafu Wayaudi wakaweza kuvuka. Busara ambayo ingetumika na Lesan kama angefanikiwa ilimithilishwa na ya Musa kwani msanii alifafanua kwamba watu wangevukishwa, yaani, wangefaulu katika mambo yanayohitajika katika maisha kama vile ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Alitaja kwamba wakiwa na maendeleo kama hayo, wanaume wale wengine wangewaheshimu. Nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume yamesawirika katika wimbo huu.

(Carrigan na wengine 1985:595) waeleza kwamba kipengele kikubwa cha kuangazia somo kwa wanaume, ni lengo kuhusu mabadiliko ya kisaikolojia ya kijinsia. Walisisitiza kuwa hayawezi kutenganishwa na mahusiano ya kijamii ambayo yanakuza na kujenga ubabe-dume. Maelezo hayo yanasawirika katika sehemu ya wimbo nambari kumi na tatu.

**_13. PROFESA WILLIAM LESAN_**

| | |
|---|---|
| *Ong'alal ak bik ele kiribto barnotik ak keipto somanet.* | *Mjadiliane na wenyeji jinsi ya kutunza vijana na kuyaendeleza masomo.* |

| | |
|---|---|
| *Ak kerib emenyon ba kolele.* | *Na kutunza nchi yetu hadi ing'are.* |
| *Somanet ko i chonjo.* | *Kimasomo wewe ni bingwa.* |
| *Konyoiset ko i chonjo.* | *Kimatibabu wewe ni bingwa.* |
| *Digrii ne itindoi ko kerge ok* ***kiroki*** *kibo Musa.* | *Shahada ya masomo uliyo nayo ni kama* ***fimbo ile*** *ya Musa.* |
| *Kilondoi ra akechek.* | *Sisi tutafaulu wakati huu.* |

Lesan, akiwa mwanaume, alisifiwa na mwimbaji. Alieleza kwamba shahada ya masomo yake ilikuwa ya kuwaondolea watu ujinga katika Kaunti ya Bomet. Yeye angekuwa mfano mwema kwa watoto hususan wasichana. Hili ni dhihirisho kwamba jinsia ya kike iko nyuma katika masomo kuliko ya kiume. Hadhi yao imedhihirika kuwa chini ikilinganishwa na ya kiume. Ni wazi kwamba jinsia ya kiume bado huhodhi uwezo na mamlaka katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na nne.

***14. <u>PROFESA WILLIAM LESAN</u>***

| | |
|---|---|
| *Somaneng'ung profesa ko* ***sobunit*** *ne kiunen abusnatet.* | *Masomo yako Profesa Lesan ni* ***sabuni*** *ya kusafishia ujinga.* |
| *Si kwo ta somanet en logokyok che tibik.* | *Ili masomo yaendelee mbele hasa kwa wasichana wetu.* |

Wimbo unaofuata uliwahimiza wanaume wote kuweka amani mbele waweze kupiga kura kwa njia ifaayo. Hii ni amri ya wazee wa jinsia ya kiume. Walieleza kwamba ni vyema watu wawe na urafiki na waelewe kwamba maelewano ni fahali tangu enzi zile za mababu zetu. Watu wote washikane mikono wapate kuyatenda mambo mema yatakayokuwa taa katika jamii ya Wakalenjin. Wenyeji walishawishiwa wawe kitu kimoja kwa minajili ya kumwinua Lesan aliye mfupi kama buyu na kifuniko chake lakini ni mwenye hekima chungu nzima. Wimbo huu ulitukuza mwanaume kuashiria kwamba yeye ni mwenye mamlaka. Holmes (1997) afahamisha kwamba nafasi za utawala mara nyingi hushikiliwa na wanaume. Mikakati hii husimbwa na zinapotumika katika maingiliano, zinachangia katika uundaji wa ubabe-dume. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na tano.

***15. PROFESA WILLIAM LESAN***

| | |
|---|---|
| *Onginde kalyet tai murenchu.* | *Tuweke amani mbele enyi wanaume.* |
| *Profesa kochome amani.* | *Profesa anapenda amani.* |
| ***Kirgit** choruandit.* | *Urafiki ni **fahali.*** |
| *Ng'otut en boisiekyok.* | *Ni amri ya wazee wetu.* |
| *Kong'eten kuko ak baba.* | *Tangu enzi zile za mababu zetu* |
| *Ongekanabten kiptesot ak muget.* | *Tumwinue mtu huyu mfupi kama buyu na kifuniko chake.* |
| *Nyitat ng'omnotet.* | *Buyu hili limejaa hekima.* |

Tapnyole Rotich alimtetea mgombezi wa jinsia ya kiume aitwaye Kimutai aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge katika Kaunti ndogo ya Chepalungu mwaka 2017. Mada ya wimbo wake ilikuwa 'Wenye busara wang'ae'. Waliokuwa wakienda kumchagua mgombezi huyo, walikuwa wale wenye busara ambao walikuwa waking'aa kama mwangaza. Hii ilidhihirisha kwamba wenyeji walikuwa na imani kuwa mgombezi angekuwa mshindi katika kinyang'anyiro hicho. Waliona kwamba kiti hicho cha ubunge kilikuwa kikifaa mwanaume. Nadharia ya Ubabe-dume inaeleza kwamba majukumu ya kijinsia yamo ndani ya historia ya jamii na utamaduni wake. Waters (1989) afundua kuwa mabadiliko katika mifumo ya jinsia ya kiume kihistoria, yameathiriwa na mambo mengine katika jamii. Bila mambo hayo, mfumo huo ungejiendeleza namna ulivyokuwa tangu awali. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na sita.

| ***16. INGOLUU CHE NG'OMEN*** | ***WENYE BUSARA WANG'AE*** |
|---|---|
| *Ingoluu che ng'omen kou kakweng'et.* | *Wenye busara wan'gae kama mwangaza.* |
| *Ichek cheimuti Kimutai Parliament.* | *Ndio hao wanaopeleka Kimutai bungeni.* |
| *Kongoi we vijana,boisiek ak Chepyosok.* | *Asanteni vijana,wazee na kina mama* |
| *che kokokochi ng'echerani Kimutai.* | *waliompatia Kimutai kiti hiki.* |
| *Kokonyolun nge'cheret.* | *Kiti kimekufaa.* |

Yule mwimbaji alimsifu mgombezi akisema kwamba kazi yake nzuri aliyowatendea watu katika eneo hilo ilikuwa imetambulika. Alikuwa amewasaidia hata wanyonge. Kwa vile alikuwa

amemwona mgombezi akiingia bungeni, msanii alimsihi awakumbuke watu wake kwa kuwaongoza kwa amani na kuwaletea maendeleo. Udume ulidhihirika katika wimbo huu kwa namna ambavyo msanii, aliyewakilisha wenyeji, alimwona mgombezi akiwa na uwezo wa kuongoza. Walsh (1997) aeleza kwamba mwanaume hazaliwi na udume kama sehemu ya viungo vyake vya uzazi bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na saba.

***17. <u>INGOLUU CHENG'OMEN</u>***

*Kakisabin echek asi indochi Lungu*
*inyon.*
*Indochin en kalyet.*
*Kikeker boisieng'ung nebo NHIF.*
*Kiisoru che nyorotin.*

***<u>WENYE BUSARA WANG'AE</u>***

*Sisi tunakuunga mkono halafu*
*uongoze Lungu yetu.*
*Uingoze kwa amani.*
*Tumeona kazi yako ya NHIF.*
*Umewaokoa wanyonge.*

Titus Kosgei aliimba kuhusu Nathan Kirui aliyekuwa akigombea kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki mwaka 2017. Mgombezi mwenyewe alizungumza akijitetea kabla ya wimbo kuanza. Hilo ni dhihirisho kwamba mgombezi na msanii waliyaunda pamoja maneno yote ya wimbo. Katika wimbo huu, mgombezi alitumia saikolojia kushawishi wapiga kura kuwa yeye alikuwa na msimamo thabiti na mwenye hekima. Kupitia maneno hayo, alikuwa akilenga watu kumwamini kwamba angeungana nao na kufanya kazi pamoja. Iwapo wangemchagua, angewawakilisha kikamilifu katika bunge. Rejea wimbo nambari kumi na nane.

***18. <u>NATHAN KIRUI KITYO</u>***

*Otinye kayanet en muguleldanyuny.*
*Otinye komong'unet.*
*Inoni ko korwotitet ne inegen.*
*Otinye maketab keboisien tugul*
*kibagenge.*
*Okoswok, omwoitewok*
*ak oyoiywuok.*

***<u>NATHAN KIRUI PEKEE</u>***

*Ninayo imani rohoni mwangu.*
*Ninalo tumaini.*
*Hii ni ndoto ya kipekee.*
*Nathamani tufanye kazi pamoja*
*kwa umoja.*
*Nawasikiza, nawasemea*
*na kuwatendea.*

Katika wimbo wake, msanii alimtetea mgombezi akieleza kwamba huyo alikuwa mwanaume mpya aliye chipukizi na shujaa. Aliwaomba vijana, kina mama na wazee kumpatia kura zao kwa wingi. Alieleza kwamba yeye anaweza kazi na anaelewa uchumi kwani yeye ni mtu wa maendeleo. Aliwaambia watu kuwa yeye ni mwana wa mtu aliyekuwa akiitwa Simba na kwa hivyo, yeye pia ni simba, yaani, shujaa kama baba yake. Sifa zilizoelezwa na msanii kuhusu mgombezi ziliakisi uhodari na nguvu zake kama mwanaume anayestahili kuwa mbunge. Rejea sehemu ya wimbo nambari kumi na tisa.

| | |
|---|---|
| ***19. NATHAN KIRUI KITYO*** | ***NATHAN KIRUI PEKEE*** |
| *Kikochini ra chito nyiganet neto koming'in.* | *Tutampatia wakati huu shujaa aliye chipukizi.* |
| *Chitab maendeleo, kijanayat ne nomeke ak kasit.* | *Ni mtu wa maendeleo, kijana anayewezana na kazi* |
| *Arwetab* ***Simba.*** | *Mwana wa* ***Simba.*** |

Richard Cheselet aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge wa wadi, alipigiwa debe na msanii aitwaye Kachwes Rotich mwaka 2017. Aliwasihi wananchi wampigie kura tena kwa sababu ni mwanaume aliye na roho safi na hana ubaguzi wala ukabila. Matendo yake yameonekana wazi tangu awe kwenye kiti hicho 2013 kama vile kujenga barabara, shule na kuleta pesa ya serikali ya kusaidia wanafunzi shuleni. Maelezo ya msanii yamedhihirisha uwezo aliokuwa nao mgombezi katika kazi yake tangu 2013. Wimbo huu unaukuza ubabedume kulingana na jinsi ambavyo msanii aliwashawishi wapiga kura kumchagua tena yule mgombezi. Wanajamii huamini kwamba uongozi unamfaa mwanaume, jambo lililokolea kwenye akili zao. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini.

| | |
|---|---|
| ***20. <u>OLOL MASANI (CHESELET)</u>*** | |
| *Olewen chi tugul Cheselet koik MCA kototen.* | *Nyote mchague Cheselet awe MCA mara nyingi.* |
| *Chi ne mie mugulel.* | *Ni mtu mwenye roho safi.* |

| | |
|---|---|
| *Motinye ubaguzi ako motinye ukabila.* | *Mtu asiye na ubaguzi wala ukabila* |
| *Barabarosiek ko miach, ng'alekab sugul, ak bursaries.* | *Barabara ni nzuri, amejenga shule na ameleta 'bursaries.'* |
| *Bikab Olol Masani, ongeketyin Cheselet.* | *Watu wa Olol Masani, tumrudishe Cheselet kitini.* |

Kachwes alimtetea Cheselet kupitia methali. Alieleza kwamba kuna mhenga aliyesema kuwa haifai mtu yeyote mwenye akili timamu kujikinga kwenye mti fulani kukiwa kunanyesha kisha mvua ikikoma, aukate mti huo. Alifahamisha kwamba yeyote aliye na ng'ombe ampatiaye maziwa mengi, asithubutu kumwacha na kujaribu kumtafuta ng'ombe mwingine tofauti asiyemjua. Ni afadhali aendelee kumkama yule yule amemzoea kuliko kumtafuta yule usiyemjua. Msanii alieleza hivi akiyafananisha na matendo mema ya Cheselet. Alimtetea akisema kuwa mgombezi anawapenda watoto, wazee na hata walemavu. Alimpatia moyo aendelee na uongozi uo huo wake mwema kama vile Musa alivyowaongoza Waisraeli katika Biblia. Wimbo huu ulikuwa ukiwashawishi wapiga kura wampigie tena yule mgombezi wa kiume. Jambo hili lilikuwa likiendeleza na kudumisha utawala wa jinsia ya kiume kama tulivyoelezwa na Connell (1987). Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na moja.

### *21. <u>OLOL MASANI (CHESELET)</u>*

| | |
|---|---|
| *Kikamwa boiyon kole **meyumen sosur ye moen iyeb.*** | *Mhenga alisema **usijikinge katika 'sosur' kukinyesha na kuukata mvua ikikoma.*** |
| *Yon karibai teta ako igosu chego ko mebwat ile awalda asi awal butiot.* | *Ukimfuga ng'ombe aliye na maziwa mengi usifikirie ubadilishe upate mwingine tofauti.* |
| *Cheselet kochome ne ming'in, ne kakoyosit okot solomwet.* | *Cheselet anampenda aliye mdogo, aliyezeeka na hata mlemavu.* |
| *Ongeketyin we bikyok.* | *Tumrudishe tena kwenye kiti.* |
| *Indochin bikuk kou Musa we Richard Cheselet.* | *Waongoze watu wako kama Musa ewe Richard Cheselet.* |

#### *4.2.1.2. Hitimisho*

Kupitia nyimbo zilizochanganuliwa na kufasiliwa katika sehemu hii, iligundulika kwamba utawala wa jinsia ya kiume umedumishwa na wa kike bado unajitafutia nafasi yake katika jamii. Jambo hili limelandana na namna ambavyo nadharia ya Ubabedume yaeleza kwamba nguvu na mamlaka yanamilikiwa na jinsia ya kiume kulingana na utamaduni wa jamii husika. Wasanii wengi wa jinsia ya kiume waliimba nyimbo za kampeni za kisiasa kuliko jinsia ya kike. Kulikuwa na waimbaji wa jinsia ya kiume waliopigia debe wagombezi wa jinsia zote mbili. Wagombezi wa jinsia ya kiume walikuwa wengi kuliko wa kike.

Nyimbo za kampeni za kisiasa ni za kuburudisha, kuelimisha, kuhamasisha, kushawishi, kuunganisha watu katika jamii na kuwashikamanisha wanachama wa chama fulani angalua chama chao cha kisiasa kipate kuwa na nguvu. Katika nyimbo hizi, kila msanii alikuwa akimsifu mgombezi kwa njia ya kipekee, mgombezi awe wa jinsia ya kike au ya kiume. Wale ambao wangeweza kudhihakiwa katika nyimbo ni wagombezi ambao wasanii hawakutaka kuwaunga mkono. Nyimbo kadhaa ziliiwaelezea wananchi kuhusu nguvu za wagombezi kisiasa hususan kupitia sera zao. Wananchi waliahidiwa kwamba wangeletewa maendeleo makubwa kama vile kuletewa maji na umeme, kujengewa shule, hospitali na barabara, kuwalipia karo watoto wa wazazi wasiojiweza, kuwasaidia vijana kupata ajira, na kuwasaidia hata walemavu. Vilevile, kupitia nyimbo hizo wananchi waliwaelezea wagombezi matatizo waliyo nayo ambayo wangependa yatatuliwe. Baadhi ya wagombezi wengine walikuwa wakiwasilisha jumbe zao wao wenyewe kupitia nyimbo wakifahamu kwamba ni vigumu watu kusahau maneno ya wimbo kama ya mazungumzo. Wasanii wengine waliwatetea wagombezi wengine wapigiwe kura tena kuambatana na kazi waliyofanyia watu katika miaka mitano iliyopita. Waliotaka kugombea viti vya kisiasa hususan walikuwa wa jinsia ya kiume.

### *4.2.2 Mahusiano ya Uwezo Kijinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa*

Wamitila (2003) aeleza kwamba maudhui yanayopatikana katika nyimbo za kampeni za kisiasa hasa ni zile zinazo kiwango kikubwa cha mfumodume. Nia za nyimbo hizi hasa ni kuwasilisha ujumbe kuhusu mgombezi.

#### *4.2.2.1 Siasa ya Kijinsia*

Siasa ya kijinsia inahusishwa na mfeministi Kate Millet katika kitabu chake ambacho aliandika 1978. Anatumia dhana hii kuonyesha jinsi tofauti za kijinsia na uana zinavyokuwa na mchango katika muundo wa kijamii wa mfumo wa ubabedume kuanzia uchumi hadi muundo wa kijamaa, visasili hadi dini. Naye Mclaughlin (1990:155) katika Jarida la Mulika, anadai dhana ya mwanamke kwa uhalisia wake ni dhana ya kisiasa. Haielezi uana pekee bali inaeleza hadhi na nafasi yake katika jamii. Wimbo ufuatao unahusika na siasa ya kijinsia. Wimbo huu uliimbwa na msanii maarufu wa kabila la Kalenjin marehemu Kipchamba Arap Tapotuk. Anaeleza kwamba mwanaume hapaswi kusikia maneno ya mwanamke kwani maneno yao ni akili iliyomo upande wa kushoto. Alifafanua kwamba mwanaume yuko mbele katika asasi zote za kijamii na mwanamke humfuata nyuma daima. Wimbo huu unaidhalilisha jinsia ya kike huku ukitukuza ya kiume. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na mbili.

| ***22. MUREN*** | ***MWANAUME*** |
| --- | --- |
| *Ng'al chebo kwonyik ko mokisibi mureno.* | *Mwanaume hapaswi kusikia maneno ya wanawake.* |
| *Ng'alekab kwonyik angot kisib kosurtos bik.* | *Maneno ya wanawake yakifuatwa yatakosanisha watu.* |
| *Ng'alekwak ko ng'omnotet ne mi katam.* | *Maneno yao ni akili iliyomo upande wa kushoto.* |
| *Mwaat kong'eten keny kele indochin kwony mureno.* | *Inasemekana kutoka zama za zama kwamba mwanamke anaongozwa na mwanaume.* |
| *Ng'omnotetab muren kosibi neutab ta.* | *Akili ya mwanaume inafuata mkono wa kulia.* |
| *Nebo kwonyik kosibi nebo katam.* | *Ya mwanamke hufuata wa kushoto.* |
| ***Mildoke kityo mukungonik ko one nebo ta kipkoi.*** | ***Magurudumu ya nyuma yanakimbiza ya mbele milele.*** |

#### *4.2.2.2 Kinyang'anyiro cha Kiti cha Urais*

Matokeo ya uchaguzi wa kitaifa katika Kaunti ya Bomet, yameonyesha kwamba wanaume wengi huchaguliwa kuliko wanawake. Uwezo kijinsia ni mhimili wa pili ya nadharia ya Ubabedume

uliomwezesha mtafiti kueleza namna nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri mahusiano ya uwezo kijinsia.

Richmond (1992) asisitiza kuwa jamii ni taasisi muhimu ambayo hujenga na kuratibu majukumu na shughuli za kijamii kiuana. Nadharia ya Ubabedume huwa inaangazia jinsi majukumu ya kiuana hufungamanishwa na tofauti za kibiolojia, uwezo na hadhi. Msanii aitwaye Jeremiah Kosgei katika wimbo wake, alimsihi Ruto aendelee kumwunga mkono Kenyatta kuongoza nchi ya Kenya kama rais hadi kipindi chake kiishe halafu ashike usukani. Hili ni dhihirisho kwamba inatabiriwa kuwa rais wa nchi ya Kenya atakuwa wa jinsia ya kiume miaka mingi ijayo. Ruto alitajwa kama shujaa amwuaye simba akiwa ananguruma. Huu ni ukuzaji na uhalalishaji wa ubabe-dume kwa kuuendeleza uwezo wake. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na tatu.

***23. <u>JUBILEE</u>***

| | |
|---|---|
| *Kiwegun kongoi Samoei en kasetab it.* | *Tunakushukuru Samoei kwa utiifu wako.* |
| *Bokokyin Uhuru kotwoisiok.* | *Umwachie Uhuru atimize.* |
| *Si ngemi tai ko likwobit sumenyon.* | *Halafu kuweko na mwelekeo mbeleni.* |
| *Kongoi mising nyiganenyon.* | *Asante sana shujaa wetu.* |
| ***Bar ng'etundo ko rose*.** | ***Amwuaye simba anayenguruma.*** |

Frosh na wengine (2004) waeleza kwamba mwanaume huhusishwa na madaraka ya juu, uwezo thabiti na mshindani katika jamii. Maelezo haya yanasawirika katika wimbo wa Jeremiah Kosgei. Ruto kama mwanaume, alitumwa ampeleke Uhuru ambaye ni mwanaume mwingine kwenda kutakaswa na wazee wa kiume wa Kalenjin. Alikuwa anahitajika atakasike ili apate uwezo thabiti wa kulinda nchi ya Kenya. Alifananishwa na Daudi, mwana wa Jesse. Daudi alikuwa mfalme tajika wa Wayaudi aliyetenda makuu kule Uyaudi. Aliimarisha nasaba iliyodumu kwa miaka mia nne iitwayo Nasaba ya Daudi. Vilevile, alikuwa na nguvu nyingi aliyopewa na Mungu iliyomwezesha kumwua Goliathi. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na nne.

***24.*** ***JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kokiyokten Samoei Arap Ruto.* | *Tunakutuma Samoei Arap Ruto.* |
| *Asiimutwech Uhuru konyo Kapkatet.* | *Uende utuletee Uhuru nyumbani Kapkatet.* |
| *Si kikochin mwaita nebo Kalenjin.* | *Ili tumtakase kwa mafuta ya Kalenjin.* |
| *Kou weritab Jesse nemi Bible.* | *Kama mwana wa Jesse katika Biblia.* |
| *Si koribwech emet.* | *Yeye apate kutulindia nchi.* |

Nyimbo za kampeni za kisiasa zinatumika kama sifo za kusifia viongozi waadilifu na mashujaa. Msanii aliendelea kumsifu na kumwombea Ruto ale chumvi nyingi apate kutawala kwa muda mrefu wakati wake ukiwadia. Alifahamisha kuwa Ruto ni ndume na baba ya jamii ya Kalenjin. Huu ni wimbo udhihirishao namna mwanaume anaweza kulinda na kuongoza wanajamii. Carrigan, Connell na Lee (1985) na Messner (1990) waeleza kwamba ubabedume ni desturi ya kuishi kwa watu inayosababishwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi na kiutamaduni, na hutegemea mipango ya kijamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na tano.

***25.*** ***JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kongoi mising Samoei Arap Ruto.* | *Asante sana Samoei Arap Ruto.* |
| *Kisoun any kot iween kutungoi.* | *Tunakuombea uishi miaka mingi.* |
| *Asi rib gaa.* | *Upate kulinda jamii.* |
| *Kongoi **kirginyon** weritab Kalenjin.* | *Asante **fahali** yetu mwana wa Kalenjin.* |
| *Kitienge babanyon.* | *Tunakutegemea baba yetu.* |

Kipkurui Ng'eny alimtetea William Ruto katika wimbo wake wenye mada 'Asante Arap Ruto, shujaa wetu'. Ruto alisifika kama shujaa wa Kalenjin mwenye uwezo mwingi wa kuilinda mipaka yote, kuwa baba wa mayatima na kuwasaidia maskini. Vilevile, alihimizwa awe anakaa na wazee wa jinsia ya kiume ili apewe mawaidha. Mawazo haya yanaandamana na maelezo ya Uchendu (2005). Alieleza kwamba mwanaume hutamani kuwa na mamlaka ya uamuzi, kulinda wanyonge, kuwa na msimamo thabiti, mwenye hadhi ya juu katika jamii, mwenye akili na hekima na kutoonyesha mhemko. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na sita.

***26. KONGOI ARAP RUTO NYIGANET***

*Kongoi Arap Ruto nyiganenyon.*
*Telel we nyiganenyon.*
*Telel we nyiganetab Kalenjin.*
*Ribwech che seretos, ribwech che motinye sikik.*
*Iweigu babanyuan.*
*Indochin bikab Kalenjin kot iit Tugen*
*ak Markweta.*

***ASANTE SHUJAA ARAP RUTO***

*Asante Arap Ruto shujaa wetu.*
*Simama imara shujaa wetu.*
*Simama shujaa wetu wa Kalenjin.*
*Uwatunze maskini, ututunzie mayatima.*
*Uwe baba yao.*
*Uwaongoze Wakalenjin mpaka kwa Watugen*
*na Wamarakwet.*

Aswani na wengine (2014) wafahamisha kwamba mahusiano ya kiuwezo ya kijinsia yameacha hiba kwa jinsi ambavyo wanaume humiliki uwezo mkubwa katika rasilimali za jamii. Mwanaume huwa na haki zaidi ya mwanamke katika masuala mbalimbali yanayohusu asasi ya jamii ya mfumodume. Suala hili linalingana na namna ambavyo dhana ya jinsia inavyojitokeza katika nyimbo hizi za kampeni. Wasanii waliojiita 'Shuttle Sisters' walimpigia debe Ruto kuwa naibu wa Kenyatta wakati wa malumbano ya kisiasa ya 2013. Ruto alitambulika kama shujaa maarufu nchini Kenya. Alihimizwa afuate nyayo za Mstaafu Hayati Arap Moi wakati wake wa kutawala nchi ya Kenya ukifika. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na saba.

***27. URP***

*Nyiganenyon Ruto, koriborjige kot iboru*
*chamaitab URP.*
*Bikab Kenya tugul, okusyikong Arap Ruto.*
*Momi bororiet Kenya ne moingen*
*kainetab Samoei.*
*Mo meten Mungu.*
*Ye indochi emenyon, ibur kou*
*baba Moi.*

*Shujaa wetu Ruto,umejitahidi hadi ukaunda*
*chama cha URP.*
*Watu wote wa Kenya, mkumbuke Arap Ruto.*
*Hakuna jamii nchini Kenya isiyolitambua*
*jina la Samoei.*
*Mungu hakutupi.*
*Utakapoongoza nchi yetu, ukae kama*
*baba Moi.*

Marion Chelang'at ni mwimbaji aliyetetea Muungano wa Jubilee, William Ruto, Joyce Laboso na wagombezi wengine wa muungano huo. Ruto alitajwa kama fahali, kifungua mimba na shujaa

ainuaye mlima. Walishauriwa wasiwahi kushtuliwa na wanaume wengine. Laboso alielezewa kwamba yeye anapendezeka akiambiwa kuwa hata kama maziwa yanahitajika si lazima kuweko na ndume. Ingawa mwimbaji alizisawiri jinsia zote katika kazi yake, jinsia ya kiume ilijitokeza kuwa na nguvu zaidi kuliko ya kike. Walsh (1997) afafanua kwamba udume hubainika bayana katika misingi ya uhuru wa kijinsia, ushari, ushindani na uwezo wa kutawala, kuamuru na kuzuia. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na nane.

***28. JUBILEE OIYE***

| | |
|---|---|
| *Kitindoi taitanyon.* | *Tunaye kifungua mimba yetu.* |
| *Robe morik si tun ketilchi.* | *Anaungana mkono ili aungwe baadaye.* |
| *Kiwegun kongoi Samoei.* | *Tunakushukuru Samoei* |
| *Kole vijana 'Igaske ii* ***kirginyon kipkeleny tulwo.'*** | *Vijana wamesema, 'Ujihisi* ***fahali yetu ainuaye mlima.'*** |
| *Kirginyon ne ingosil ke yebchin it.* | *Fahali yetu ambaye akilia hutegewa masikio.* |
| *Ongeti konyon si koron keluen chego.* | *Tutunze nyumba yetu keshoye tunywie maziwa.* |
| *Amat oywei kwanechon mengimuok.* | *Msiogope wale wanaume wengine, msishtuliwe.* |
| *Omwochin Chemaluk chamat mising.* | *Mmwambie Chemaluk kuwa anapendezeka sana.* |
| *Ngandan kimoche chego ko ma lazima kirgit.* | *Ingawa tunataka maziwa, si lazima kuwe na ndume.* |
| *Kimoche tuguk che lelach.* | *Tunataka vitu vipya.* |
| *Ongele kiwole o en Bomenyon.* | *Tuseme tatabadilisha katika Kaunti ya Bomet.* |
| *Gavana ko Joyce.* | *Gavana ni Joyce.* |

#### *4.2.2.3 Sifo ya Muungano wa NASA*

Habermas (1977:259) atufafanulia kwamba lugha ni msimbo unaomiliki na kudhihirisha mahusiano ya kiuwezo na kiutawala katika jamii. Lugha hutumika katika kuhalalisha mahusiano ya kiuwezo katika jamii. Aidha, lugha huhodhi historia na itikadi za jamii. Kupitia wimbo ulioimbwa na msanii aliyejiita Sweet Star, tunayapata maelezo haya.

Mwimbaji huyo alikuwa akitetea Muungano wa NASA ( National Super Alliance) uliokuwa ukiongozwa na Raila katika malumbano ya kisiasa ya 2017. Muungano huu uliundwa na vyama vingi, ulikuwa na nguvu na ulikuwa ukipambana na Muungano wa Jubilee. Uwezo wa jinsia ya kiume ilisawirika katika wimbo huo. Rejea sehemu ya wimbo nambari ishirini na tisa.

***29. <u>NASA TIBIM</u>***

*Tugetab NASA, NASA Tibim.*
*Baba Raila, Raila Tibim.*
*Kalonzo Musyoka, Wiper NASA Tibim.*
*Mudavadi NASA, NASA Tibim.*
*Tugetab NASA, NASA Tibim.*
*Baba Raila, Raila Tibim.*
*Isaac Ruto, Mashinani, NASA .*
*Orengo, Kidero, NASA, NASA.*
*Wetangula, Ntutu Narok, NASA, Intuita Lala.*
*Hassan Joho, Gavana Mombasa, NASA.*
*Zakayo Cheruiyot, Kuresoi, NASA.*
*Mochesanen emenyon leiye, NASA Tibim.*
*Kakiam okwoindab emet en NASA Tibim.*
*Emenyon mokiwole en NASA Tibim.*
*Serkali koki nenyon en NASA Tibim.*

*Sauti ya NASA NASA Tibim.*
*Baba Raila,Raila Tibim.*
*Kalonzo Musyoka, Wiper, NASA Tibim.*
*Mudavadi NASA, NASA Tibim.*
*Sauti ya NASA NASA Tibim.*
*Baba Raila, Raila Tibim.*
*Isaac Ruto, Mashinani, NASA*
*Orengo, Kidero ,NASA, NASA .*
*Wetangula, Ntutu, Narok, NASA Intutia Lala.*
*Hassan Joho Gavana Mombasa, NASA .*
*Zakayo Cheruiyot,, Kuresoi, NASA .*
*Msichezee nchi yetu nyie, NASA Tibim.*
*Tule kwenye nchi yetu yenye rutuba kupitia NASA Tibim.*
*Nchi yetu haiwezi kubadilishwa ni NASA Tibim.*
*Serikali ilikuwa yetu kupitia NASA Tibim.*

#### *4.2.2.4 Kampeni ya Kiti cha Ugavana*

Jinsia ya kike imesawirika katika wimbo uliotungwa na msanii aitwaye Ben Bii. Alimpigia debe marehemu Laboso aliyekuwa akigombea kiti cha ugavana katika Kaunti ya Bomet mwaka wa 2017. Aliwaambia watu wa Kaunti ya Bomet waamke kwa sababu kumekucha na kwa hivyo wanataka mabadiliko katika kaunti hiyo. Badiliko lenyewe ni kumpokea Laboso kuwa gavana. 'Daktari Joyce Laboso, Kaunti ya Bomet, Mama na Kazi' ilikuwa anwani ya mtunzi huyo. Dhamira yake ilikuwa kumtetea mgombezi huyu katika kinyang'anyiro hiki. Alieleza uwezo na msimamo wa mgombezi katika sehemu ya wimbo nambari thelathini.

***30. <u>DR. JOYCE LABOSO BOMET MAMA NA KAZI</u>***

| | |
|---|---|
| *Bikab Bomet Kounti, ong'et kakoech emet.* | *Watu wa Kaunti ya Bomet, mwamke kumekucha.* |
| *Kogeger konyone walet.* | *Tumeona mabadiliko yaja.* |
| *Dr. Joyce Laboso ne koketach koik Gavana.* | *Tumempokea Dkt. Joyce Laboso kuwa Gavana* |

Maudhui tunayoyapata katika nyimbo za kampeni za kisiasa ndiyo yale ambayo yanapatikana katika jamii anuwai za kiafrika hususan zilizo na kiwango kikubwa cha mfumodume. Kupitia nyimbo hizi na pia kazi nyingine za kifasihi, hadhi na nafasi ya jinsia ya kike husawirika. Katika wimbo ule ulioimbwa na Ben Bii, wanawake watatu pekee walisawirika kati ya wanaume kadhaa. Wanawake hawa ili wapate kuwa maarufu kisiasa kulingana na wimbo huu, walikuwa katika Mrengo wa Jubilee ulioimarika na kuwa na nguvu zaidi kuliko vyama vingine vyote kote nchini Kenya. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na moja.

***31. <u>DR. JOYCE LABOSO BOMET KAUNTI MAMA NA KAZI</u>***

| | |
|---|---|
| *Kongoi en kondoikyok.* | *Asante kwa viongozi wetu.* |
| *Kokelewen en chamaitab Jubilee.* | *Wameichaguliwa katika Muungano wa Jubilee* |
| *Kondochin Joyce Laboso.* | *Wakiongozwa na Joyce Laboso.* |
| *Kiwole ra kele kiwole.* | *Tutabadilisha wakati huu tutabadilisha.* |

*Dr Christoper Lang'at komi.* / *Dkt. Christopher Lang'at akiwemo.*

| | |
|---|---|
| *Dr Christoper Lang'at komi.* | *Dkt. Christopher Lang'at akiwemo.* |
| *Beatrice Kones komi.* | *Beatrice Kones akiwemo.* |
| *Komi Engineer Kosgei.* | *Injinia Kosgei akiwemo.* |
| *Women Rep. Joyce Korir.* | *Joyce Korir Mwakilishi wa wanawake.* |
| *Komi Paulo Savimbi.* | *Paulo Savimbi akiwemo.* |
| *Dr. Hillary Barchok.* | *Dr. Hillary Barchok.* |
| *Ronald Kiprotich Tonui.* | *Ronald Kiprotich Tonui.* |
| *Komi Brighton Konoin.* | *Brighton Konoin akiwemo.* |
| *Tugetab ng'omnotet o papa.* | *Hii ni sauti ya busara pappa.* |
| *Walaken anan komataikany si kewalin.* | *Badilika ama ungoje ubadilishwe.* |

Wimbo unaofuata unaeleza kwamba wanawake ni mwangaza na wanaweza kuleta maendeleo katika jamii. Msanii alieleza kwamba Joyce Laboso ni mwanamke na anatarajiwa kuwa gavana ili afagie Kaunti ya Bomet hadi ing'are. Msanii huyo aliwasihi watu kuleta mabadiliko katika mtindo wa kuchagua viongozi wa kisiasa bila kujali aina ya jinsia mradi tu wapate huduma ifaayo. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na mbili.

### *32. __DR. JOYCE LABOSO BOMET COUNTY MAMA NA KAZI__*

| | |
|---|---|
| *Kwonyik ko loboiyet.* | *Kina mama ni mwangaza.* |
| *Chu ko sitimok.* | *Hawa ni stima.* |
| *Okweng'wech Bomet amakichut keringonik.* | *Mtumulikie Bomet ili tusiingie mashimoni.* |
| *Kondoikyok, asi oyoiywech maendeleo.* | *Viongozi wetu, mtufanyie maendeleo.* |
| *Nyone walet choruenyun.* | *Mabadiliko yanakuja rafiki yangu.* |
| *Joyce Laboso, Gavana nebo Bomet Kounti.* | *Joyce Laboso Gavana wa Kaunti ya Bomet.* |
| *Chepyoset o papa.* | *Ni mwanamke o papa.* |
| *Ibuch Bomet kwo kotililit.* | *Fagia Bomet hadi ing'are.* |

Kikundi cha kina mama waliojiita Chama cha Mashinani (CCM), kilionyesha uwezo na mafanikio aliyokuwa nayo Isaac Ruto ambaye alikuwa akigombea kiti cha ugavana mwaka wa

2017. Alikuwa anapambana na marehemu Laboso katika kinyang'anyiro hicho. Yeye alikuwa gavana wa Kaunti ya Bomet kuanzia 2013. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na tatu.

***33. <u>GAVANA KO ISAAC ARAP RUTO</u>***

*Gavana ko Arap Ruto.*
*Kiribwech kounti Arap Ruto kot kegas en Kenya.*
*Kikoik chairman Arap Ruto en 47.*
*Boiboiyet ne tiana yon kiketyi kora Arap Ruto.*

***<u>GAVANA NI ISAAC ARAP RUTO</u>***

*Gavana ni Arap Ruto.*
*Arap Ruto ametulindia kaunti hadi ikasikika nchini Kenya.*
*Arap Ruto akawa mwenyekiti akiwa 47.*
*Ni furaha iliyoje Arap Ruto akirudishwa tena.*

Waimbaji walitaja kazi yote ambayo Ruto alikuwa amefanya na hivyo basi walimwunga mkono agombee kiti hicho tena. Walieleza kuwa yeye hana mapendeleo na amewaajiri vijana wengi katika Kaunti ya Bomet. Ameweza kununua ambulensi na kujenga shule pamoja na uga. Malumbano hayo yanawahitaji mashujaa kama yeye kwani yeye ni jasiri mfano wa moto. Anastahili kuwa kiongozi. Wimbo huu umeonyesha namna mwanaume anamiliki uwezo mkubwa kisiasa katika jamii. Ubabedume, kulingana na maelezo ya Chapman na Rutherford (1988), huhusika na namna fulani ya kuwatawala wanawake. Kwa maoni yao, ubabedume huambatana na uwoga mkubwa wa wanaume kwa wanawake. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na nne.

***34. <u>GAVANA KO ISAAC ARAP RUTO</u>***

*Kiketwech ambulens ne toreti*
*chi tugul.*
*Kikosir vijana Arap Ruto, boiboiyet*
*netiana!*
*Motinye kolotunet Arap Ruto.*
*Kitekwech kiwanjet Arap Ruto*
*neu Kasarani.*
*Kitekwech sugulisiek.*

***<u>GAVANA NI ISAAC ARAP RUTO</u>***

*Ametuletea ambulensi inayosaidia*
*kila mtu.*
*Arap Ruto amewaajiri vijana, ni*
*furaha iliyoje!*
*Arap Ruto hana mapendeleo*
*Ametujengea uga unaofanana*
*na Kasarani.*
*Ametujengea shule.*

*Kongoi Kipnyole Arap Ruto.*
*Nyoljin kandoinatet.*
*Kimitos ra tugul,ne moche nyigonik.*
*Kongoi nyiganenyon neu mat.*

*Asante Kipnyole Arap Ruto.*
*Anastahili kuwa kiongozi.*
*Uongozi huu unang'ang'aniwa na wengi, unahitaji mashujaa.*
*Asante shujaa wetu aliye kama moto.*

Ras Wageni alifafanua kwamba Ruto ni fahali wa Kalenjin ambaye ameungana na watu wa Kenya na ameleta maendeleo katika kaunti yake. Alieleza kuwa aliwatetea watu wa Mau na wakapata haki yao. Yeye ni baba yao na hawezi akashtuliwa kwa ngozi. Msanii alisawiri ushujaa, uwezo na msimamo wa Isacc Ruto ambaye alikuwa akigombea kiti cha ugavana katika Kaunti ya Bomet mwaka wa 2017. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na tano.

***35. <u>CHAMA CHA MASHINANI</u>***

*Kongoi kirginyon.*
***Ingosil** koitu tuguk gaa.*
*Weche kongoi Kalenjin en tononeng'ung.*
*Kiiyan otonose ak bikab Kenya komugul.*
*Kongoi nyiganenyon Isaac Ruto en chamainyon Mashinani.*
*Kin itweku, konyorchige imanda bikab Mau.*
***Magimuenen magatet.***
*Kongoi any babanyon.*

*Asante fahali yetu.*
***Akilia** vitu vinafika nyumbani.*
*Wakalenjin wanakushukuru kwa msimamo wako.*
*Umekubali kusimama na watu wote wa Kenya nzima.*
*Tunakushukuru shujaa wetu Isaac Ruto kwa chama chetu cha Mashinani.*
*Uliponena, watu wa Mau wakapata haki yao.*
***Hushtuliwi kwa ngozi**.*
*Asante baba yetu.*

#### *4.2.2.5 Kampeni ya Kiti cha Useneta*

Walsh (1997) afafanua kwamba katika jamii za kiafrika, udume huhusishwa na uwezo wa mwanaume kuwa na mafanikio, kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Maelezo ya mtaalamu huyu yanalandana na wimbo uliotungwa na Arumutik Kosgei. Msanii huyo alimtetea

Lesan ambaye alikuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet. Alifahamisha kwamba Kaunti ya Bomet inahitaji mtaalamu atakayeing'arisha kwa hekima yake. Alieleza kuwa Lesan ni maarufu na amebarikiwa na wazee wa kiume apate kulinda pembeni. Alihimizwa awalishe watu wake namna Yusufu alitenda kule Misri. Lesan ni ngao, taa na macho yao. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na sita.

***36. PROFESA WILLIAM LESAN***

| | |
|---|---|
| *Asi ketech ba kolili Bomet Kounti, ko moche chito ne somanat.* | *Tukitaka tujenge Kaunti ya Bomet hadi imetemete, tunahitaji mtaalamu.* |
| *Somananing'ung Profesa ko* ***sobunitab*** *Bomet Kounti.* | *Profesa masomo haya yako ni* ***sabuni*** *ya Kaunti ya Bomet.* |
| *Si kotililit bororienyon en ng'omnotet.* | *Ili Kenya yetu itakasike kihekima.* |
| *Ko kogonin boisiek* ***ng'ulek.*** | *Wazee wamekupatia* ***mate.*** |
| *Seneta nenyon ko Kipkorir ne kikeren sormotiek si koribwech emet.* | *Seneta wetu ni Kipkorir ambaye tumemweka pembeni ili atulindie nchi.* |
| ***Tainyon*** *ne lole bet ak kemoi kot kotok Bomet Kounti.* | ***Taa*** *yetu inayowaka usiku na mchana hadi Kaunti ya Bomet ijulikane.* |
| *Asi koribwech malikyok ama chesanen bik alak.* | *Atutunzie mali yetu yasichezewe na watu wengine.* |
| *Ma kitisioni en tai yun.* | *Huwezi ukatishwa hata kidogo hapo mbeleni.* |
| *Seneta nenyon ko ne motumtumokse matiny.* | *Seneta wetu hawezi kutingishika kamwe.* |
| *Boisiek kongenin, chepyosok kongenin, logok kongenin akot ne werto kongenin.* | *Wazee wanakujua, kina mama wanakujua na hata wapita njia wanakujua.* |
| *Profesa Lesan kochome bandab tai ako moilotu chi.* | *Profesa Lesan anapenda maendeleo na hana mapendeleo.* |
| *Ine ko* ***long'enyon*** *nemi tai asi koik konyek en tai.* | *Yeye ni* ***ngao*** *yetu na macho yetu katika siku za usoni.* |
| *Ng'otut en boisiekyok kole kirgit kosyinet.* | *Wazee wanaelewa kwamba maelewano ni fahali* |

#### *4.2.2.6 Kampeni ya Kiti cha Ubunge*

Tannen (1990) aeleza kwamba wanaume hutumia lugha apate kuboresha utawala na uhodhi wa kijamii. Wao huonyesha madaraka na kuona mazungumzo kama njia ya kupata matokeo yafaayo. Mazungumzo yao hayanuiwi kujenga uhusiano wowote wa kijamii bali ni ya kupitisha ujumbe kuonyesha nguvu, utawala na uhodhi. Wazo hili linapatikana katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Titus Kosgei wakati wa kampeni ya kisiasa ya mwaka 2017. Alikuwa akimwunga mkono Nathan Kirui aliyekuwa akigombea kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki. Kabla ya wimbo kuanza kuimbwa, mgombezi mwenyewe aliwazungumzia wananchi. Alidhihirisha nguvu zake za utawala kwa wenyeji kama angechaguliwa. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na saba.

***37. <u>NATHAN KIRUI KITYO</u>***

*Okotok tugul bikab borienyon,*
*Kong'asis ne lel.*
*Inoni ko kurset ne inegen.*
*Otinye kayanet en muguleldanyun.*
*Otinye komong'unet.*
*Inoni ko korwotitet ne inegen*
*Otinye magetab keboisien tugul kibagenge.*
*Okoswok, omwoitewok ak oyoiywok.*

***<u>NATHAN KIRUI PEKEE</u>***

*Nawasalimia watu wote wa Bomet yetu,*
*Kongasis mpya.*
*Huu ni mwito wa kipekee.*
*Ninayo imani rohoni mwangu.*
*Ninalo tumaini.*
*Hii ni ndoto ya kipekee.*
*Ninathamani kufanya kazi pamoja nanyi. kwa umoja.*
*Nawasikiza, nawasemea na kuwatendea.*

Msanii alieleza kwamba mwanaume chipukizi aliye shujaa anahitajika. Alisema kwamba Kirui ana uwezo wa kuwatafutia kazi vijana na kina mama. Mgombezi alisifika juu ya nguvu zake kisiasa na utawala wake. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na nane.

***38. <u>NATHAN KIRUI KITYO</u>***

*Kikochin ra nyiganet ne to koming'in, Nathan Kirui.*

***<u>NATHAN KIRUI PEKEE</u>***

*Tutampatia wakati huu shujaa aliye chipukizi, Nathan Kirui.*

*Chitab maendeleo, kijanayat ne nomeke ak kasit.*
*Arwetab* ***Simba.***
*Chitab maendeleo, kosich bik che meng'ech kasisiek.*
*Koyai kwonyik mung'aret ak kobotisiet.*

*Mtu wa maendeleo, kijana anayewezana na kazi.*
*Ni mwana wa* ***Simba.***
*Mtu aelewaye maendeleo, vijana watapata kazi.*
*Kina mama wafanye biashara na kilimo.*

Aswani na wengine (2014) waeleza kwamba lugha haina uwezo wala mamlaka bali hupata uwezo huu kutokana na wanajamii wenye kumiliki uwezo katika jamii husika. Usemi au matini ni sehemu ya mapambano ya kubainisha tofauti katika itikadi, mamlaka na uwezo unaobainisha mvutano wa kiutawala baina ya jinsia ya kiume na ya kike. Maelezo haya yanashamiriwa katika wimbo ulioimbwa na Tapnyolei aliyekuwa akimtetea Kimutai ambaye alikuwa akiwania kiti cha ubunge wa Chepalungu mwaka wa 2017. Walieleza kwamba wang'arao ndio wale wanaomchagua yule mgombezi kwani wameshuhudia kazi aliyofanyia watu. Ameweza kuwasaidia wasiojiweza na angeleta maendeleo zaidi kama angechaguliwa. Wimbo umeusawiri uwezo wake wa kuongoza. Rejea sehemu ya wimbo nambari thelathini na tisa.

***39. INGOLUU CHE NG'OMEN***

*Ingoluu che ng'omen kou kakweng'et.*
*Ichek che imuti Kimutai parliament.*
*Kongoi vijana, chepyosok ak boisiek che ko kokochi ng'echerani Kimutai.*
*Ko konyolun ng'echeret.*
*Kakisabin echek asi indochi Lungu inyon en kalyet.*
*Neng'ung ng'echeret.*
*Ki keker boisieng'ng nebo NHIF.*
*Ki isoru che nyorotin.*
*Ko tiana yon imi ng'echeret, tiana boisionik che ko ibongonwech?*

***WENYE BUSARA WANG'AE***

*Wenye busara wang'ae kama mwangaza.*
*Wao wanaompeleka Kimutai bungeni.*
*Asante vijana, kina mama na wazee waliompatia Kimutai kiti hiki.*
*Kiti kimekufaa.*
*Tumekuunga mkono Kimutai halafu uongoze Lungu yetu kwa amani.*
*Kiti ni chako.*
*Tumeona kazi yako ya NHIF.*
*Umewaokoa walalahoi.*
*Na je, utakapokuwa kitini, ni mambo mangapi umetupangia?*

Levant na wenzake (2010) waeleza kwamba mambo yanapokuwa magumu, mwanaume anapaswa kuwa mgumu. Mwanaume sharti awe na uwezo wa kujipa maisha yenye mwelekeo ulimwenguni humu. Kuhusiana na ubabedume, Lombard (2003) anaeleza kwamba mwanaume mwenye udume, anapaswa kuwa mgumu, mwenye sifa ya urazini, hekima, mantiki, urijali na akili ikiwa hana nguvu za kimwili na misuli. Thibitisho lapatikana katika wimbo ulioimbwa na msanii aliyebobea katika muziki marehemu Kipchamba. Katika wimbo wake hakuna mahali ambapo jinsia ya kike ilisawirika. Msanii huyo aliimba wakati wa kampeni za kisiasa ya mwaka wa 2002 kuhusu wagombezi wawili wanaume, Kipkalya Kones na Nick Salat, waliokuwa wakigombea kiti cha ubunge katika Kaunti ya Bomet. Mgombezi wa chama cha KANU wakati huo alikuwa Salat na wa Ford People alikuwa marehemu Kones. Yule wa chama cha KANU alifanikiwa kwa kuchaguliwa na yule wa chama cha Ford People alifanikiwa kwa kuteuliwa. Kulingana na wimbo wa msanii huyo, wote wawili walikuwa wakikaribiana kwa nguvu kisiasa na wote walikuwa maarufu. Mada ya wimbo wake ilikuwa ‘Vyuma Vilishindana’. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini.

| ***40. KIIBELGE CHUMOINIK*** | ***VYUMA VILISHINDANA*** |
|---|---|
| *Kikasomangei* ***jumoinik.*** | ***Vyuma*** *vilikuwa vimeshindana.* |
| *Amo terektoge buch ketit komomi tigitik.* | *Na mti hauwezi kusimama bila mizizi.* |
| *Ki en kenyitab 2002, kobelge jumoinik en Bomet.* | *Katika mwaka wa 2002, vyuma vilishindana katika Bomet.* |
| *Jumoiyot en KANU, karnet en FORD PEOPLE.* | *Chuma kutoka chama cha KANU na kingine kutoka chama cha FORD PEOPLE.* |
| *Kobelike twan an Bomet Constituency komoitos parliament.* | *Vyuma hivyo viwili vikang’ang’ania bunge.* |
| *Kin kobelke jumonichoton, kosintan jumoiyot age age.* | *Vikishindana, chuma kimoja kikashinda, Kingine.* |
| *Kong’eten met ingo.* | *Kilichoshindwa, kikainua kichwa chake.* |
| *Ak koba twan parliament.* | *Na vyote viwili vikaingia bungeni.* |
| *Kongoi we Bomenyon,kotab murenik.* | *Asante Bomet yetu, nyumba ya wanaume.* |

| | |
| --- | --- |
| *Otech Bomet komeme, en kalyet ak chomnyet.* | *Mjenge Bomet yetu, imetemete kwa amani na upendo.* |

***4.2.2.7 Kampeni ya Kiti cha Ujumbe wa Wadi (MCA)***

Kimmel (1997) afahamisha kwamba nadharia ya Ubabedume hufafanua sifa mahususi anazostahili kuwa nazo mwanaume. Nadharia hii hujengeka mintarafu ya uwezo na mafanikio hasa ya mwanaume, uwezo ambao hufafanuliwa na kubainishwa kwa njia tofauti. Hii ni kipengele muhimu cha mtazamo wa nguvu za jinsia ya kiume. Wazo kama hili linathibitishwa katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Kachwes Rotich. Alimpigia debe mgombezi aitwaye Richard Cheselet aliyekuwa akiwania kiti cha Wadi ya Olol Masani. Alifafanua kwamba Cheselet awanie tena kiti hicho kwa maana kazi aliyofanya imeshuhudiwa. Ameunda barabara, amejenga shule na kuwasaidia wasiojiweza. Yeye hana ubaguzi wala ukabila na hawezi kukasirika hata akikasirishwa. Yeye huwa anawapenda watu wote. Msanii alimshauri aongoze watu wake namna Musa katika Biblia aliwafanyia Wayaudi. Uwezo na mafanikio ya mgombezi huyo wa jinsia ya kiume yalishamiriwa katika wimbo. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na moja.

***41. <u>OLOL MASANI</u>***

| | |
| --- | --- |
| *Olewen tugul Cheselet koik MCA kototen.* | *Nyote mchague Cheselet awe MCA mara nyingi.* |
| *Chi ne mie mugulel.* | *Ni mtu mwenye roho safi.* |
| *Motinye ubaguzi ako motinye ukabila.* | *Hana ubaguzi wala ukabila.* |
| *Barabarosiek ko miach, ng'alekab sukul ak 'bursaries.'* | *Amejenga barabara, shule na kuleta 'bursaries'.* |
| *Harambee, ko mokosoni.* | *Harambee, Cheselet hakosi.* |
| *Kikotok boisionik kong'eten 2013.* | *Kazi yake imeonekana tangu 2013.* |
| *Ingili ko monereche.* | *Hakasiriki hata akikasirishwa.* |
| *Chito ne ribe olon bo gaa.* | *Mtu anayelinda nyumbani.* |
| *Ne mingin ko chome, ne kakoyosit ko chome okot solomwet ko chome.* | *Anawapenda wadogo, wazee na hata walemavu.* |
| *Indochin bikuk kou Musa.* | *Waongoze watu wako kama Musa.* |

*Indochin komie.* *Waongoze kwa njia inayofaa.*

Ingawa nyimbo nyingi za kampeni za kisiasa zinasawiri nguvu na uwezo wa jinsia ya kiume, kuna nyingine zidhihirishazo sifa mahususi ya jinsia ya kike. Mfano ni wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Sogers Mekenyo. Msanii huyu alimtukuza mgombezi wa kike aitwaye Luisa aliyekuwa akigombea kiti cha ubunge wa wadi akitoka kaunti ndogo ya Segemian. Alimtetea akigombea tena kiti hicho 2017. Aliwashauri watu wampigie kura Luisa pekee kwani akishindana na wengine, yeye huwa mshindi. Alikuwa amelinda wadi hiyo na kuyaleta maendeleo mengi. Kupitia maendeleo hayo, watu wote walifaidika. Aliwafahamishia wapiga kura kuwa mama ni wa maana kwa familia yake na jamii kwa jumla. Hizi ni sifa mahususi zinazodhihirisha kwamba mwanamke ana uwezo wa kutawala akipewa nafasi na jamii. Wafula na Njogu (2007) waeleza kuhusu nadharia ya Ufeministi kwamba kimsingi, nadharia hii imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pingu ambazo zimejengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na mbili.

***42. <u>MCA LUISA FINAL</u>***

*Ongebirjin kura Luisa*
*kityo.*
*Kongoi chepset lug ak kobor.*
*Kongoi Luisa chemaluk*
*inyon.*
*Kongoi kamenyo* ***koaba tany***
*kot kekei.*
*Kongoi cherib gaa.*
*Kiritoret logokyok ikochi*
*'basari.'*
*Momi kit neu mama.*

*Tumpigie kura Luisa*
*pekee.*
*Asante aendaye vitani na kuwa mshindi.*
*Asante Luisa wetu ambaye maziwa yake*
*hayaishi.*
*Asante mama yetu* ***akamuaye***
***ng'ombe*** *mpaka maziwa yapatikane.*
*Asante mlinzi wa nyumbani.*
*Umewasaidia watoto wetu kwa kuwapatia*
*'bursary'.*
*Hakuna kinachofananishwa na mama.*

#### *4.2.2.8 Hitimisho*

Sehemu hii ilikuwa ikishughulikia mahusiano ya uwezo kijinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Ilisawirika kwamba jinsia ya kiume imepewa nguvu na uwezo mkubwa wa mamlaka. Nyimbo kadhaa ziliipa hadhi ya juu kuliko ya kike. Kulingana na nyimbo hizo, mwanamume anapaswa kuwa shujaa anayeweza kukabiliana na mambo mengi magumu katika jamii. Mwanaume thabiti ambaye anaweza kutawala, ni yule aliye jasiri.Anayeweza kumwua simba anayenguruma, anayeweza kukinga mipaka, asiyeshtuliwa kwa ngozi, asiyetingishika, awezaye kukimu familia yake na kuwalinda wasiokuwa na uwezo katika jamii kwa ujumla. Anahusishwa hususan na maneno yadhihirishayo ujasiri na nguvu za kimwili kama vile moto, simba, fahali, chuma, ngao, na mlima.

Nyimbo chache ziliitukuza jinsia ya kike. Mwanamke hakuhusishwa kwa ukamilifu na ujasiri, nguvu au uwezo wa kimwili. Msanii mmoja alieleza kwamba kina mama ni stima waletao mwangaza. Mwanamke alisifika kuwa mwenye uwezo wa kulisha jamii. Yeye ni mkarimu kwa maana huwa analeta maendeleo katika jamii. Yeye ni mwangaza ashughulikiaye usafi. Msanii mwingine alieleza kwamba marehemu Laboso alikuwa anaweza kuwa gavana na alipendezeka kwa sababu alikuwa na uwezo wa kunena yanayojenga na kuboresha mambo mengi katika Kaunti ya Bomet. Msanii mwingine alimtetea mgombezi wa kike aitwaye Luisa akieleza kwamba yeye ni mtunzaji wa nyumbani kwake na akienda vitani mwa siasa anakuwa mshindi. Vilevile, alitaja  kwamba hakuna mtu mzuri kama mama. Ni fika kwamba mama ana fadhila kama upendo, huruma, unyenyekevu, ukarimu na uaminifu.

### *4.2.3 Itikadi Kuhusu Jinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa*

#### *4.2.3.1 Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kiume*

Connell and Messerschmidt (2005:832) waeleza kwamba nadharia ya Ubabedume huhitaji wanaume kujihusisha nao na huhalalisha kiitikadi wanaume kuwatawala wanawake duniani. Deacon, Pinkering na wengine (1999) waeleza kwamba ni muhimu kutaja kuwa desturi za kijamii na mahusiano ya wanajamii huundwa kutokana na raghba ya mtazamo na dhana mahususi mintarafu ya uhalisi wa kijamii.

Marion Chelang'at ambaye alikuwa akitetea Muungano wa Jubilee, alijitahidi kuwashikamanisha watu ili wawe na umoja. Alielewa kwamba wanachama wa Muungano wa Jubilee wangepata wapiga kura wengi iwapo watu wangeungana kwani umoja ni nguvu. Muungano wa Jubilee uliundwa na wanaume wengi na wanawake wachache mno. Kulingana na wimbo huu, uchinjaji wa ng'ombe hufanywa na wanaume kuonyesha kwamba Muungano huo wa Jubilee ulitawaliwa na wanaume. Hili ni dhihirisho kwamba bado jinsia ya kiume ina uwezo mkubwa kisiasa kuliko ya kike katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na tatu.

***43. <u>JUBILEE OIYEE</u>***

| | |
|---|---|
| *Kokiyonjine kiy.* | *Tumeamua kubaliano la siri.* |
| *Kiyenye tany ak kepchei.* | *Tutachinja ng'ombe na tuigawe.* |
| *Kole alak moche chatit.* | *Wengine wanasema wanataka paja.* |
| *Kole alak moche chatit akichek.* | *Wengine wanataka paja pia.* |
| *Kyome tugul en konyon.* | *Tutakula sisi sote katika nyumba yetu.* |

Izugbara (2005) aeleza kwamba chimbuko la nadharia ya Ubabedume hufungamanishwa na dhakari na wenye kuimiliki, yaani, wanaume. Wanachukuliwa kuwa na nguvu na wa kuheshimika katika jamii. Siku zote mwenye dhakari hupewa hadhi ya juu na kuchukuliwa kuwa bora zaidi ya wale ambao hawana kiungo hiki, yaani, wanawake. Uhusiano baina ya mwanamke na mwanaume umejengwa katika mazingira yanayotukuza ukuu wa wanaume na udogo wa wanawake katika jamii.

Kupitia wimbo ulioimbwa na Jeremiah Kosgei, Samoei Ruto anaheshimiwa na jamii ya Wakalenjin kama kiongozi wao kwa kuitwa baba. Ruto alitumwa ampeleke Uhuru kutawazwa ili afanikiwe katika kinyang'anyiro cha kiti cha urais. Uhuru alifananishwa na Mfalme Daudi mwana wa Jesse katika Bibilia. Mfalme Daudi alikuwa mwenye nguvu kupindukia na aliheshimika sana kupitia matendo yake. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na nne.

***44 JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kokiyokten bamong'o Arap Ruto.* | *Tunakutuma baba yetu Arap Ruto.* |
| *Imutwech Uhuru konyo Kapkatet.* | *Utuleteee Uhuru aje Kapkatet.* |
| *Si kikochin mwaita nebo Kalenjin.* | *Ili tumtawaze kwa mafuta ya Kalenjin.* |
| *Kou weritab Jesse nemi Bible.* | *Kama mwana wa Jesse katika Biblia.* |

Aswani na wengine (2014) waeleza kuwa uwezo, itikadi, majukumu na mamlaka ni masuala yanayobainisha mahusiana na utofauti na hasa zaidi athari ya tofauti hizi katika mfumo wa jamii. Wimbo ulioimbwa na Jeremiah Kosgei, unaeleza kwamba Ruto ni shujaa awezaye kumwua simba anayenguruma na hakuna adui anayemweza. Yeyote aliye mamlakani, anapaswa kuwa shujaa na mwenye uwezo mkubwa wa kumwezesha kuongoza kulingana na sehemu hii ya wimbo nambari arubaini na tano.

***45. JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kongoi nyiganet.* | *Asante shujaa.* |
| *Bar ng'etuny korose.* | *Amwuaye simba anayenguruma.* |
| *Kogerin bunyon koimen.* | *Adui akikuona kunakuwa giza.* |
| *Iger inye kolaba.* | *Ukimwona kunakuwa mwangaza.* |

Kosgei alimhimiza Ruto arudishe utawala kwa jamii ya Kalenjin wakati Uhuru atakapohitimisha kipindi chake cha utawala. Tendo hili linaonyesha jinsi jinsia ya kiume inasawirika kuwa na mamlaka. Hii ni itikadi inayoleta udumishaji wa ubabedume katika jamii. Fairclough (1989) anabainisha mikakati maalumu ya uchanganuzi wa lugha mintarafu ya mahusiano na uwezo, itikadi na mabadiliko ya jamii na utamaduni. Anaeleza kwamba kutokana na urudiaji usioepukika katika utamaduni mzima, itikadi mwishowe hufanywa kuonekana kuwa suala la kiasili na ina nafasi yake maalumu katika mchakato mzima wa kujenga ubabedume. Usemi au matini ni sehemu ya mapambano ya kubainisha tofauti katika itikadi, mamlaka na uwezo unaobainisha mvutano wa kiutawala baina ya jinsia ya kiume na ya kike. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na sita.

***46. JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Wegun tuga ak irib en kaptich.* | *Warudishe ng'ombe na uwachunge zizini.* |
| *Bokokyin Uhuru kotwoisiok.* | *Umwachie Uhuru atimize.* |
| *Si ngemi tai kotililit sumenyon.* | *Halafu tuwe na muungano mwema mbeleni.* |

Macleunness (1998) afafanua kwamba udume hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanaume bali hutokana na itikadi na utamaduni wa jamii husika. Masharti mahususi ya kihistoria yanayothibiti imani za mume na mke katika jamii na majukumu yao tofauti huendelezwa kupitia kwa imani za jamii, matarajio na mielekeo yao. Ruto kama mwanaume, anashauriwa na Kosgei kwamba hekima ni uwezo. Alimwarifu kuwa yeye ni baba ya Wakalenjin, ndume ambaye amewekwa pembeni. Maelezo haya yanabainika katika sehemu hii ya wimbo nambari arubaini na saba.

***47. JUBILEE***

| | |
|---|---|
| *Kimnotet naet we Samoei.* | *Samoei akili ni mali.* |
| *Kongoi kirginyon.* | *Asante ndume yetu.* |
| *Kongoi kipwalei kipken bun.* | *Asante mweza adui.* |
| *Kitienge en tobonik we babanyon.* | *Baba yetu tunakutegemea pembeni.* |
| *Kikamwa boiyon kiba kel belyon.* | *Mhenga alisema kutakuwa na fanaka.* |
| ***Kibendi mochei keldo.*** | ***Pole pole ndio mwendo**.* |

Vilevile, Shuttle Sisters ni wasanii ambao walidhihirisha maelezo tuliyopewa na Maclenness katika wimbo wao. Walifafanua kwamba Samoei ni mwanaume anayetambulika katika nchi nzima ya Kenya kwa kuwa na nguvu ya kutawala akipata nafasi. Aliombewa na wasanii kuwa rais wa nchi ya Kenya wakati mmoja. Walimhimiza afuate nyayo za Mstaafu Rais Moi kutoka jamii ya Wakalenjin aliyetawala nchi ya Kenya kwa miaka kadhaa. Wimbo huu unashamiri ujengaji wa ubabedume katika jamii ya Wakalenjin. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na nane.

***48. URP***

| | |
|---|---|
| *Mami bororiet Kenya ne moingen* | *Hakuna jamii nchini Kenya isiyolitambua* |
| *kainetab Samoei.* | *jina la Samoei.* |
| *Kisaun kot indochi emenyon* | *Tunakuombea hadi uongoze nchi yetu ya* |
| *Kenya.* | *Kenya.* |
| *Ye indochi emenyon, ibur* | *Utakapo ongoza nchi yetu ukae* |
| *kou Baba Moi.* | *kama Baba Moi.* |

Marion Chelang'at alikuwa na wazo kama hili katika wimbo wake. Alieleza kwamba wanaye mwanaume ambaye ni kifungua mimba anayewaunga wengine mkono siasani ili hata yeye aungwe mkono siku za usoni. Wenyeji wanamwita fahali ainuaye mlima na ni yule akinena, husikilizwa. Jamii ya Wakalenjin hutarajia mwanaume kuwa na nguvu ya kipekee ya kutawala na anapewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na tisa.

***49. JUBILEE OIYE***

| | |
|---|---|
| *Kitindoi taitanyon.* | *Tunaye kifungua mimba wetu.* |
| *Kole robe morik,* | *Alisema anaungana mkono,* |
| *si tun ketilji.* | *kusudi aungwe mkono baadaye.* |
| *Kole neranik,, chepyosok koboto* | *Vijana, kina mama na wazee walisema,* |
| *boisiek, i kirginyon kipkeleny tulwo.* | *wewe ni fahali yetu ainuaye mlima.* |
| *Kirginyon ne ingosil* | *Fahali yetu ambaye akilia hutegewa* |
| *ke yepchin it.* | *masikio.* |

Fiske (1987) anaangaza masimulizi ya matukio hatari, ushari wa vitendo na mashindano sambamba na wanasesere wa kiume. Utamaduni na mazingira huwa vigezo muhimu katika kukuza ubabedume ambao hukolea katika fahamu za wanajamii. Ubabedume unadhihirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Kipkurui Ng'eny. Alimhimiza Ruto asimame imara katika siasa na awe kiongozi wa jamii ya Wakalenjin. Awachunge wanaoteseka na awe baba ya mayatima. Kulingana na itikadi na utamaduni ya Wakalenjin, jinsia ya kiume huhusishwa na mambo makuu na huonekana kama mweza yote. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini.

***50. KONGOI ARAP RUTO NYIGANETAB KALENJIN***

*Telel Arap Ruto nyiganetab Kalenjin.*
*Ribwech che seretos.*
*Ribwech che motindo sigik.*
*Iweiigu babanyuan.*
*Indochin bikab Kalenjin.*

***ASANTE ARAP RUTO SHUJAA WA KALENJIN***

*Simama imara shujaa wetu wa Kalenjin.*
*Utuchungie wanaoteseka.*
*Utuchungie mayatima.*
*Uwe baba yao.*
*Uwaongoze jamii ya Wakalenjin.*

Carrigan na wengine (1985) wafahamisha kwamba Patricia Sexton alitufafanulia kwamba kanuni za jinsia ya kiume zinasisitiza sifa kama vile ujasiri, mwelekeo wa kibinafsi, ubingwa, ustadi wa kiufundi na ugumu katika akili na mwili. Wazo kama hili linasawirika katika wimbo wa msanii aitwaye Ras Wageni. Alikuwa akimwunga mkono Isaac Ruto aliyegombea kiti cha ugavana mara ya pili katika Kaunti ya Bomet. Kupitia wimbo wa Ras, wenyeji walifurahia Isaac Ruto, fahali yao aliye jasiri, ambaye alikiunda chama cha Mashinani. Walimpongeza kwa kuungana na wananchi wa Kenya na kuwatetea watu wa Mau katika tatizo la shamba hadi wakapata haki yao kwani yeye hawezi kushtuliwa na chochote. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na moja.

***51. CHAMA CHA MASHINANI***

*Kisime echek en chamaitab*
*Mashinani.*
*Kongoi kirginyon.*
*Ingosil koitu tuguk gaa.*
*Kiiyan otononse ak bikab*
*Kenya komugul.*
*Kongoi nyiganenyon Isaac Ruto.*
*Kin itweku konyorchige imanda bikab Mau.*
*Magimuenen magatet.*

*Tunashabikia chama chetu cha*
*Mashinani.*
*Asante fahali yetu.*
*Akilia, mali yanafika nyumbani.*
*Umekubali kusimama na watu wote wa*
*Kenya.*
*Asante shujaa wetu Isaac Ruto.*
*Uliponena, watu wa Mau walipata haki yao.*
*Hushtuliwi kwa ngozi.*

Connell (1987) afafanua kwamba ubabedume, wazo la kimsingi katika maandishi ya Gramsci na mchango mkubwa wa mawazo ya Umaksi, ni kuhusu ushindi na umilikaji wa mamlaka na uundaji (na uharibifu) wa vikundi vya kijamii katika mchakato huo. Ni hasa kuhusu namna ambavyo tabaka la utawala huanzisha na kudumisha utawala huo. Ubabedume huhusu ushawishi wa idadi kubwa ya watu hasa kupitia vyombo vya habari na shirika la taasisi ya kijamii kwa njia zinazoonekana kuwa "kawaida". Ras ni Mwimbaji ambaye alimtaja Isaac Ruto kuwa baba yao aliyeunda chama cha Mashinani ambacho kimeunganisha jamii ya Wakalenjin. Alieleza kwamba tangu Ruto awe gavana wa Kaunti ya Bomet 2013, kazi kubwa ambayo amewafanyia wenyeji imetambulika. Msanii aliwashawishi wenyeji wampigie tena kura 2017 kwani si ungwana kujikinga chini ya mti kukinyesha halafu mvua iishapo, uukate mti huo. Kuna mambo matatu yaliyodhihirika katika wimbo huu kama yafuatayo: Uundaji wa utawala, udumishaji wa utawala huo na ujengaji wa ubabedume katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na mbili.

***52. <u>CHAMA CHA MASHINANI</u>***

| | |
|---|---|
| *Kongoi en chamainyon.* | *Tunashukuru kwa chama chetu.* |
| *Kongoi babanyon.* | *Tunakushukuru baba yetu.* |
| ***Mokiyumen sosur ye moen keyeb.*** | ***Haifai kujikinga chini ya mti kukinyesha, halafu mvua ikiisha uukate.*** |
| *Kikotok boisionik tugul chebo kandoindenyon Isaac Ruto.* | *Kazi yote ambayo Isaac Ruto ameifanya, imeonekana.* |
| *Koiyumenech bik tugul chebo Kalenjin chamainyin nebo CCM.* | *Kalenjin wote wameunganishwa katika chama chake cha CCM.* |

Waimbaji waliojiita Chama Cha Mashinani (CCM) Women walionyesha maelezo tuliyopewa na Connell. Walifahamisha kwamba Ruto ni shujaa mfano wa moto ambaye ameimarisha maendeleo katika Kaunti ya Bomet hadi ikagundulika kote nchini Kenya. Amewahi kuwa mwenyekiti wa magavana wote nchini Kenya akiwa na umri mdogo. Yeye hana mapendeleo na ameweza kuongoza kaunti yake ipasavyo. Walieleza kuwa malumbano ya kisiasa yanahitaji walio na ujasiri mwingi kama yeye. Waliwasihi wenyeji wamchague yeye tena kuwa gavana

kwani ni mwanaume anayestahili kuwa kiongozi. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na tatu.

| ***53. GAVANA KO ISAAC ARAP RUTO*** | ***GAVANA NI ISAAC ARAP RUTO*** |
|---|---|
| *Kiribwech kounti Arap Ruto.* | *Arap Ruto ametulindia Kaunti.* |
| *Kot kegas en Kenya.* | *Ikasikiga nchini Kenya.* |
| *Kigoik chairman Arap Ruto* | *Amewahi kuwa mwenyekiti akiwa na* |
| *en 47.* | *Miaka 47.* |
| *Boiboyet ne tiana yon kiketyi* | *Ni furaha iliyoje Arap Ruto akirudishwa* |
| *kora Arap Ruto?* | *tena?* |
| *Motinye kolotunet Arap Ruto.* | *Arap Ruto hana mapendeleo.* |
| *Ngokerin bunyon koimen,* | *Adui akikuona kunakuwa giza,* |
| *iger kolaba.* | *ukimwona kunakuwa na mwangaza* |
| *Nyoljin kandoinatet.* | *Unastahili kuwa kiongozi.* |
| *Kongoi we Kipkutuny si koet Bomenyon.* | *Asante Kipkutuny apate kulinda Bomet.* |
| *Kimoitos ra tugul ne moche* | *Uongozi huu unang'ang'aniwa na wengi na* |
| *nyigonik.* | *unahitaji mashujaa.* |
| *Kongoi we nyiganet neu mat.* | *Asante shujaa kama* ***moto.*** |

Connell (1983): 236, 255 ,256 anaeleza kuhusu makundi yanayohusika zaidi na uundaji wa itikadi za kijinsia. Ni kweli kwamba makundi haya na udikteta wao husababisha kwa kishindo ugomvi, utawala na miundo ya kikatili ya taasubi za kiume. Kwa ujumla, wale wanaohusika zaidi inaaminika kuwa ni: mapadri, waandishi wa habari, watangazaji, wanasiasa, wanasaikolijia, watengenezaji wa filamu, waigizaji, waandishi wa riwaya, makocha wa michezo na wasomi. Watu hawa wanaendeleza utawala wa kijinsia, tajriba zifaazo, mitazamo; kutafakari na kufasiri mahusiano ya kijinsia. Itikadi za jinsia ya kiume zinadhihirika katika wimbo ulioimbwa na Chama Cha Mashinani (CCM) Women. Walimtaja Ruto kama fahali, shujaa kama moto, kiongozi, mwelekezi, mwenye roho safi, mnenaji, baba yao na mfanyikazi maarufu nchini Kenya. Maelezo hayo yote kupitia wimbo wao, waliwasihi wenyeji kuwa Ruto angebaki kuwa

gavana wao tena. Wimbo huu umedhihirisha kwamba waimbaji wa jinsia ya kike huunda utawala wa taasubi za kiume katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na nne.

| ***54. <u>GAVANA KO ISAAC RUTO</u>*** | ***<u>GAVANA NI ISAAC RUTO</u>*** |
|---|---|
| *Kongoi kirginyon.* | *Asante fahali yetu.* |
| *Mokichomndoi kesilwech.* | *Haturuhusu aumizwe.* |
| *Kichome nyiganet neu* ***mat.*** | *Twampenda shujaa mfano wa* ***moto.*** |
| *Kongoi Kimurany ne motinye kolotunet.* | *Asante Kimurany asiye na mapendeleo.* |
| *Kichome Koterkut.* | *Twapenda Koterkut.* |
| *Kikotok boisienyin.* | *Kazi yake imeonekana* |
| *Kongoi babanyon ne kikenai* | *Asante baba yetu aliyejulikana nchini* |
| *en Kenya.* | *Kenya.* |
| *Mokiwole kora.* | *Haibadilishwi tena.* |
| *Ne kikondochi gavanaek.* | *Aliyewaongoza magavana.* |

Sattel (1983:119-124) anahisi kwamba chanzo cha kuelewa ubabedume huhusika na utawala wa hadhi ya juu ya kiume katika jamii. Upendeleo wa jinsia ya kiume na ukuu wao kwa wanawake, kuambatana na uchunguzi wa Sattel, inaendelezwa katika jamii nyingi za Nijeria. Tofauti ya kijinsia katika tamaduni za jamii za Nijeria, huruhusu uwezo na hadhi ya juu kuliko wanawake. Wanaume ni wafalme na viongozi wanaongoza katika kila jambo hata kama maamuzi yao haifaidi jamii. Mawazo haya yanasawirika katika wimbo wa msanii aliyejiita Hotstar Kutundetunde aliyekuwa akimwunga mkono Isaac Ruto. Mwimbaji alifafanua kwamba Ruto ambaye ni jasiri na anawapenda watu wote, atabaki kuwa gavana tena kwani yeye ni mashuhuri. Alieleza kuwa wenyeji wote wamemwunga mkono awe gavana yao tena. Wazee wa kiume ambao wameeleza kwamba wamefaidika kutokana na uongozi wa Ruto, wamembariki yeye apate kuongoza kaunti ipasavyo kama Musa katika Biblia. Musa alipogonga maji kwa fimbo aliyokuwa nayo, maji yakatawanyika na Wayaudi wakavuka. Wazee walimshauri mgombezi pamoja na wenyeji wawe watu wenye busara wasiotaka vita ili wafaulu katika kaunti yao. Kulingana na maelezo ya wimbo huu, ubabedume unaendelezwa katika jamii ya Wakalenjin. Wanaume wanaamua karibu kila kitu kwani ndio wao wanatoa mawaidha yote. Wao hasa

waliamua kwamba hawataki gavana mwingine ndipo walimsifu na kumbariki mgombezi. Walieleza namna wamenufaika na kushauri wenyeji kuepukana na vita. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na tano.

***55. <u>MASHINANI-NASA</u>***

| | |
|---|---|
| *Mokiwole Isaac Ruto.* | *Isaac Ruto habadilishwi.* |
| *Kisimchini nyiganenyon.* | *Tunashabikia shujaa wetu.* |
| *Mwoe boisiek, chepyosok ak vjana mokiwole.* | *Wazee,kina mama na vijana wanasema haibadilishwi* |
| *Mie mugulel.* | *Ana roho safi.* |
| *Ki kokonin kirokto boisiek neu nikibo Musa si kelanda.* | *Wazee wamekupatia fimbo kama ile ya Musa ili tuvuke.* |
| *Okot ne iwerto en oret kongenin.* | *Hata mpitanjia anakutambua.* |
| *Keikun bik che utoten, che mobo boriot.* | *Tuwe watu wenye busara, wasio wa vita.* |
| *Okot echek boisiek kemi komie.* | *Hata sisi wazee tuko salama.* |

Carrigan, Connell na Lee (1985) waeleza kwamba ubabe-dume ni suala la jinsi makundi fulani ya wanaume humiliki mamlaka na utajiri na namna wanahalalisha na kuendeleza utawala wao. Kutokana na ubabedume, wanaume wengi hufaidika kwa kuwatawala wanawake. Kwa wanaume wengine, huwawezesha kutawala wanaume wenzao. Maelezo haya yanasawirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Arumutik Kosgei.

Alimtetea Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet. Lesan alikuwa amechaguliwa kuwa seneta kuanzia 2013. Alikuwa akigombea kiti hicho mara ya pili. Msanii alifahamisha kuwa kaunti yao inahitaji mtaalamu ambaye angeiimarisha. Lesan alikuwa amebarikiwa na wazee wa kiume kuwa seneta na alitarajiwa kukitumia kiti hicho ipasavyo ili wanaume wengine chipukizi waje wakitumie siku za usoni. Mwimbaji alimshaua Lesan kwa kueleza kwamba yeye ni shujaa ambaye ni ngao na macho ya wenyeji. Yeye hawezi kutishwa wala kutingishika na taa yake inawaka usiku na mchana. Mgombezi alitajika kuwa jasiri wa kukinga pembeni. Alihimizwa na msanii awatatulie wenyeji matatizo kama vile Yusufu na Musa

waliwalisha Wayaudi jinsi ilivyoelezwa katika Biblia. Mwimbaji aliwaelezea wenyeji kuwa maelewano, amani na urafiki ni  muhimu na kwamba jamii ya Wakalenjin huongozwa na ngao na amri za mababu zetu tangu enzi. Jambo hili likitimizika, wanaume wengine watawaheshimu. Kupitia maelezo ya wimbo huu, mambo yote yamepangwa na jinsia ya kiume kwani imepewa hadhi ya juu na uwezo wa kutawala. Jinsia ya kike ilifichika katika wimbo huu kuonyesha kwamba jamii imeipa hadhi ya chini na imeshamirika kutokuwa na uwezo wa kutoa uamuzi. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na sita.

***56. <u>PROFESA WILLIAM LESAN</u>***

| | |
|---|---|
| *Asi ketech Bomet Kounti bo kolili komoche chito ne somanat.* | *Ili tujenge Bomet Kaunti hadi imetemete tunahitaji mtaalamu.* |
| *Somananing'ung profesa ko **sobunitab** Bomet Kounti.* | *Profesa masomo yako ni **sabuni** ya Kaunti ya Bomet.* |
| *Kokokonin boisiek ng'ulek.* | *Wazee wamekupatia mate.* |
| *Si koribwech kisienyon bo kok si nyo kwomisien murenjun mengech.* | *Apate kutulindia sahani yetu ya wazee ili wanaume wale wengine wadogo wailie.* |
| ***Taing'ung** ne lole bet ak kemo.* | ***Taa** yako inawaka usiku na mchana.* |
| *Profesa Lesan ko nyiganet ne kokikere sermosiek.* | *Profesa Lesan ni shujaa wetu ambaye tumemweka  pembeni.* |
| *Ma kitisionin en ta yun.* | *Huwezi ukatishwa hata kidogo siku za usoni.* |
| *Seneta nenyon ko moitumtumokse matiny.* | *Seneta wetu hawezi kutingishika kamwe.* |
| *Asi isoru bik en rubet kou Joseph en Egypt.* | *Waokoe walio na njaa kama Yusuf kule Misri.* |
| *Digrii ing'ung ne itindoi ko kerge ak kiroki kibo Musa.* | *Digrii uliyo nayo ni sawa na ile fimbo Musa alikuwa nayo.* |
| *Si kotekisech murenchun.* | *Ndipo wanaume wale wengine watatuheshimu.* |
| *Lesan ko **long'enyon** ne mi tai asi koik **konyek.*** | *Lesan ni **ngao** yetu aliye mbele yetu ili awe **macho** yetu.* |

| | |
|---|---|
| *Borienyon ak oret indochin ng'atutik kosibike ak **long'et.*** | *Kabila letu na ukoo huongozwa na amri zikifuatana na **ngao.*** |
| *Kalyet en tai murenchu.* | *Tuweke amani mbele nyinyi wanaume.* |
| *Kirgit choruandit ng'otut en boisiek.* | *Urafiki ni fahali na ni amri ya wazee wetu.* |
| *Kirgit kosyinet kong'eten kuko ak baba.* | *Maelewano ni fahali tangu enzi zile za mababu zetu.* |

Whitehead (2003):4 aeleza kwamba suala la ubabedume hutegemea jamii husika. Ubabedume ni jinsi jamii yoyote huamini sifa zinazohusika na jinsia ya kiume na tabia za uume. Uume huhusu mazoea na njia zinazotumika kuthibitisha uume katika mwanaume au mvulana. Rangi, tamaduni, dini, mifumo ya imani, hali halisi ya mazingira na tajriba za kihistoria huchangia katika kuendeleza taasubi za kiume duniani hususan barani Afrika. Mawazo ya Whitehead yanalandana na maneno yapatikanayo katika wimbo ulioimbwa na Arumutik Kosgei. Msanii huyo alimtetea Profesa Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet 2017. Rejea sehemu ya wimbo namba hamsini na sita.

Uchendu (1965) anatuarifu kuhusu maandishi ya Mouiche. Mouiche anatueleza jinsi bara la Afrika linaendeleza ubabe-dume na kusababisha ubaguzi wa kijinsia. Mageuzi ya hali ya kisiasa ya Waafrika na haki husika kimsingi, yalihamasishwa na ukoloni ambapo uliacha bara la Afrika na ubabedume uliokithiri. Mouiche alidhihirisha namna utawala wa kikoloni uliokuwa mkali, ulisababisha kuenea kwa ubabedume wa kisiasa baada ya ukoloni. Wakati wa utawala wa kikoloni, wanajeshi na hata wafanyikazi wengine walikuwa wa jinsia ya kiume. Kulingana na namna tumeelezewa na Uchendu juu ya ubabedume, hebu rejea wimbo ufuatao unaohusika na maelezo haya. Wimbo wenyewe uliimbwa na msanii aitwaye Titus Kosgei kuhusu Nathan Kirui aliyegombea kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki. Katika wimbo huu, msanii alimwachia mgombezi kunena maneno machache kabla ya wimbo kuanza. Mgombezi alikuwa mwanaume na alinena kwamba kuingia kwake siasani, kulikuwa mwito wa kipekee. Yeye kama mwanaume, alifafanua mwenyewe kwamba alikuwa na imani na tumaini kubwa kuwa angepata kiti cha ubunge. Ndoto yake ilimwelekeza kwamba angefanya kazi pamoja na wenyeji na angewasikiza, angewasemea na kuwatendea. Msanii naye alimwinua Kirui akihamasisha wenyeji wamchague mwanaume chipukizi aliye shujaa na mwenye nguvu anayeweza kazi. Alifananisha mgombezi huyo na simba kuonyesha ujasiri, nguvu, msimamo na uwezo wake kama kiongozi kwa kutaja

kwamba ni mwana wa Simba. Wimbo huu unausawiri uenezaji wa ubabedume, utawala wa jinsia uliokithiri katika jamii ya Wakalenjin. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na saba.

| ***57. <u>NATHAN KIRUI KITYO</u>*** | ***<u>NATHAN KIRUI PEKEE</u>*** |
|---|---|
| *Inoni ko kurset ne inegen.* | *Huu ni mwito wa kipekee.* |
| *Otinye kayanet en muguleldanyun.* | *Ninayo imani rohoni mwangu.* |
| *Otinye komong'unet.* | *Ninalo tumaini.* |
| *Inoni ko korwotitet ne inegen.* | *Hii ni ndoto ya kipekee.* |
| *Otinye maketab keboisien tugul kibagenge.* | *Nataka tufanye kazi pamoja.* |
| *Okoswok, omwoitewok ak oyoiwok.* | *Nawasikiza, nawasemea na kuwatendea* |
| *Kikochin ra chito nyiganet neto koming'in Nathan Kirui.* | *Tutampatia wakati huu mtu mpya, shujaa wetu aliye chipukizi Nathan Kirui.* |
| *Chitab bandab tai, kijanayat ne nomeke ak kasit.* | *Ni mtu wa maendeleo, kijana chipukizi anayewezana na kazi.* |
| *Arwetab Simba, ki Simba kwanda.* | *Ni mwana wa Simba,baba yake alikuwa anaitwa Simba.* |

Uchendu (2005) alifahamisha kuwa kwa ujumla, kulingana na vijana wa Nijeria, wanaume au wavulana huhusishwa na sifa fulani za kimwili, za kibiolojia na kisaikolojia kando na sifa za utu. Ifuatayo ni mifano ya sifa hizo: nguvu za kimwili, udhabiti, ujasiri, mwenye maamuzi, mwenye uwezo wa kulinda wanyonge, mwenye msimamo, mwenye uwezo wa kudhibiti, na anayeweza kuongoza. Mengi ya maelezo haya huonekana katika wimbo unaofuata ambao uliimbwa na msanii aitwaye Daniel Cheres. Alieleza wazi kwamba nchini Kenya tunao viongozi wapendanao wasioweza kutenganishwa hata kama siasa imechacha. Alikuwa akiwalenga Uhuru na Ruto kwa kufafanua kuwa Uhuru ni kama mti ulionawiri ambao umemea kando ya mto. Ruto ni tawi moja la mti huo na anatarajiwa ashike usukani Uhuru amalizapo kipindi chake cha utawala. Aliwashawishi wenyeji wautunze mti ipasavyo ili uendelee kustawi. Ruto aliyetajwa kama shujaa alishauriwa awalishe walio na njaa, watibiwe walioumizwa na wasiojiweza wasaidiwe. Kuungana pamoja kwa wanasiasa hawa wawili kunaonyesha ubabedume uliokithiri, tabaka ya

utawala, msimamo na ujasiri wao kisiasa. Maana ya kupalilia mti ni namna wananchi walivyowaunga mkono wanasiasa hao wapate kuwa na nguvu thabiti na uwezo wa kuongoza nchi. Ruto alitarajiwa kuwalinda wanyonge kusawiri uwezo wake kama mwanaume aliye kiongozi. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na nane.

***58. <u>JUBILEE</u>***

| | |
|---|---|
| *Kitinye kondoik che makibestos.* | *Tunao viongozi wasiotenganishwa.* |
| *Chame kalyet matiny komi bolet.* | *Wanapenda amani hata kama kuna siasa.* |
| *Orogendoen **ketit** ne mi tabandab oinet.* | *Nafananisha na **mti** ulio kando ya mto.* |
| *Ketit ne tinye temet neboe emet.* | *Mti ulio na tawi linalolisha nchi.* |
| *Temet ne tinye kimnatet, temoni ko nenyon Kalenjin.* | *Tawi lililo na nguvu, tawi hili ni letu Wakalenjin.* |
| *Ongikutyin ng'ung'unyat temoni si ye kayosit keti ketinye ne nome boisiet.* | *Tupalilie mti huu, halafu ukizeeka tutakuwa na wa kushika usukani.* |
| *Kiboe che ome rubet.* | *Walio na njaa walishwe.* |
| *Kityoche che kigirat.* | *Waliofungwa wafunguliwe.* |
| *Kisobe che kikikoten.* | *Watibiwe walioumizwa.* |
| *Nyoru kiy che motinye kiy.* | *Wasio na chochote watapata.* |
| *Osome toretet koyobun nyiganetab Kalenjin.* | *Naomba usaidizi kutoka wewe shujaa wa Kalenjin.* |

Mawazo makuu tuliyopewa na Uchendu, vilevile, hudhihirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Arumutik Kosgei aliyemtetea Shadrack Koech. Koech alikuwa akigombea kiti cha Ujumbe wa Wadi ya Obosi katika Kaunti Ndogo ya Ndanai 2017. Mgombezi huyo alikuwa akigombea kiti hicho kwa mara ya pili. Mwimbaji alimsifu akieleza kwamba yeye ni msomi na amepokelewa na wenyeji kuwa mjumbe wao wa Wadi. Alibarikiwa na wazee, vijana na kina mama. Walimfurahia kwa sababu hakukata tamaa aliposhindwa katika uchaguzi wa 2013. Mgombezi aliamua kuwa wadi hiyo ingeinuka kwani angeleta mabadiliko. Mgombezi alionyesha msimamo, ujasiri na nguvu zake kisiasa alipoamua agombee kiti hicho upya. Alisawiri uwezo wake na uamuzi aliponena kuwa angeleta mabadiliko katika wadi. Wenyeji walipompokea

mwanaume huyo kugombea kiti hicho, inadhihirisha jinsi jamii huunga mkono na kuuendeleza ubabedume uliokithiri. Rejea sehemu ya wimbo nambari hamsini na tisa.

***59. <u>SHADRACK KOECH FOR MCA NDANAI</u>***

| | |
|---|---|
| *Kisoman koyam somanet.* | *Alisoma ya kutosha.* |
| *Kotoroch kokwenyin.* | *Kijiji chake kimemlaki.* |
| *Iguitos tabusiek tugul chebo kasisiek.* | *Anaelewa kazi atakazofanya.* |
| *Kirinemuge kong'eten 2012.* | *Uligombea tangu 2012.* |
| *Kiimwa ile king'ete.* | *Ulisema tutainuka.* |
| *Ki kituiye vijana, boisiek ak chepyosok ak kekonin ng'ulek.* | *Tulikutana tukiwemo vijana, wazee na kina mama na kukubariki.* |
| *Imache iibu walet.* | *Unataka kuleta mabadiliko.* |

#### *4.2.3.2 Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kike*

Hochschild (1989):257 aeleza kwamba wakati huu, hali ya uchumi imebadilika. Kuna kupunguka kwa uwezo wa kifedha hususan mshahara wa jinsia ya kiume, kupunguka kwa idadi ya kazi za wanaume zinazohitaji ustadi na zile zisizohitaji na kuongezeka kwa kazi za jinsia ya kike katika kanda za huduma. Wazo hili la Hochschild liko katika wimbo ulioimbwa na mwimbaji aitwaye Ben Bii. Alikuwa mtetezi wa marehemu Dkt. Laboso aliyekuwa akiwania kiti cha ugavana katika Kaunti ya Bomet na Beatrice Kones aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki 2017. Katika wimbo wake anatufafanulia kwamba mambo ya kisiasa yanaenda kubadilika. Watu wa Bomet wameamua kubadilisha gavana na mbunge wa Bomet Mashariki wawe wa jinsia ya kike. Alieleza kuwa jambo hili ni la busara na yule asiyetaka kubadilika, dunia itambadilisha. Tendo kama hili litaleta ongezeko la kazi za jinsia ya kike kwenye kanda za huduma na kupunguza nguvu za ubabedume uliokithiri katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari tano.

Wimbo ulioimbwa na Marion Chelang'at, unadhihirisha maelezo tuliyopewa na Hochschild. Mwimbaji huyo alikuwa akimtetea marehemu Laboso. Alifafanua kwamba watu walikuwa wanahitaji Laboso kuwa gavana kwani walitaka mabadiliko. Alieleza kuwa si lazima mwanaume

atawale. Wanawake wapewe nafasi kisiasa na katika asasi nyingine za kijamii. Rejea sehemu ya wimbo nambari nane.

Utawala wa wanawake kabla ya ukoloni kule Yorubaland, Hausaland na Igalaland ulileta changamoto kubwa kwa ubabedume katika jamii hizo. Walakini, kwa kurejelea Edoland, Shokpeka (2002:111) anaamini kwamba kufanikiwa kwa utawala wa malkia wawili katika ufalme wa Benin, kabla ya ukoloni, kulitokana na mafanikio yao ya kiuchumi na utajiri wao. Baada ya utawala wao, uongozi wa kiume katika ufalme huo, uliondoa utawala wa wanawake. Waliamini kwamba kulingana na mila zao, 'wanawake hawakutambulika wakiwa wa hadhi ya juu katika jamii'. Wimbo unaofuata uliimbwa na Rodgers Mekenyo ambaye alitetea nguvu za mwanamke mgombezi aitwaye Luisa aliyegombea kiti cha Ujumbe wa Wadi 2013 na 2017. Msanii alieleza kuwa Luisa ana ujasiri, msimamo na uwezo wa kuongoza kwani akiingia siasani, anakuwa mshindi namna alivyofanya katika kinyang'anyiro cha 2013. Alimwinua akieleza kwamba alilinda wadi yake ipasavyo kwa kustawisha maendeleo. Aliwashauri wenyeji wampigie kura tena kwa vile hakuna kitu cha kufananishwa na mama. Rejea sehemu ya wimbo nambari arubaini na mbili.

#### *4.2.3.3 Hitimisho*

Hii ni sehemu iliyoshughulikia suala la itikadi kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Nyimbo kadha wa kadha ziliwatafutia wagombezi wapigaji kura kwa wingi. Wasanii walioimba nyimbo hizo waliwapigia debe wagombezi hao pamoja na vyama vyao wakitumia lugha ya kuvutia iliyoandamana na sauti zao pamoja na ala zao za muziki. Waliwaunganisha watu ili wafuate mkondo mmoja kisiasa na kuweko na upigaji wa kura ulio shwari. Miongoni mwa wasanii hao, kulikuwa na wale waliowachochea wagombezi wengine. Waliodhihakiwa hususan walikuwa wa jinsia ya kiume.

Kuambatana na nyimbo hizo, wagombezi wa kiume walipewa uwezo, hadhi ya juu na mamlaka hasa kulingana na nguvu zao za kimwili. Wasanii walieleza kwamba wao ni ngao walio na msimamo na wanategemewa pembeni. Walieleza kwamba mwanaume anapaswa kuwa shujaa kama moto asiyeshtuliwa kwa ngozi. Yeye ni mwenye nguvu kwani anaweza kuinua mlima na

hawezi kutingishika. Yeye amefananishwa na fahali na chuma. Anastahili kuwa kiongozi na mchungaji, yaani, macho au taa ya watu wengine. Wasanii waliwasifu wagombezi wa kiume kwa njia tofauti na wa kike. Mwanamke alisifika kama mama, mwanamke, mwangaza, mshindi na mtunzaji wa nyumbani kwake. Yeye ni mwenye uwezo wa kulisha jamii yake na ni yule anayependezeka. Inatupasa tumkumbuke mama kwani hakuna kitu kinachofananishwa naye kama wanavyofafanua wasanii. Kuna wasanii walioeleza kwamba kumekucha na tunataka mabadiliko na hata ingawa tunataka maziwa, si lazima tuwe na ndume.

## SURA YA TANO
## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sehemu hii ilishughulikia muhtasari wa utafiti huu kwa kueleza suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia iliyoongoza utafiti huu, deta iliyokusanywa na matokeo ya utafiti. Katika hitimisho, mtafiti alieleza matokeo ya utafiti, mafanikio ya utafiti na mapendekezo.

### 5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina sura tano kwa ujumla. Sura ya kwanza ilieleza kuhusu nyimbo za kampeni za kisiasa zinazotumika wakati wa uchaguzi wa kitaifa nchini Kenya. Sura hii ilieleza kuhusu matokeo ya uchaguzi mkuu nchini Kenya ya miaka 1992, 1997, 2002, 2007, 2013 na 2017. Vilevile, mambo yafuatayo yalishughulikiwa: Suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na maelezo ya istilahi. Utafiti ulichunguza namna jinsia inawakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya.

Sura ya pili ilishughulikia maandishi mbalimbali ya awali yanayohusiana na utafiti huu. Pia, mambo yafuatayo yalishughulikiwa: Nyimbo kwa jumla katika jamii, nyimbo za kisiasa katika harakati za uchaguzi, maandishi mengine kuhusu mada ya utafiti, dhima za nyimbo za kisiasa na nadharia ya Ubabedume iliyoongoza utafiti huu.

Sura ya tatu ilieleza kuhusu mbinu za utafiti. Maelezo kuhusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, ukusanyaji wa deta na uteuzi wa sampuli, vifaa vya ukusanyaji wa deta na uchanganuzi na uwasilishaji wa deta yalitolewa. Deta iliyokusanywa ilikuwa nyimbo za kampeni za kisiasa zilizoimbwa wakati wa uchaguzi wa kitaifa.

Sura ya nne ilieleza kuhusu uchanganuzi na ufasili wa deta. Mambo yafuatayo yalishughulikiwa katika sura hii ya nne: Mpangilio wa deta, maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa kuhusu jinsia, mgawanyo wa mamlaka, hitimisho ya sehemu hii, mahusiano ya uwezo kijinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa, siasa ya kijinsia, kinyang'anyiro cha kiti cha urais, sifo ya Muungano wa NASA, kampeni ya kiti cha ugavana, kampeni ya kiti cha useneta, kampeni ya kiti

cha ubunge, kampeni ya kiti cha ubunge wa wadi, hitimisho ya sehemu hii, itikadi kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa, itikadi za kisiasa kwa jinsia ya kiume, itikadi za kisiasa kwa jinsia ya kike na hitimisho ya sehemu hii.

Sura ya tano imeeleza kuhusu muhtasari, matokeo ya utafiti, mafanikio ya utafiti, hitimisho ya utafiti na mapendekezo.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Nyimbo nyingi zilizochanganuliwa na kufasiliwa ziliwatetea wagombezi wa jinsia ya kiume. Kati ya wasanii walioimba nyimbo hizo, wengi walikuwa wanaume. Wasanii wachache sana waliwapigia debe wagombezi wa jinsia ya kike. Kati ya wasanii wa kike walioimba, ni mmoja aliyemtetea mgombezi wa kike. Wagombezi wa jinsia ya kiume walikuwa wengi kuliko wa kike.

Kupitia nyimbo hizo tunajifunza mambo mengi kwani wasanii wanapobuni nyimbo zao, huwa hawaendi nje ya utamaduni wa jamii zao katika mazingira wanamokulia. Wasanii walieleza kuhusu nguvu za wagombezi kisiasa hasa kupitia sera zao. Wagombezi wengine wa kiume walitetewa na wasanii wawanie upya viti vya kisiasa. Nyimbo nyingi zilieleza kuhusu maendeleo kadhaa waliyofanya walipokuwa vitini. Hili ni jambo ambalo lingewashawishi wapiga kura wawapigie kura tena. Kulikuwa na wimbo mmoja ulioidhalilisha jinsia ya kike kwa kueleza kwamba gari likiwa mbioni, magurudumu ya nyuma hukimbiza ya mbele na hayatafikia kamwe. Kulingana na msanii huyo, magurudumu ya mbele husimamia jinsia ya kiume na ya nyuma husimamia ya kike. Huu ni mwelekeo chanya kwa mwanaume na mwelekeo hasi kwa mwanamke.

Kupitia nyimbo za kampeni za kisiasa, wanaume hupewa nguvu, uwezo, hadhi ya juu na mamlaka kuliko wanawake. Wanaume hutukuzwa zaidi kuliko wanawake katika jamii ya Kalenjin, jambo ambalo limewafanya wanawake wachache kuingia siasani. Sifa zifuatazo zinahusishwa na mwanaume kulingana na itikadi na utamaduni wa Kalenjin: Ni shujaa, ngao, moto, fahali, chuma, macho, baba, mtaalamu, mtetezi, mchungaji, mkarimu na yeye hana ubaguzi. Vilevile, nyimbo zilieleza kwamba yeye ni jasiri kwa sababu anaweza kumwua simba

anayenguruma, anaweza kumwua simba kama simba anasimama, hashtuliwi kwa ngozi, anaweza kuinua mlima, analinda pembeni, akilia hutegewa masikio na akilia mali yanafika nyumbani. Yeye ni 'Kipkutuny' yaani, anawezana na maadui kwani anajua mbinu za vita na hatishwi, hashtuliwi wala kutingishika. Yeye ni 'Koterkut' yaani, mtetezi wa watu hasa katika siasa. Yeye ni 'Kosilei' yaani, anashughulikia mambo makuu, anaendeleza uzazi, anawakilisha watu wengine katika jamii. Ni kama mti uliomo kando ya mto wa kulisha jamii, ni baba ya mayatima, analinda mali, anawalinda wanyonge, ana msimamo, ni mwenye hekima na hana mapendeleo.

Kuna wimbo mmoja ulioimbwa na msanii maarufu wa jamii ya Kalenjin marehemu Kipchamba Arap Tapotuk, ulioeleza kwamba mwanaume hapaswi kusikia maneno ya mwanamke kwani maneno yao hutoka kwenye akili ya kushoto ilhali ya mwanaume hutoka upande wa kulia. Maneno ya mwanamke yakisikilizwa, yatakosanisha watu katika jamii. Kupitia wimbo huu, imedhihirika kwamba hadhi ya mwanamke imeshukishwa na ya mwanaume imeinuliwa. Wakati wa kampeni, mwanaume anahimizwa kwamba akipata uongozi afuate mkondo fulani wa uongozi ambao mwanaume mashuhuri wa awali aliutumia.

Mwanaume anafananishwa na watu mashuhuri wapatikanao katika Bibilia takatifu. Anafananishwa na Musa aliyegonga maji ya Bahari Nyekundu akitumia fimbo hadi maji yakatawanyika kisha Wayaudi wakavuka. Anafananishwa na Yusuf kule Misri aliyewalisha watu wake wakati wa njaa kali. Kulingana na nyimbo hizo, inambidi mwanaume abarikiwe na wazee wa jinsia ya kiume namna mwana wa Jesse alibarikiwa kama tuelezwapo katika Biblia. Kuambatana na Ubabedume ambao umekithiri na kukolea katika akili za watu katika jamii, mwanaume anaonekana kana kwamba anastahili kutawala.

Kulingana na nyimbo hizo za kampeni za kisiasa, mwanamke hasawiriwi kuwa na uwezo mkubwa wa kutawala. Sifa zake zidhihirishwazo si za nguvu za kimwili ama za misuli. Wasanii wa nyimbo walikuwa wakimtetea wakieleza kwamba yeye anaweza kuwa kiongozi kwa sababu yeye ni mama. Yeye ana uwezo wa kulisha jamii, ana upendo, ni mwenye huruma, ni mnyenyekevu, mpole, mtulivu, mwaminifu, mkarimu na ni mtunzaji wa nyumbani kwake. Mama huletea jamii maendeleo makubwa kila mara daima kwani yeye ni mwaminifu. Mwanamke anaweza kufanya mambo makuu yeye mwenyewe bila usaidizi wa mwanaume kwani hata

anaweza kwenda vitani mwa kisiasa na kuwa mshindi. Vilevile, nyimbo zilieleza kwamba hakuna kitu kinachofananishwa na mama. Nyimbo nyingine zilitetea haki za mwanamke kwa kueleza uwezo wao. Nyimbo hizo zilifahamisha kwamba kumekucha na tunataka mabadiliko kuhusu jambo hili katika masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kifikra.

Katika jamii ya Kalenjin wanawake na watoto hujumlishwa kuwa sawa lakini ni wazi kwamba jambo kama hili limepitwa na wakati kuambatana na maelezo tuliyoyapata katika nyimbo za kampeni za kisiasa kuhusu jinsia ya kike. Jambo hili lilikuwa likitendeka ili mwanamke apate kuongozwa, kutawaliwa na kuelekezwa pamoja na watoto bila kuteta.

## 5.4 Mafanikio ya Utafiti

Utafiti huu umefanikiwa kuonyesha kwamba nyimbo nyingi ziliunga mkono taasubi za kiume. Kwa kueleza kwamba mwanaume ni mfano wa moto, anaweza kumwua simba anayenguruma au hukinga pembeni, husawiri ujasiri, nguvu na uwezo wake mwingi. Hizi ni sifa hasa za kimwili zihitajikazo katika jambo gumu kama vita. Kwa sababu nyimbo hizi zilikuwa zikilenga siasa, inamaanisha kwamba siasa yenyewe imefananishwa na vita na kwa hivyo inahitaji mtu mwenye sifa kama hizi. Mwanamke hawezi kuhusishwa na sifa kama hizi katika jamii. Hapo ndipo mwanaume atapata nafasi ya kupanda ngazi kisiasa akijilimbilizia mali. Mwanamke hajapewa nafasi ya kutosha na jamii  kufikia kiwango hicho. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba jamii inakuza na kuendeleza ubabedume.

## 5.5 Matatizo ya Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ya Bomet. Kulikuwa na changamoto kadhaa ambazo mtafiti alikumbana nazo akifanya utafiti huu. Haikuwa rahisi kupata deta ya kutosha siku moja na ikambidi atafute kwa muda. Ilikuwa vigumu kunukuu, yaani, kusikiliza na kuandika maneno ya nyimbo zenyewe. Mtafiti alifanya unukuzi huo kwa muda mrefu. Kutafsiri nyimbo zote alizokusanya kabla ya kuteua za kufanyia utafiti kulikuwa kugumu. Alizitafsiri nyimbo hizo akisaidiwa na baadhi ya wenyeji.

## 5.6 Hitimisho

Hitimisho ya utafiti ulitoa matokeo ya malengo yote matatu. Kulingana na lengo la kwanza, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri historia, itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu jinsia ya kike na ya kiume. Kulingana na nadharia ya Ubabedume, kiutamaduni, wanaume hufundishwa katika jamii wawe viongozi hasa wa wanawake. Kisaikolojia, wanaume hutakikana wawe jasiri na wasionyeshe uwoga lakini waweze kulinda wanyonge hasa wanawake na watoto.

Kuambatana na namna jinsia imewakilishwa katika nyimbo tisa za kampeni za kisiasa, wagombezi wa kiume waliogombea viti mbalimbali vya kisiasa walikuwa wengi kuliko wa kike. Jambo hili linadhihirisha kuwa ubabedume umedumishwa katika jamii ilhali ubabejike bado unajitafutia nafasi kwa umbali. Kwa mfano, tazama wimbo nambari kumi na moja. Vilevile, wasanii walieleza kuhusu maendeleo yaliyofanywa na wagombezi wa kiume waliotaka kuwania viti vya kisiasa tena. Hii ni njia moja ya kuendeleza utawala wa wanaume. Wanawake bado wananyimwa nafasi ya uongozi kisiasa katika jamii ambapo itikadi inayotawala inawakuza wanaume.

Lengo la pili, matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba wanaume wamesawirika kuwa mashujaa ambao wanamiliki nguvu na mamlaka ndipo jamii ikawainua wawe wa hadhi ya juu kuliko wanawake. Viashiria kadhaa vilivyotumika katika nyimbo za kampeni za kisiasa kama vile moto, simba, fahali, ngao au chuma zinaashiria nguvu ya mwanaume na kumsahau mwanamke. Maneno haya husawiri ujasiri na nguvu za kivita, jambo ambalo ni tofauti na siasa. Mwanaume amepewa uwezo mkubwa na jamii ambao umemwezesha kupanda ngazi kiutawala. Anapiga hatua kujilimbikizia mali, tendo lililo kinyume kwa jinsia ya kike.

Kulingana na lengo la tatu, matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba nyimbo za kampeni za kisiasa zinafahamisha namna jamii huratibu majukumu kijinsia. Jambo hili hutokana na matarajio ya kiitikadi na utamaduni kuhusu jinsia zote mbili. Kuna sifa anuwai zinazomkweza mwanaume, jambo lililodumisha taasubi za kiume. Kumfananisha na watu maarufu katika Biblia kama Daudi, Musa na Yusufu ni namna ya kuujenga na kuupa nguvu zaidi ubabedume ulioshika mizizi duniani. Itikadi ya kisiasa kwa jinsia ya kike imesawiri mwanamke kama mama, mtunzaji

wa nyumbani kwake, mwenye uwezo wa kulisha jamii yake, mwangaza na sifa nyingine zisizoakisi nguvu au uwezo wake hususan wa kimwili. Wasanii wachache waliutukuza ubabe-jike wakieleza kuwa kumekucha na mabadiliko yanahitajika. Jambo hili litafanikiwa iwapo litatiliwa mkazo na taasisi mbalimbali za jamii.

## 5.7 Mapendekezo

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba nyimbo nyingi za kampeni za kisiasa zilitetea jinsia ya kiume. Nyimbo hizo zilipatia hadhi ya juu jinsia ya kiume kuliko ya kike. Viashiria vingi vya nyimbo hizo vilisawiri nguvu na uwezo wa mwanaume. Huu ni mwelekeo chanya kwa mwanaume na hasi kwa mwanamke. Kwa kuzingatia matokeo hayo, mtafiti apendekeza kwamba yapasa jamii ielimishwe kupitia sanaa kuhusu uwezo wa jinsia ya kike katika uongozi wa siasa na usawa wa jinsia katika asasi nyingine za jamii. Mtafiti apendekeza kuwa wasanii wahamasishwe wabuni na kuwaimbia wanawake nyimbo za kuwaunga mkono na kuwapa motisha katika siasa jinsi wanaume wanavyoimbiwa. Pia, apendekeza kuwa wasanii wa jinsia ya kike wahimizwe kuimba nyimbo za kisiasa wakilenga wagombezi wa kike ili kuwapa moyo kwani wanawake kwa wanawake huelewana.

Kwa mujibu wa lengo la kwanza, nyimbo za kampeni za kisiasa zilidhihirisha kwamba wanawake bado wananyimwa nafasi ya uongozi siasani katika jamii. Mtafiti apendekeza kwamba utafiti ufanywe kuhusu namna jinsia ya kike husawirika kupitia maongezi na majadiliano katika mikutano ya kampeni za kisiasa. Maongezi na majadiliano hayo yanaweza kuwa ya wagombezi wa jinsia ya kiume na kike, kila mmoja akiwa na wafuasi na wapinzani wakeo.

Kwa mujibu wa lengo la pili, matokeo ya utafiti yameonyesha kwamba nyimbo za kisiasa zimehusisha mwanaume na ujasiri, nguvu na mamlaka katika jamii lakini mwanamke ameelezwa kama mama, mwanamke, mwangaza na mtunzaji wa nyumbani kwake. Mtafiti apendekeza kwamba utafiti zaidi ufanywe kuchuguza namna ya kusawasisha uwezo wa mwanaume na mwanamke kupitia vyombo vingine vya kijamii na wala sio nyimbo pekee.

Kwa mujibu wa lengo la tatu, matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa jamii, kupitia nyimbo za kampeni za kisiasa, imeratibu majukumu ya kila jinsia. Hayo matokeo yamepatikana kupitia nadharia ya Ubabedume. Mtafiti apendekeza kwamba utafiti ufanywe kwa kutumia nyimbo kuchunguza nama jamii imeratibu majukumu kwa kutumia nadharia ya Ufeministi.

## MAREJELEO


Aldin, K. M. (2005). *Kisiki Kikavu*. Dar es Salaam: E & D Ltd.

Alex, Z. (1996). *Different Drummers*: *Using Music to Teach History*. San Diego: National University of San Diego.

Aswani, B., Mayaka, G., & Riro, M. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Boller, P. F. Jr. (1984). *Presidential Campaigns*. New York: Oxford University Press.

Carrigan, T., Connel, R., & Lee, J. (1985). 'Toward a New Sociology of Masculinity .' in H. Brod Editor. *The Making of Masculinities*. *The New Men Studies*: Boston

Chapman, R., & Rutherford, J. (1988). Editors. *Male Order: Unwrapping Masculinity*. London.

Chiuri, J. (1984). *Pob Music as a Form of Oral Literature on Joseph Kamaru*. Tasnifu ya PGDE: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Christine, M. (2015, April 14). *The African Women who Tried for President – and how they Fared.* Retrieved from http:/mgafrica.com/article/2015-04-13-fortunes-of-women-presidential-candidates.

Commonwealth Observer Group. (2013). 'Report of the Commonwealth Observer Group. Kenya General Elections'.

Connell, R. (1983). *Which Way is Up*. Newbury-Park: Sage Publications.

Connell, R. (1987). *Gender and Power: Society, the Person and Sexual Politics.* Newbury-Park: Sage Publications.

Connell, R. (1990). An *Iron Man*: *The Body and Some Contadictions of Hegemonic Masculinity.* Newbury-Park: Sage Publications.

Connell, R., & James, W. M. (2005) *Hegemonic Masculinity : Rethinking the Concept. Gender and Society*. New York and London: Routledge.

County Government of Bomet. (2018). *County integrated Development Plan 2018-2022*. Retrieved from https://cog.go.ke.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative,Quantitative and Mixed Methods Approaches*. Thousand Oaks, CA: Sage Publication.

David, K. D., & Willa, K. B. (1996). *Oral History*. Washington: Alta Mira Press.

DDDG. (1998). *Final Report*: Kenya General Elections 1997 (Nairobi: The Donors' Democratie Development Group).

Deacon, D., Piickering, M., Golding, P., & Murdock, G. (1999). *Researching Communications*. London: Anorld Ltd.

Deane, P. (2005). *The Ethics of Social Engagement*: *Learning to Live and Living to Learn*. London: Earthscan Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. London Longman.

Fediman, J. (1993). *When we Began there were Witchmen*: *An Oral History from Mount Kenya*. California: University of California Press.

Fiske, J., Hodge, B., & Turner, G. (1987). Myths of Oz: *Reading Australian Popular Culture.* Sydney: Allen and Unwin.

Frosh, S., Phoenix, A., & Patman, B. (2004). *Young Masculinities: Understanding Boys in Contemporary Society*. New York; Palgarave.

Hochschild, A., & Machung A., (1989). *The Second Shit: Woking Parents and the Revolution at Home.* New York: Viking.

Holmes, J. (1997). Women, Language and Identity. *Journal of Sociolinguistics*, 195-223.

Isidore, O. (1992). *African Oral Literature*. Bloomington & Indianapolis: Indiana University Press.

Izugbara, C. O. (2005). 'Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity', In *Sexuality in African Magazine*. Lagos: Africa Regional Sexuality Resource Centre 2(1) 13-14.

Habermas, J., & McCarthy, T. (1977). *A Critique of the Critics.* John Hopkins University Press.

Kimani, N., & Maupeu, H. E. (2007). *Songs and Politics in Eastern Africa*. Nairobi: Africa Books Collective.

Kimmel, M. (1997). 'Masculinity as Homophopia: Shame and Silence', in Harry Brod and Micharel Kaufam. *Theorizing Masculinities*. New York: Sage Publications.

King'ei. (1992). *Language*, *Culture and Communications*: The Role of Taarab Songs in Kenya: Howard University.

Koma, T. (1984). *The Women's Self-Help Association Movement Among the Kipsigis of Kenya.* Senri Ethnological Studies no. 15. Osaka: National Museum of Ethnology

Levant, R. F., Thomas, J. R., & Williams, C. M. (2010). Evaluation of the Factor

Structure and Contract Validity of Scores on the Male Role, Norms Inventory-Revised. *Psychology of Men and Masculinity*.

Maclaughlin, A., Braxton. (1990). *Wild Women in Whirlwing: Afro American Culture and Contemporary Literacy Renaissance*. New Brunswick: Rutgers University Press.

Matinde, R., Aswani, B., & Mayaka, G. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Matu., Wanjiku, A. (2012). *Uwezo wa Muziki Katika Siasa ya Kenya*. Haijachapishwa.

Mayaka, G., Aswani, B., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili. Peramiho*: Benedictine Publications Ndanda.

Mazrui, A. M., & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbogo, F. (2008) *How President Daniel Arap Moi used Power of Choral Music to Rule Kenya.* Unpublished.

Mdee, J. S., Njogu, K., & Shafi A. (2011*). Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers (Ltd).

Messner, M., & Sabo, D. (1990). *Sport, Men and the Gender Order*: *Critical Feminist Perspectives*, Illonois Human Kinetics.

Millet, K. (1978). *Sexual Politics*: London. Verso London: Routledge.

Mhatre, M. (2009). *Women in Electoral Politics*: A Case Study of Women's Political Participation in Maharashtra.

Miles, J. F. (1990). *Traditional Oral Epic*. California: University of California.

Miruka, O. (1999). *Studying Oral Literature* . Nairobi: Acacia Publishers.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*: Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Newman, P. S. (1997). *Parades and the Poiltics of Streets*. Pennsylvania: University of Pennsylvania Press

Norm, C. (2005). *A Folk Music*: *A Regional Exploration*. New York: Greenwood Publishing Group.

Obenga, T. (2004). *African Philosophy: The Pharaonic Period, 2780-330 BC.* Popenguine: Per Ankh.

Paul, C. (1991). *Labour and Poverty in Rural Tanzania*: *Ujamaa and Rural Development in the United Republic of Tanzania*. New York: Oxford University Press.

Richmond, A. M. (1992). *Masculine and Feminine: Gender Roles Over the Life Cycle*. New Delhi : Sage Publications.

Riordan, L. (2007). *The American Revolution and its Legacy in the Mid-Atlantic.* University of Pennsylvania Press.

Robert, J. D. (1989). *Campaigning in America: A History of Election Practices*. New York: Greenwood Prees.

Sakawa, D. K. (2012). Entertainment, Education and Communication Strategy in Tanzania:*The Efficacy and Efficiency of Bongo Flava Television Programs in Youth Behaviour Influence*. Saarbrucken, Germany: LAP Lambert Academic Publishing.

Samwel, M. (2010/2011). Masuala ya Kisiasa Katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo Fleva. *Mulika Toleo Maalumu la Muziki wa Kizazi Kipya, 29*, 17-18.

Sattel, J. (1983) Men, Inexpressiveness, and Power. In: *Language, Gender and Society,* Barrie Thorne, Cheris Kramarae and Nancy Henley (eds.) pp. 119-124, Massachusetts; Newbury House.

Schwandt, T. A. (2000). *Three Epistemological Stances for Qualitative Inquiry: Interpretivism, Hermeneutics and Social Constructivism*. In N. K. Denzin & Y. S. Lincoln (Eds.), Handbook of Qualitative Research (2nd ed., pp. 189-214). Thousand Oaks, CA: Sage.

Sengo, T. S. Y., & Kiango, S.D. (1973) *Hisi Zetu.* 1. TUKI: Dar es Salaam

Shokpeka, A. (1999) Women in the History of Pre-colonial Nigeria: *The Example of Women in Edo State.* Nsuka Journal of the Humanities 12:108-119.

Simatei, P. (2010). Kalenjin Popular Music and the Contestation of National Space in Kenya. *Journal of Eastern African Studies, 4,* 425-434.

Sisanda, M. N. (2013). *Songs that shaped the Struggle*: *A Rhetorical Analysis of South African Struggle Songs*. Unpublished.

Smith, J. E. (2012). *Eisenhower in War and Peace***.** New York: Random House.

Tannen, D. (1990). *You Just Don't Understand: Women and Men in Conversation*. New York: Ballantine Books.

Uchendu, V. (1965). *The Igbo of South Eatern Nigeria*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Uchendu, E. (2005). '*Masculinities from Perspectives of Youth'* Paper Presented at the Gender Institute-CODERSIA.

Sturmer, M. (1998). *The Media History of Tanzania*. Salzburg: Afro-Asiatiches Intitute.

Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walsh, M. R. (1997). *Women, Men and Gender: Ogoing Debates*. London: Yale University Press.

Wambua, M. S. (2001). *Mtindo wa Nyimbo za Kakai Kilonzo* Tasnifu ya M.A. Kenyatta University: Haukuchapishwa.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Simulizi Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Folk Literature*. Dar es Salaam: Focus Publication.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Waters, M. (1989*). 'Patriachy and Viriarchy: An Exploration and Reconstruction of Concepts of Masculine Domination.* New York: Viking.

Whitehead, S. M. (2003). *Men and Masculinities: Key Themes and New Directions*. Malden, M.A: Blackwell Publishers.

William, S. B. (2012). *Winning Political Campaigns*. New York: Denali Press.

## Kiambatisho A: Ramani ya Kaunti ya Bomet



**Kiambatisho B: Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Jinsia**

***(i) WANAUME***

***1. <u>MSANII:JEREMIAH KOSGEI</u>***

| ***JUBILEE*** | ***JUBILEE.*** |
|---|---|
| *Kokiyokten Samoei Arap Ruto.* | *Tuna kutuma Samoei Arap Ruto.* |
| *Asiimutwech Uhuru konyo* | *Uende utuletee Uhuru aje Nyumbani* |
| *Kapkatet x 2.* | *Kapkatet x2* |
| *Si kikochin mwaita nebo Kalenjin x2* | *Ili tumtakase na mafuta ya Kalenjin x 2.* |
| *Kou werikab Jesse chemi Bible x 2.* | *Kama wana wa Jesse katika Bibilia x 2.* |
| *Si koribwech emet x 2.* | *Yeye apate kutulindia nchi x2.* |

***2. <u>MSANII: SHUTTLE SISTERS</u>***

| ***URP*** | ***URP*** |
|---|---|
| *Nyigamenyon Ruto koriborjige.* | *Shujaa wetu Ruto, amejitahidi.* |
| *Kotiboru chamaitab URP x2.* | *Hadi akaunda chama cha URP.* |
| *Arap Ruto ko chorwet ab chi tugul.* | *Arap Ruto ni rafiki ya kila mtu.* |
| *Momi bororiet Kenya ne moingen kainetab Samoei.* | *Hakuna jamii nchini Kenya isiyolitambua jina la Samoei.* |
| *Kisaun kot indochi emenyon Kenya.* | *Tunakuombea hadi uongoze nchi yetu ya Kenya.* |
| *Ye indochi emenyon ibur kou Baba Moi.* | *Utakapoongoza nchi yetu, ukae kama Baba Moi.* |

***3. MSANII: CHERES DANIEL***

| ***JUBILEE*** | ***JUBILEE*** |
|---|---|
| *Kitinye keljinet en Kenya ketinye kondoik che mokibestos.* | *Tunayo bahati nchini Kenya kuwa na viongozi wasiotenganishwa.* |
| *Kondoik che chame kalyet matiny komi bolet.* | *Viongozi wanaopenda amani hata kama kuna siasa.* |

*Matiny komi bolet koribe emenyon komobet kalyet.*
*Ko rokendoen ketit ne mi tabandab oinet.*
*Ketit ne tinye temet, temet ne boe emet.*
*Temet netinye kimnatet.*
*Temoni ko nenyon Kalenjin.*
*Ongikutyin ng'ung'unyat temoni si ye kayosit keti ketinye ne nome boisiet.*
*Kiboe che ome rubet, kityoche che kigagirat.*
*Kisobe che kikikikoten, nyoru kiy che matindo kiy.*
*Oribech asi keribok.*
*Miten bik che moimucheke.*
*Osome toretet koyobun nyiganetab Kalenjin.*

*Hata kama kuna siasa, wanachunga nchi yetu amani isivurugike.*
*Nalinganisha na mti ulio kando ya mto.*
*Mti ulio na tawi, tawi linalolisha nchi.*
*Tawi lililo na nguvu.*
*Tawi hili ni letu Wakalenjin.*
*Tupalilie mti huu halafu ukizeeka tutakuwa na wa kushika usukani.*
*Walishe walio na njaa,waliofungwa wafunguliwe.*
*Waponywe walioumizwa,wasio na chochote watapata.*
*Mtuchunge halafu tuwachunge.*
*Kuna wale wasiojiweza.*
*Naomba usaidizi kutoka shujaa wa Wakalenjin.*

***4. WASANII: CCM WOMEN***

***<u>KIBO CCM</u>***
***<u>(CHAMA CHA MASHINANI)</u>***
*Kongoi inye kirginyon o Mashinani kityo.*
*Mokichomndoi kesilwech, Mashinani kityo.*
*Kichome echek nyiganet o Mashinani kityo.*
*Kongoi nyiganet neu mat Mashinani kityo.*
*Ne kikegas en Kenya Mashinani kityo.*
*Kole makiwole kora Mashinani kityo.*

***<u>SISI NI WACCM</u>***
***<u>(CHAMA CHA MASHINANI)</u>***
*Asante fahali yetu o Mashinani pekee.*
*Haturuhusu aumizwe, o Mashinani pekee.*
*Twampenda shujaa wetu o Mashinani pekee.*
*Asante shujaa mfano wa moto o Mashinani pekee.*
*Amejulikana nchine Kenya o Mashinani pekee*
*Haibadilishwi tena o Mashinani pekee.*
*pekee.*

***5. MSANII: ARUMUTIK KOSGEI***

***PROFESA WILLIAM LESAN***

